# Kiswahili

## kwa

## Shule za Rwanda

## Mchepuo wa Lugha

## Kitabu cha Mwanafunzi

## Kidato cha 6


Sylvain Ntawiyanga
Jacqueline M. Kinya
Ali Muhamud
Sanja Leonard



LONGHORN
PUBLISHERS LIMITED
expanding minds

Kimechapishwa na:

Longhorn Publishers (Rwanda) Ltd
Remera mkabala na Benki ya COGE
S.L.P. 5910
Kigali, Rwanda

Longhorn Publishers (Kenya) Ltd.,
Barabara ya Funzi, Eneo la Viwandani
S.L.P. 18033–00500
Nairobi, Kenya

Longhorn Publishers (Uganda) Ltd
Ploti 4 Vubyabirenge, Ntinda
S.L.P. 24745
Kampala, Uganda

Longhorn Publishers (Tanzania) Ltd.
Barabara Mpya ya Bagamoyo/Garden,
Mikocheni B, Ploti Namba: MKC/MCB/81
S.L.P 1237, Dar es Salaam, Tanzania

© S. Ntawiyanga, J. M. Kinya, A. Muhamud, S. Leonard 2017

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupigisha chapa, kutafsiri au kukitoa kitabu hiki kwa jinsi yoyote ile bila idhini, kwa maandishi ya Longhorn Publishers Ltd.

Chapa ya kwanza 2017

**ISBN 978 9997 77 132 2**

Kimepigwa chapa na Ramco Printing Works Ltd,
Unit 2, Ramco Industrial Complex,
Barabara ya Mombasa, Eneo la Viwandani,
S. L. P. 27750 - 00506, Nairobi.

# Yaliyomo


SURA YA KWANZA ........................................................................ 1

MADA KUU 1: FASIHI KATIKA KISWAHILI................................ 1

MADA NDOGO: Ufafanuzi wa tanzu za fasihi andishi katika Kiswahili ........................................................ 1

Somo la 1: Fasihi andishi ........................................................... 1

1.1 Kifungu kuhusu tanzu za fasihi andishi ................................................ 1

1.2 Msamiati kuhusu tanzu za fasihi andishi ............................................... 4

1.3 **Matumizi ya lugha:** Umuhimu wa fasihi andishi ............................... 5

1.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Majadiliano ......................................... 5

1.5 **Sarufi:** Maana ya sentensi ...................................................................... 6

1.5.1 Sehemu kuu za sentensi ........................................................................... 7

Somo la 2: Utanzu wa hadithi fupi................................................ 11

2.1 Hadithi fupi kuhusu uhifadhi wa mazingira ......................................... 11

2.2 Msamiati wa hadithi fupi kuhusu uhifadhi wa mazingira ..................... 13

2.3 **Matumizi ya lugha:** Majadiliano kuhusu uhifadhi wa mazingira ..... 14

2.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Sifa bainifu za hadithi fupi .................. 16

2.5 **Sarufi:** Maana ya kirai ............................................................................ 16

Somo la 3: Utanzu wa riwaya ...................................................... 19

3.1 Sura moja ya riwaya kuhusu uchaguzi wa viongozi ............................. 19

3.2 Msamiati kutokana na sura moja ya riwaya husika .............................. 23

3.3 **Matumizi ya lugha:** Sifa bainifu za riwaya ........................................ 24

3.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Majadiliano kuhusu maudhui ............ 24

3.5 **Sarufi:** Kirai kivumishi ............................................................................ 25

**Somo la 4: Utanzu wa tamthilia ........ 28**
4.1 Sura moja ya tamthilia ........ 28
4.2 Msamiati kutokana na sura moja ya tamthilia husika ........ 34
4.3 **Matumizi ya lugha:** Sifa bainifu za tamthilia ........ 35
4.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Maigizo ........ 36
4.5 **Sarufi:** Kirai kitenzi ........ 37

**Somo la 5: Utanzu wa ushairi ........ 40**
5.1 Shairi kuhusu kuyalinda mazingira ........ 40
5.2 Msamiati wa shairi kuhusu kuyalinda mazingira ........ 42
5.3 **Matumizi ya lugha:** Sifa bainifu za shairi ........ 42
5.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Kukariri shairi ........ 43
5.5 **Sarufi:** Maana ya kishazi ........ 43
Tathmini ya mada ya 1 ........ 46
Faharasa ........ 49

**SURA YA PILI ........ 50**
**MADA KUU 2: FASIHI KATIKA KISWAHILI ........ 50**
**MADA NDOGO: Uhakiki wa tanzu za fasihi andishi ........ 50**

**Somo la 6: Uhakiki wa fasihi ........ 50**
6.1 Kifungu kuhusu fasihi katika Kiswahili ........ 50
6.2 Msamiati kuhusu fasihi katika Kiswahili ........ 52
6.3 **Matumizi ya lugha:** Uhakiki wa maudhui katika fasihi ........ 53
6.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Majadiliano ........ 54
6.5 **Sarufi:** Maana ya kitenzi ........ 54

**Somo la 7: Wahusika katika fasihi andishi** ........ **58**
7.1 Hadithi fupi kuhusu urithi wa mali ........ 58
7.2 Msamiati kutokana na hadithi fupi husika ........ 63
7.3 **Matumizi ya lugha:** Aina mbalimbali za wahusika ........ 64
7.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Tabia na sifa za wahusika ........ 64
7.5 **Sarufi:** Kauli ya kufanyiwa/kutendewa ........ 65

**Somo la 8: Maudhui na dhamira katika fasihi andishi** ........ **68**
8.1 Shairi kuhusu ukulima ........ 68
8.2 Msamiati kutokana na shairi husika ........ 70
8.3 **Matumizi ya lugha:** Uhakiki wa maudhui na dhamira ........ 71
8.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Majadiliano ........ 71
8.5 **Sarufi:** Kauli ya kufanyisha/kutendesha ........ 72

**Somo la 9: Mandhari katika fasihi andishi** ........ **75**
9.1 Sura moja ya tamthilia yenye mandhari mbalimbali ........ 75
9.2 Msamiati kutokana na maonyesho ya tamthilia husika ........ 79
9.3 **Matumizi ya lugha:** Majadiliano kuhusu mandhari ........ 79
9.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Majadiliano ........ 80
9.5 **Sarufi:** Kauli ya kufanywa/kutendwa ........ 80

**Somo la 10: Uhakiki wa mbinu za lugha katika fasihi** ........ **83**
10.1 Sura moja ya riwaya yenye mbinu za lugha ........ 83
10.2 Msamiati kutokana na sura ya riwaya husika ........ 86
10.3 **Matumizi ya lugha:** Majadiliano kuhusu mbinu za lugha ........ 87
10.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Majadiliano ya mbinu za lugha ........ 88
10.4.1 Uhakiki wa waandishi mashuhuri wa fasihi ya Kiswahili ........ 88
10.5 **Sarufi:** Kauli ya kufanyua/kutendua ........ 89
Tathmini ya mada ya 2 ........ 91
Faharasa ........ 93

**SURA YA TATU** ........................................................................ **94**

**MADA KUU 3: UBUNAJI** ........................................................... **94**

**MADA NDOGO: Hotuba na ufupisho** ........................................... **94**

**Somo la 11: Sehemu kuu za hotuba** ............................................ **94**

11.1 Hotuba kuhusu usafi .................................................................... 94

11.2 Msamiati wa hotuba kuhusu usafi ................................................... 97

11.3 **Matumizi ya lugha:** Majadiliano ................................................ 98

11.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Kutunga hotuba ................................. 99

11.5 **Sarufi:** Uambishaji wa vitenzi ...................................................... 99

**Somo la 12: Sifa za hotuba** ............................................................ **102**

12.1 Hotuba kuhusu ushirikiano wa kijinsia ............................................ 102

12.2 Msamiati kutokana na hotuba ya ushirikiano wa kijinsia .................... 105

12.3 **Matumizi ya lugha:** Majadiliano kuhusu sifa za hotuba..................... 105

12.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Majadiliano ......................................... 106

12.5 **Sarufi:** Uambishaji wa vitenzi ...................................................... 106

**Somo la 13: Hotuba na insha** ......................................................... **110**

13.1 Hotuba kuhusu kupigana na umaskini................................................ 110

13.2 Msamiati kutokana na hotuba husika ................................................ 113

13.3 **Matumizi ya lugha:** Tofauti kati ya hotuba na insha ........................ 113

13.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Kutunga hotuba ................................. 114

13.5 **Sarufi:** Viambishi tamati ............................................................... 114

**Somo la 14: Ufupisho** ...................................................................... **116**

14.1 Hotuba kuhusu umuhimu wa maadili ................................................ 116

14.2 Msamiati kutokana na hotuba ya umuhimu wa maadili ...................... 119

14.3 **Matumizi ya lugha:** Majadiliano kuhusu sifa za ufupisho ................ 120

14.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Kufupisha hotuba ............................... 120

14.5 **Sarufi:** Uundaji wa nomino kutokana na vitenzi ................................ 121

**Somo la 15: Mwongozo wa kuandika ufupisho ............................ 123**
15.1 Hotuba kuhusu manufaa ya elimu ........................................................ 123
15.2 Msamiati wa hotuba kuhusu manufaa ya elimu .................................... 126
15.3 **Matumizi ya lugha:** Majadiliano kuhusu mwongozo wa kuandika ufupisho ............................................ .126
15.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Kufupisha hotuba ................................ 127
15.5 **Sarufi:** Uundaji wa vitenzi jina ........................................................ 127
Tathmini ya mada ya 3 ................................................................. 129
Faharasa ..................................................................................... 131

**SURA YA NNE ....................................................................... 132**
**MADA KUU 4: UKUZAJI WA MATUMIZI YA LUGHA KIMAZUNGUMZO ........................................ 132**
**MADA NDOGO: Midahalo na mijadala ..................................... 132**

**Somo la 16: Sifa za mdahalo ...................................................... 132**
16.1 Mdahalo kuhusu athari za mavazi ya kisasa ........................................ 132
16.2 Msamiati kutokana na mdahalo husika ................................................ 135
16.3 **Matumizi ya lugha:** Sifa bainifu za mdahalo .................................... 136
16.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Maigizo ................................................ 137
16.5 **Sarufi:** Maana ya nomino ................................................................ 137
16.5.1 Uundaji wa nomino ........................................................................ 138

**Somo la 17: Mwongozo wa kuandika mdahalo ............................ 141**
17.1 Mdahalo kuhusu athari za rushwa ...................................................... 141
17.2 Msamiati kutokana na mdahalo husika ................................................ 144
17.3 **Matumizi ya lugha:** Majadiliano ...................................................... 145
17.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Kutunga mdahalo ................................ 145
17.5 **Sarufi:** Maana ya kivumishi ............................................................ 145
17.5.1 Uundaji wa vivumishi .................................................................... 148

**Somo la 18: Mjadala** .................................................................. **150**

18.1 Mjadala kuhusu umuhimu wa uzalendo ................................................ 150

18.2 Msamiati kutokana na mjadala husika ................................................ 152

18.3 **Matumizi ya lugha:** Sifa bainifu za mjadala ...................................... 153

18.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Maigizo ................................................ 154

18.5 **Sarufi:** Maana ya kitenzi ......................................................................... 154

18.5.1 Uundaji wa vitenzi ..................................................................................... 155

**Somo la 19: Mwongozo wa kuandika mjadala** ............................... **157**

19.1 Mjadala kuhusu ugonjwa wa Ukimwi .................................................... 157

19.2 Msamiati kutokana na mjadala husika ................................................ 161

19.3 **Matumizi ya lugha:** Majadiliano ........................................................ 161

19.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Kutunga mjadala ................................. 162

19.5 **Sarufi:** Maana ya kiwakilishi ................................................................ 162

19.5.1 Uundaji wa viwakilishi ............................................................................. 164

Tathmini ya mada ya 4 ................................................................................ 165

Faharasa ........................................................................................................ 167

Vitabu vya Rejea ........................................................................................... 168

# UTANGULIZI

## Nafasi ya Kiswahili katika jamii na mfumo wa elimu

Lugha ya Kiswahili imepewa hadhi kubwa kwa kuteuliwa kuwa mojawapo katika lugha rasmi za Jumuiya ya Afrika. Nchini Kenya na katika nchi ya Tanzania, Kiswahili ni lugha ya taifa na pia lugha rasmi. Nchi za Uganda na Burundi nazo hazijaachwa nyuma kwani lugha ya Kiswahili imeanza kukita mizizi huko na kufunzwa kikamilifu. Nchini Rwanda, Kiswahili ni lugha rasmi.

Nchi nyingine kama Marekani, Ujerumani na mataifa mengi ya Ulaya yameanza kufunza lugha ya Kiswahili katika vyuo vikuu. Wanaelewa kuwa Kiswahili ndiyo lugha inayoweza kuunganisha nchi za ng'ambo na Afrika. Lugha hii huwafaa sana watalii wanaozuru Afrika.

Mipango imefanywa ili kuhakikisha kuwa lugha ya Kiswahili inawekwa katika programu za tarakilishi na kwenye mtandao duniani kote. Ni wazi kuwa Kiswahili kinapiga hatua kwa kasi sana ili kuweza kwenda na wakati.

## Kiswahili katika mfumo wa elimu nchini Rwanda

Somo la Kiswahili limekuwa likifundishwa katika viwango vya elimu vya sekondari nchini Rwanda. Kwa sasa, somo hili linatathminiwa kitaifa kwa wanafunzi wanaosoma Kiingereza, Kiswahili na Kinyarwanda.

Lugha ya Kiswahili imepewa nguvu zaidi hasa tukizingatia kuwa wanafunzi wengi hulichukua somo hili katika sekondari na vyuo vikuu na kupata mafunzo katika fasihi na isimu na kufuzu katika somo hili. Tukitilia maanani mambo haya yote, tutaona kuwa wizara ya elimu imeipa lugha ya Kiswahili heshima inayostahili na kuhakikisha kuwa lugha hii inakuzwa.

**Stadi mbalimbali zilizoshughulikiwa katika kitabu hiki:**

### a) Ufahamu

Ufahamu ni kipengele muhimu katika lugha ya Kiswahili. Ufahamu umebeba stadi zote zinazoweza kushughulikiwa kama vipengele tofauti tofauti.
Katika kusoma fahamu zilizopo humu ndani, wanafunzi watatazama michoro iliyo katika vitabu vyao na kuelezana wanachokiona kisha wasome fahamu husika. Ni muhimu wanafunzi wasome fahamu kwa sauti huku wakipokezana kwa zamu. Wanafunzi wajibu maswali ya ufahamu baada ya kuusoma.

Wanafunzi katika kiwango hiki wanapaswa kuwa wanajua kusoma kwa ufasaha. Katika usomaji, wanafunzi wahakikishe kuwa hawasogezi vitabu karibu sana na macho na pia hawatumii vidole kuelekeza macho. Huu ni usomaji mbaya usiofaa kuwepo.

### b) Msamiati

Wanafunzi wanaweza kutumia vifaa halisi katika kueleza maana na matumizi ya msamiati kama vile kamusi za Kiswahili.

### ch) Kusikiliza na kuzungumza

Kusikiliza na kuzungumza ni kipengele muhimu sana katika kujifunza lugha yoyote ile. Ni wazi kuwa mtu ambaye hajapata kusikia neno lolote, yaani alizaliwa kiziwi, kamwe hawezi kuongea. Ataongea akisema nini? Binadamu yeyote alijifunza kuongea kupitia kwa kuwasikiliza watu wengine wakiongea na maneno ya kwanza aliyoyazungumza ni yale aliyoyasikia.

Wanafunzi wajifundishe funzo la kusikiliza na kuzungumza kwa kuigiza michezo ya kuigiza na kuwasilisha kazi za makundi darasani. Wanafunzi wanaweza pia kuandaa mijadala na midahalo na kuiwasilisha mbele ya wanafunzi wenzao.

### d) Sarufi

Sarufi ni mpangilio maalum wa maneno kwa ufasaha kulingana na kanuni zake au kupanga na kutumia maneno vizuri kulingana na mipango au taratibu zilizokubaliwa kuwa ni sahihi. Sehemu muhimu katika sarufi ni ngeli. Mtu yeyote asiyejua na kuzitawala ngeli kamwe hawezi kusema kuwa anaielewa lugha ya Kiswahili. Atakuwa akitudanganya. Sarufi pia hujumuisha sehemu muhimu kama vile: matamshi, majina, vielezi, vitenzi, viambishi, uakifishaji, nyakati, vivumishi, mnyambuliko wa vitenzi n.k.

### e) Kuandika

Katika kuandika, wanafunzi wahakikishe wanaandika kwa hati nadhifu na inayosomeka kwa urahisi. Kila herufi iandikwe vizuri. Uakifishaji bora uzingatiwe.

Wanafunzi wanaweza kuandika insha mbalimbali, mijadala, midahalo, mashairi n.k.


# SURA YA KWANZA

**MADA KUU 1:** **FASIHI KATIKA KISWAHILI**
**MADA NDOGO:** **Ufafanuzi wa tanzu za fasihi andishi katika Kiswahili**

## Somo la 1: Fasihi andishi

### 1.1 Kifungu kuhusu tanzu za fasihi andishi

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tazameni mchoro huu kisha msome kifungu cha habari kinachofuata kuhusu ufafanuzi wa tanzu za fasihi andishi, umuhimu wake pamoja na sifa zake na baadaye mjibu maswali ya ufahamu yanayofuata.*




Fasihi andishi ni moja kati ya tanzu za fasihi ya lugha ya Kiswahili. Hii ni aina ya sanaa ambayo msanii au mtungaji hutumia maneno ambayo huandikwa kwa lengo la kupitisha ujumbe. Ni sanaa ambayo hutengenezwa kiufundi kwa njia ya maandishi ya aina mbalimbali. Ni aina ya sanaa ambayo hueleza maisha ya binadamu kwa ujumla na hujikita katika maadili na shughuli zote za watu. Katika sanaa hii, msanii hujitenga na ***hadhira*** kabisa, yaani hawi pamoja na wasomaji. Kazi hii huchukua muda mrefu kuandika. Fasihi andishi ni kazi za uandishi zinazolenga kuchanganua, kuchunguza, kufundisha na kukosoa jamii.

Fasihi andishi ni sanaa inayoandikwa kwenye vitabu, karatasi, magazeti , majarida na kwenye mitandao. Kazi hii huweza kuchapishwa na kuhifadhiwa maktabani au kwenye mtandao kwa ajili ya usomaji wa wakati wowote. Sanaa hii huwa ni mali ya mtu binafsi ambaye ndiye mwandishi wa kazi husika na huwa na haki za kisheria kuhusiana na kazi alizotunga, kuandika na kuchapisha. Fasihi andishi haiwezi kubadilishwa na mtu yeyote isipokwa mtungaji au mwandishi mwenyewe.

Kuna tanzu nne kuu za fasihi andishi ambazo ni: ***hadithi fupi, riwaya, tamthilia*** *na* ***ushairi***.

***Hadithi fupi*** ni utanzu wa fasihi andishi usiokuwa mrefu sana ukilinganishwa na riwaya. Hadithi fupi huandikwa kwa aya zinazosimulia matukio mbalimbali. Hii huwa ni kazi inayogusia maisha ya binadamu. Kazi hii huwa na wahusika wachache mara nyingi wasiozidi watatu. Wahusika katika hadithi fupi huweza kuwa watu, wanyama na vitu visivyokuwa na uhai kama vile: mizimu, vinyago na vinginevyo. Kuna hadithi fupi kadhaa katika mikusanyo ya hadithi fupi ifuatayo: *Nyashya ya Baba, Ndabaga, Yanyoye Nzobya* (za Kinyarwanda), *Baada ya Dhiki Faraja, Tumbo Lisiloshiba* (ya Kiswahili) na nyingine nyingi.

***Riwaya*** ni utanzu wa fasihi andishi ambao huwa mrefu kuliko hadithi fupi. Riwaya huandikwa kwa aya na kwa mfululizo wa matukio mengi mbalimbali. Ni kazi inayojadili maisha ya watu kwa ujumla. Riwaya huwa na wahusika wa kubuni ambao ni wengi. Kazi hii hutumia wahusika wa aina mbalimbali kuliko ilivyo katika hadithi fupi. Mifano ya riwaya ni kama vile: *Isiha rusahuzi* (ya Kinyarwanda), *Roza Mistika, Adili na Nduguze, Siku Njema, Utengano* (za Kiswahili) na nyingine nyingi.

***Tamthilia*** ni utanzu wa fasihi andishi unaowasilisha mchezo wa kuigiza. Tamthilia huandika kwa mtindo wa maneno yanayoandikwa mbele ya mhusika anayeyazungumza maneno hayo. Michezo hii ya kuigiza huandikwa kwa lengo la kuigizwa kwenye jukwaa kwenye tamasha mbalimbali. Mara kadhaa tamthilia hurekodiwa na kuigizwa hata kwenye redio. Mifano ya tamthilia ni kama vile: *Urunana, Musekeweya, Uwera* (za Kinyarwanda) *Kinjeketile, Wakati Ukuta, Kifo Kisimani, Kilio cha Haki, Kijiba cha Moyo* (za Kiswahili) na nyingine nyingi.

***Ushairi*** ni utanzu wa fasihi andishi unaotumia maandiko ya kisanii na kitaaluma. Mashairi huandikwa kwa sentensi zenye idadi fulani ya silabi. Aya za mashairi huitwa ***beti*** (ubeti katika umoja), sentensi katika mashairi huitwa ***mistari*** (mstari katika umoja), au ***mishororo*** (mshororo katika umoja) na silabi zake huitwa ***mizani***. Mashairi yaliyochapishwa huainishwa katika fasihi andishi. Mifano ya mashairi inapatikana katika diwani (vitabu vya mikusanyo ya mashairi) kama vile: *Ibyiruka rya Maheru, Indyoheshabirayi* (za Kinyarwanda), *Titi la mama, Maisha, Pesa, Jicho la Ndani, Kina cha Maisha* (za Kiswahili) na mengine mengi.

Tanzu za fasihi andishi husaidia kuhifadhi historia pamoja na mienendo na desturi za binadamu tangu zamani hadi leo. Kazi hizi huwasaidia viongozi kutunga na kuboresha sera za maendeleo ya jamii zao. Kama vile Waswahili walivyosema: '*asiyejua anapotoka hajui anapokwenda'*, tanzu hizi pia huweza kutabiri hali ya changamoto, maisha bora, hasara, huzuni au mateso yanayoweza kuathiri maisha ya binadamu katika shughuli zake. Mbali na hayo, fasihi andishi huwezesha uhifadhi wa majina na michoro au picha za vifaa vinavyotoa habari zaidi kuhusu mila na desturi za jamii mbalimbali na nchi nzima kwa ujumla.

Kila nchi huwa na vifaa vinavyoashiria mila na desturi zake. Vifaa vya kidesturi nchini Rwanda ni kama vile: *Igisabo, umuvumu, umuvure* n.k. Kama tunavyojua, lugha ni msingi wa mawasiliano kati ya watu duniani kote. Kwa hivyo, fasihi andishi pia huchangia katika ukuzaji wa lugha mbalimbali. Kupitia kwa kazi ya uandishi, watu wameweza kuhifadhi baadhi ya msamiati wa kale wa mamboleo na ule mpya kabisa na kuutumia katika mawasiliano kimaandishi na kimazungumzo.

Fasihi andishi ni kazi inayokusanya matukio ya dunia nzima na kuyaleta karibu na msomaji. Leo hii, ni rahisi kufahamu historia, mila na desturi za nchi nyingi kama vile: nchi za Ulaya, Marekani pamoja na sehemu nyingine nyingi za dunia kupitia kwa mtandao. Waandishi wa habari na wa vitabu hutufahamisha kuhusu mila, desturi, siasa na michezo kila kukicha kupitia kwa maandishi kwenye mtandao. Dunia ya leo imekuwa kama kijiji kimoja kutokana na maendeleo ya fasihi andishi yaliyoenea kote duniani kupitia kwa uandishi na usomaji kwenye mtandao.

Fasihi andishi hutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya utamaduni wa nchi. Utamaduni ni nguzo kubwa ya umoja na mshikamano wa wananchi. Bila shaka, fasihi andishi huwa chanzo cha maendeleo hayo kupitia maandishi ambayo huzingatia elimu kuhusu utamaduni. Utamaduni wa nchi unafananishwa na mali. Kwa mfano, mgeni yeyote akija nchini Rwanda halafu aonyeshwe mchoro wa Mfalme wa Rwanda wa zamani pamoja na nyumba yake, ng'ombe wake, askari wake na kiti chake cha heshima bila shaka atafurahia sana na atakuwa amelipia kuona hayo yote. Kwa kweli utamaduni ni maliasili ya nchi. Hayo yote hutoa mchango katika kuimarisha uchumi wa nchi husika kwani watalii wanapozuru au wanaposoma vitabu kuhusu utamaduni na desturi za nchi, wao huja kuyashuhudia yote hayo kwa kuyalipia.

Fasihi andishi ni sanaa inayosaidia binadamu kujiendeleza na kuelimika, kuhusu historia ya mtu tangu kale mpaka leo na pia kutabiri kisayansi yatakayoathiri binadamu siku zijazo kupitia maandishi ya aina mbalimbali. Fasihi andishi ni chanzo cha utangazaji na usambazaji wa desturi, maadili baina ya watu ulimwenguni.

## Maswali ya ufahamu

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, someni tena kifungu cha habari kuhusu tanzu za fasihi andishi kisha mjibu maswali yafuatayo.*

1. Eleza maana ya fasihi andishi.
2. Kwa nini dunia ya leo imekuwa kama kijiji kimoja?
3. Taja tanzu za fasihi andishi.
4. Eleza sifa mbili za utanzu wa riwaya.
5. Bainisha vipengele vitatu vinavyobainisha shairi.

6. Eleza tofauti mbili kati ya hadithi fupi na riwaya.
7. Jadili tofauti mbili kati ya shairi na tamthilia.
8. Jadili umuhimu wa fasihi andishi kwa jamii na nchi kwa ujumla.
9. Msanii hutunga kazi ya fasihi akilenga nini?
10. Je, mtu yeyote anaweza kubadilisha kazi ya fasihi andishi? Eleza.

## 1.2 Msamiati kuhusu tanzu za fasihi andishi

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tafuteni msamiati mpya katika kifungu cha habari kuhusu tanzu za fasihi andishi mlichosoma hapo awali kisha mweleze maana zake. Zingatieni muktadha wa kifungu husika. Mnaweza kutumia kamusi inapohitajika.*

**Kwa mfano:**

***Desturi*** – mwenendo unaozoeleka kufanywa na jamii; ni mfumo wa sheria au kanuni za jamii.

### Zoezi la 1

A. *Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, elezeni maana ya msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi zifuatazo kisha mtunge sentensi sahihi kwa kutumia msamiati huo katika tungo yakinishi.*

**Kwa mfano:** tamthilia

**Sentensi yakinishi:** *Mwalimu wetu ameandika **tamthilia** nzuri.*

1. Waliigiza ***tamthilia*** nzuri sana.
2. Kamana ataandika ***riwaya*** ndefu.
3. Nilikariri ***shairi*** lenye lugha ya mkato.
4. Mzee wetu alitusimulia ***hadithi fupi*** inayopendeza.
5. Mwalimu wetu hutumia lugha ya ***ishara***.
6. Kaka yake haamini mambo ya ***mizimu*** na majini.
7. Watu wengi hutumia ***mtandao*** kupitia tarakilishi.
8. Kazi yake ya fasihi ina ***wahusika*** wengi.
9. Fasihi andishi ni ***sanaa*** itumiayo maandishi ya kitaaluma.
10. Baraza kuu la ***wasanii*** lilipata kiongozi mkuu.

B. *Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, andikeni sentensi mlizotunga hapo juu katika tungo kanushi.*

**Kwa mfano:**

***Tungo yakinishi:*** *Mwalimu wetu ameandika* ***tamthilia*** *nzuri.*

***Tungo kanushi:*** *Mwalimu wetu hajaandika* ***tamthilia*** *nzuri.*

### Zoezi la 2

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, chagueni jibu sahihi kutoka kwa majibu yaliyo katika mabano kujazia nafasi zilizoachwa wazi katika sentensi hizi.*

1. ______ ni moja kati ya tanzu za fasihi ya lugha ya Kiswahili. (Fasihi, Fasihi andishi)
2. Fasihi andishi huandikwa kwa ____________ la kupitisha ujumbe. (njia, lengo)
3. Katika fasihi andishi, msanii hujitenga na _____________ kabisa. (umati, hadhira)
4. Fasihi andishi huwa ni ___________ ya mtu binafsi. (mali, uwezo)
5. Hadithi fupi huwa na wahusika ____________. (wengi, wachache)
6. _______________ huwa na wahusika wa kubuni ambao ni wengi. (Hadithi fupi, Riwaya)
7. Aya za mashairi huitwa ___________. (mishororo, beti)

## 1.3 Matumizi ya lugha: Umuhimu wa fasihi andishi

*Katika makundi ya wanafunzi watano watano, jadilini mambo matano yanayofafanua umuhimu wa fasihi andishi ya Kiswahili katika jamii.*

**Kwa mfano:**

Fasihi andishi hutoa mchango mkubwa katika usambazaji wa mila na desturi za watu duniani kote. Watu huweza kusoma vitabu vya fasihi andishi vilivyochapishwa kutoka kwenye maeneo yote duniani kupitia kwa mtandao.

## 1.4 Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, jadilini kuhusu kazi ya utanzu wowote wa fasihi andishi ambayo umewahi kusoma na namna ilivyokuwa na umuhimu kwa maisha yako. Kila kundi liwasilishe ufupisho wa majadiliano yao mbele ya wanafunzi wenzao.*

**Kwa mfano:**

*Mimi nilipata fursa ya kusoma Riwaya ya **Siku Njema** iliyoandikwa na Ken Walibora kutoka nchini Kenya. Riwaya hii ilinihimiza kuwa, licha ya matatizo ninayoyapitia katika maisha yangu sasa hivi, nisife moyo kwani ipo siku moja ijayo ambayo itakuwa njema kwangu pamoja na familia yangu. Pia, kutokana na riwaya hii, niliweza kuufahamu umuhimu wa wazazi katika familia na kuutambua utamaduni wa Waswahili.*

## 1.5 Sarufi: Maana ya sentensi

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, pangeni maneno yafuatayo kwa usahihi ili kuunda sentensi kamili na sahihi.*

**Kwa mfano:** chakula mama anapika = Mama anapika chakula.

1. siku huenda kila shuleni wewe
2. ni sita cha mimi kidato wa mwanafunzi
3. fasihi la wetu anafundisha mwalimu somo
4. polepole hilo shairi nini kwa unakariri?
5. wengi fupi wa walio riwaya wahusika hadithi na kubuni huwa kuliko
6. Kiswahili za andishi ya utanzu mojawapo fasihi tamthilia wa ni tanzu

### Maelezo muhimu

***Sentensi*** ni kundi la maneno au neno moja lililo na maana kamili. Maana katika sentensi huonyeshwa na kitenzi. Kundi la maneno lisilohusisha kitenzi si sentensi, na neno moja ambalo si kitenzi kikuu nalo haliwezi kuwa sentensi. Kwa mfano:

1. *Uwera amenunua vitabu.*
2. *Amenipokea.*

### Zoezi la 3

A. *Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, jadilini maana ya sentensi kisha mtunge sentensi kumi katika nyakati tofauti tungo yakinishi.*

B. *Bainisha aina za maneno yaliyotumika katika sentensi mlizotunga katika sehemu ya A.*

CH. *Kanusha sentensi mlizotunga katika sehemu ya A.*

## Zoezi la 4

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadilini sifa za sentensi kamili katika lugha ya Kiswahili.*

## Zoezi la 5

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, chunguzeni sentensi zifuatazo kisha mchague na kubainisha sentensi zisizo kamili. Elezeni sababu za upungufu wa sentensi mtakazozichagua.*

1. Wasanii wa kule Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.
2. Rwanda ni nchi yenye desturi nzuri.
3. Kaneza alisoma vitabu viwili.
4. Sisi kama vijana wa hapa mjini Kigali.
5. Mwenyekiti wa kijiji chao mwenye itikadi kali.
6. Sijaona mtoto kama yule.
7. Tarakilishi hii ni dhaifu sana.
8. Tulipambana tukafuzu.
9. Aliye kando haangukiwi na mti.
10. Kwa nini wewe?

### 1.5.1 Sehemu kuu za sentensi

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, chunguzeni sentensi zifuatazo kisha mjadili kuhusu sehemu kuu za sentensi hizo.*

| **Sentensi** | **Ubainishaji** |
|---|---|
| <u>Mtoto mdogo</u> <u>aliangusha ndoo chini.</u> | *Mtoto mdogo* (Kiima)<br>*aliangusha ndoo chini* (Kiarifu) |
| <u>Mwalimu hodari</u> <u>atafundisha fasihi andishi.</u> | *Mwalimu hodari* (Kiima)<br>*atafundisha fasihi andishi* (Kiarifu) |
| <u>Msichana mrembo</u> <u>atafaulu katika mtihani.</u> | *Msichana mrembo* (Kiima)<br>*atafaulu katika mtihani* (Kiarifu) |
| <u>Tamthilia yake</u> <u>iliigizwa jana.</u> | *Tamthilia yake* (Kiima)<br>*iliigizwa jana* (Kiarifu) |

### Maelezo muhimu

Sehemu kuu za sentensi ni mbili tu: ***Kiima*** **(K)** na ***Kiarifu*** **(A).**

Kiima huhusisha ***nomino, viwakilishi*** na ***vivumishi*** ilhali kiarifu huhusisha ***kitenzi, nomino, vivumishi*** pamoja na ***vielezi***.

**Kwa mfano:** *Mtoto mdogo ameangusha sahani vibaya.*

Sehemu ya kiima itakuwa: *Mtoto mdogo* (Nomino + Kivumishi)

Sehemu ya kiarifu itakuwa: *ameangusha sahani vibaya* (Kitenzi + Nomino + Kielezi)

## Zoezi la 6

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tungeni sentensi kumi sahihi katika nyakati zozote kisha muonyeshe sehemu za kiima na kiarifu katika sentensi hizo.*

**Kwa mfano**: *Mwanamke yule anatembea polepole.*

***Sehemu ya Kiima:*** *Mwanamke yule* (nomino + kivumishi)

***Sehemu ya Kiarifu:*** *anatembea polepole* (kitenzi + kielezi)

## Zoezi la makundi

A. Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, chunguzeni sentensi zifuatazo kisha mjadili kuhusu aina za maneno zinazounda sehemu za kiima na sehemu za kiarifu katika sentensi hizo.

**Kwa mfano:** *Mzee huyu analima shamba vizuri.*

***Maneno katika kiima:*** *Mzee* (nomino) + *huyu* (kivumishi)

***Maneno katika kiarifu:*** *analima* (kitenzi) + *shamba* (nomino) + vizuri (kielezi)

1. Mama analima shamba kubwa.
2. Yeye ni mwanafunzi mwerevu.
3. Sisi tutaimba vizuri.
4. Kamana ataenda sokoni jioni.
5. Mwalimu anafundisha fasihi.

B. *Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, elezeni maneno yanayounda kiarifu katika sentensi mlizopewa hapo juu ni ya aina gani.*

**Mfano wa sentensi 1:** *Mzee huyu analima shamba vizuri.*

***Maneno katika kiarifu:*** *analima* (kitenzi) + *shamba* (nomino au ***shamirisho***) + *vizuri* (kielezi au ***chagizo***)

**Ugunduzi:**

i) Neno '*shamba*' ni nomino inayokuja baada ya kitenzi. Nomino hii inaathiriwa na kitenzi '*lima*'. Kwa hivyo, inaitwa ***shamirisho***.)

ii) Neno '*vizuri*' ni kielezi kinachofafanua kitendo cha '*kulima*'. Kwa hivyo, neno '*vizuri'* ni ***chagizo***).

**Mfano wa sentensi 2:** *Mtoto aliangusha ndoo chini.*

***Maneno katika kiarifu:*** *aliangusha* (kitenzi) + *ndoo* (nomino au ***shamirisho***) + *chini* (kielezi au ***chagizo***)

**Ugunduzi:**

i) Neno '*ndoo*' ni nomino inayokuja baada ya kitenzi. Nomino hii inaathiriwa na kitenzi '*angusha*'. Kwa hivyo, inaitwa ***shamirisho***.)

ii) Neno '*chini*' ni kielezi kinachofafanua kitendo cha 'kuangusha'. Kwa hivyo, neno '*chini'* ni ***chagizo***).

## Uchambuzi kwa kutumia jedwali

| **Sentensi** | **Kiima** | **Kiarifu** |
|---|---|---|
| Mzee huyu analima shamba vizuri. | *Mzee + huyu*<br>(nomino + kivumishi) | *analima + shamba + vizuri*<br>(kitenzi + nomino + kielezi)<br>(kitenzi + shamirisho + chagizo) |
| Mtoto aliangusha ndoo chini. | *Mtoto*<br>(nomino) | *aliangusha + ndoo + chini*<br>(kitenzi + nomino + kielezi)<br>(kitenzi + shamirisho + chagizo) |

### Maelezo muhimu

- Sehemu kuu za sentensi ni mbili: ***Kiima*** na ***Kiarifu***.
- ***Kiima*** ni neno au kundi la maneno yanayoonyesha mtenda na huja kabla ya kitenzi katika sentensi.

**Mfano:** *<u>Kaka yangu</u> anafyeka nyasi vizuri.* (Sehemu iliyopigiwa mstari ni ***Kiima***)

- ***Kiarifu*** ni sehemu ya sentensi inayoanzia kwenye kitenzi pamoja na maneno yanayofuata kitenzi hicho

**Mfano:** *Kaka yangu <u>anafyeka nyasi vizuri.</u>* (Sehemu iliyopigiwa mstari ni ***Kiarifu***)

- Maneno yanayofuata kitenzi huwa ni ***shamirisho*** na ***chagizo***.

**Mfano:** *Kaka yangu anafyeka nyasi vizuri*. (Neno *'nyasi'* ni nomino inayokuja baada ya kitenzi '*fyeka*'. Nomino hii inaitwa ***shamirisho***.)

**Mfano:** *Kaka yangu anafyeka nyasi vizuri*. (Neno *'vizuri'* ni kielezi kinachofafanua kitendo cha kufyeka. Kielezi hiki kinaitwa ***chagizo***)

## Zoezi la 7

Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, someni na mchunguze sentensi zifuatazo kisha mwonyeshe aina za maneno yanayounda kila sehemu ya kila sentensi kupitia jedwali.

Kwa mfano:


| **Sentensi** | **Kiima** | **Kiarifu** |
|---|---|---|
| Mugeni alikariri mashairi. | *Mugeni*<br>(nomino -<br>jina la mtu) | *alikariri* + *mashairi*<br>(kitenzi +nomino)<br>(kitenzi +shamirisho) |

1. Kamana alitunga hadithi fupi sana.
2. Mutoni ataigiza tamthilia jukwaani.
3. Abayo na Mukunzi waliandika riwaya mwaka jana.
4. Gazeti lilipitisha riwaya yake jana.
5. Utaondoka lini?

# Somo la 2: Utanzu wa hadithi fupi

## 2.1 Hadithi fupi kuhusu uhifadhi wa mazingira

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tazameni michoro hii kisha msome kifungu cha hadithi fupi kinachofuata kuhusu uhifadhi wa mazingira na umuhimu wake nchini Rwanda na baadaye mjibu maswali ya ufahamu yanayofuata.*





Hapo zamani, Bwana Bakame aliishi katika msitu mkubwa wa Nyarume. Huu ulikuwa msitu mzuri sana wenye miti mingi, maziwa, mito, milima, wanyamapori kama vile: kiboko, simba, fisi, ngiri, nyati, nyani, sokwe, twiga na wengineo. Pia, kulikuweko na ndege wa aina mbalimbali kama vile: kware, korongo, tai, mwewe, heroe (*flamingo*) na wengine wengi. Pembezoni mwa msitu huu kulikuwa na vijiji mbalimbali pamoja na wakazi wake. Baadhi ya wakazi hawa walifanya kazi zao katika msitu wa Nyarume. Bwana Bakame alikuwa amekula chumvi nyingi katika kufanya kazi kwenye msitu huo kiasi kwamba alikuwa anafahamu milima, maziwa, wanyamapori wote na hata ndege wote wa msitu huo. Bwana Bakame pia alikuwa anawafahamu wakazi wote walioishi pembezoni mwa msitu huo.

Walinzi na wageni wote wa msitu wa Nyarume walikuwa wanamfahamu Bwana Bakame. Walimpenda sana. Bwana Bakame alikuwa mpole, mcheshi na mwenye hekima ya kushangaza. Alikuwa na uwezo wa kuwaelekeza wageni wote waliofika pale msituni na kuwatembeza kwenye sehemu za kupendeza kule msituni.

Licha ya kuwa maarufu sana katika msitu wa Nyarume, Bwana Bakame alipewa madaraka ya kuwa kiongozi wa msitu huo wote. Siku ya uchaguzi, walinzi wa msitu waliandaa mkutano wa wanyama na ndege wote. Wawaniaji wa kiti hicho cha uongozi walikuwa Bwana Bakame na Bwana Simba. Asilimia themanini na

tano ya wapiga kura wote walimchagua Bwana Bakame. Baada ya kutawazwa kuwa mshindi, wanyama na ndege wote walikubali na kufurahia ushindi wa Bwana Bakame. Bwana Simba naye alikubali kushindwa na akatangaza kwamba atauunga mkono uongozi wa Bwana Bakame.

Baada ya miaka miwili, msitu wa Nyarume ulikabiliwa na ushambuliaji wa wawindaji, wavuvi, wauza kuni, wauza mbao na wachoma makaa. Katika kipindi hicho, wanyama wengi kama vile: kobe, nyoka, twiga, nikwata, nungu, panya na wengine walifariki katika vumanizi hilo. Wanyama wengine wenye nguvu walihamia kwenye sehemu za milimani. Mara baada ya tukio hilo, mlinzi mkuu wa msitu wa Nyarume alishirikiana na Bwana Bakame na kuandaa mkutano mkubwa wa wanyama wote pamoja na watu wote walio majirani wa msitu Nyarume na hapo waliwaeleza madhara ya kuharibu mazingira na umuhimu wa kuyahifadhi.

Mlinzi mkuu alisema, "Kwanza, samahani sana wanyama wote kwa shambulizi la watu katika msitu huu wetu. Kwa kweli, ndugu, marafiki, watoto na majirani wenu wengi walipoteza maisha yao pamoja na nyumba zenu na mapango yenu kubomolewa. Niko hapa kuwaarifu yafuatayo: ni jambo baya sana kuharibu mazingira yetu. Tukikata miti mara kwa mara tutakaribisha jangwa katika kijiji kwetu. Tukichoma msitu wetu, wanyama watapoteza maisha yao. Bila shaka, sisi wote tunafahamu kwamba wanyama ni viumbe kama sisi, wanastahiki maisha bora, haki na uhuru." Bwana Bakame alifurahia maneno aliyoyasema mlinzi mkuu wa msitu wa Nyarume. Alisimama na kuwaambia wanyama, "Pigeni makofi." Makofi, vigelegele na burudani vilifuata kwa dakika kama tano hivi. Baadaye mlinzi mkuu aliendelea kusema, "Tunajua kwamba wanyama wa msitu huu ni muhimu sana kwetu kwa sababu watalii kutoka kote duniani huja kuzuru nchi yetu kwa ajili ya kuwaona. Watalii wanapotembelea msitu huu na kuwaona wanyama wetu, wao hulipa pesa zinazosaidia katika maendeleo ya kijiji chetu."

Aliendelea akasema, "Ningependa ieleweke kwamba, hapa shambani tuna mito na maziwa mazuri, hivi vyote ni muhimu, naomba tuvilinde. Tukiharibu maziwa na mito yetu, tutakosa maji ya kunywa, kuoga, kupika na kufua nguo, bila ya kusahau kwamba majini kuna samaki, mamba, viboko na wanyama wengine wanaoishi majini. Tunafaa tuyahifadhi maji yetu ili wanyama hao wasiangamie. Ni muhimu kujua kwamba kuwepo kwa miti na maji ndio sababu ya kupatikana kwa mawingu ya mvua na hatimaye mvua inayonyesha na kutufaidi sisi sote; watu na wanyama. Ni hatia kubwa sana kuwinda katika msitu wa Nyarume, kukata miti katika msitu huu pamoja na kuharibu maji yake."

Bwana Bakame alipewa muda wa kuzungumza naye akasema, "Kwanza, shukrani zote zimwendee mlinzi mkuu wetu kwa hoja zake nzuri alizotoa. Kwa kweli, tulifanyiwa shambulizi kubwa ambapo wanyamapori wengi walipoteza maisha yao.

Naomba kwa sasa tuyasahau hayo, sisi tunataka uimarishaji na ushirikiano mwema na watu wote katika shughuli za kuhifadhi msitu huu. Sisi hatujawahi kuwashambulia watu hata kamwe. Kama mjuavyo, miongoni mwetu kuna wanyamapori wakali sana kama vile: simba ambao wanaweza kuwashambulia watu na kuwaangamiza mara moja ila tunaomba tuimarishe nidhamu miongoni mwetu. Naomba tushirikiane zaidi hata baada ya kikao hiki, asante sana."

Baada ya mkutano huo, watu wote pamoja na wanyamapori wote walishirikiana katika kuulinda msitu wa Nyarume. Watu na wanyama walianza kupata hewa nzuri na safi, mvua nyingi, miti ikanawiri, majani yakawa mengi na mazuri, ndege wakaongezeka, maziwa yakajaa maji ya kutosha. Wote waliishi maisha mazuri daima.

## Maswali ya ufahamu

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, someni tena kifungu cha hadithi fupi kuhusu uhifadhi wa mazingira pamoja na umuhimu wake nchini Rwanda kisha mjibu maswali yafuatayo.*

1. Orodhesha aina za ndege waliotajwa katika kifungu mlichosoma.
2. Eleza sababu za watu kushambulia msitu wa Nyarume.
3. Jadili umuhimu wa msitu kwa wanyamapori.
4. Wanyamapori wana umuhimu gani katika mazingira yetu?
5. Mbuga za wanyama hutoa mchango gani katika maendeleo ya nchi?
6. Jadili madhara yanayotokana na kuharibu mbuga za wanyama.
7. Eleza madhara ya kuwawinda wanyamapori.
8. Eleza madhara ya kuharibu maji asili ya nchi.
9. Jadili faida za miti na maji nchini Rwanda.
10. Eleza sifa za:
    a) Bwana Bakame
    b) Mlinzi mkuu wa msitu wa Nyarume

## 2.2 Msamiati wa hadithi fupi kuhusu uhifadhi wa mazingira

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tafuteni msamiati mpya kutoka katika kifungu cha hadithi fupi mliyoisoma hapo awali kisha mweleze maana yake na kuutungia msamiati huo sentensi sahihi kisarufi. Zingatieni muktadha wa kifungu husika. Mnaweza kutumia kamusi inapohitajika.*

**Kwa mfano:**

***Daima -*** bila ya kuwa na mwisho; milele
***Matumizi katika sentensi:*** *Upendo wa mama hudumu **daima**.*

## Zoezi la 1

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, husisheni maneno yaliyoandikwa katika sehemu A na maelezo yake sahihi kutoka katika sehemu B.*

| **Sehemu A** | **Sehemu B** |
|---|---|
| 1. Nungu | A. Idadi au kiasi fulani kwa kila mia moja |
| 2. Nyati | B. Sauti zitokazo kinywani kwa kugonganisha ulimi na kaakaa gumu ya kinywa kwa kufurahia jambo |
| 3. Msitu | CH. Ndege mfupi anayefugwa ambaye ana madoadoa |
| 4. Zuru | D. Tembelea mahali fulani ili kuonana na mtu fulani |
| 5. Mwewe | E. Mamlaka anayopewa mtu |
| 6. Vigelegele | F. Mnyamapori mkubwa afananaye na ng'ombe |
| 7. Tausi | G. Chaka la miti, majani na nyasi |
| 8. Madaraka | H. Ndege wa jamii ya tai ambaye huwakamata kuku |
| 9. Asilimia | I. Kuwa na haki ya kumiliki au kupata kitu |
| 10. Stahiki | J. Mnyama mwenye mwili uliofunikwa kwa miba |

## 2.3 Matumizi ya lugha

### Majadiliano kuhusu uhifadhi wa mazingira

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, jadilini:*

1. Faida mbalimbali za kuhifadhi mazingira yetu.
2. Madhara ya kuharibu mazingira yetu.
3. Njia za kuhifadhi mazingira yetu.
4. Shughuli zinazoharibu mazingira yetu.
5. Umuhimu wa mazingira kwa wanyamapori.

**Kwa mfano:**

*Mojawapo ya faida za kuyahifadhi mazingira yetu ni kuwa mito ni hazina ya maji. Maji haya huwasaidia watu katika shughuli mbalimbali kama vile: kilimo, ufugaji, uvuvi na kadhalika.*

## Zoezi la 2

A. Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, fupisheni kifungu cha hadithi fupi mlichosoma hapo awali kwa kutumia maneno sabini (70) pekee. Msinakili maneno moja kwa moja kutoka kwenye kifungu hicho.

B. Baada ya kuandika ufupisho, kila kundi limchague mwanafunzi mmoja atakayewasilisha kazi hiyo mbele ya wanafunzi wengine huku akieleza na kuonyesha namna walivyozingatia maagizo ya kuandika ufupisho.

## Maelezo muhimu

Kabla ya kufupisha kifungu chochote ni vyema:

a) Kuelewa ujumbe wa kifungu hicho.
- Soma kifungu mara mbili na kwa makini.
- Jibu maswali kama vile: - Kifungu kinahusisha wahusika gani?
    - Mandhari ya kifungu ni yapi?
    - Wahusika muhimu ni akina nani?
    - Kifungu kinaeleza mawazo gani?
- Jibu maswali hayo kwa kuyaandika kwenye karatasi.

b) Kufuata taratibu za kuandika ufupisho wenyewe.
- Andika kichwa cha ufupisho.
- Tutumia maneno yako mwenyewe.
- Tumia Kiswahili sanifu. (*Usichanganye lugha mbalimbali*)
- Kazi iwe safi na mwandiko wako uweze kusomeka.
- Hakikisha kwamba unaepuka makosa ya kisarufi katika ufupisho wako.
- (*Zingatia matumizi sahihi ya alama za uandishi, matumizi sahihi ya ngeli n.k.)*
- Usipunguze, usiongeze wala usiende kinyume na mawazo asilia ya mtunzi wa kifungu.
- Usiandike zaidi ya maneno uliyoagizwa.

## 2.4 Kusikiliza na kuzungumza: Sifa bainifu za hadithi fupi

### Zoezi la 3

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadilini kuhusu sifa bainifu za hadithi fupi kama mojawapo wa utanzu wa fasihi andishi.*

### Zoezi la 4

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadilini kuhusu mambo muhimu yaliyopatikana katika hadithi fupi mliyosoma hapo awali kuhusu uhifadhi wa mazingira na kuyalinganisha na maisha yenu ya kila siku.*

### Zoezi la 5

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadilini umuhimu wa hadithi fupi katika jamii. Kila kundi liwasilishe ufupisho wa majadiliano yao mbele ya wenzao.*

## 2.5 Sarufi: Maana ya kirai

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, chunguzeni sehemu zilizopigiwa mistari katika sentensi zinazofuata kisha mwelezane ugunduzi wenu.*

**Kwa mfano:** *<u>Mwanafunzi mmoja</u> amebaki darasani.*

**Jibu:** Maneno yaliyopigiwa mstari, '*mwanafunzi mmoja*', *ni* nomino pamoja na kivumishi kimoja. Fungu hili la maneno linaitwa ***kirai***. Hiki ni ***kirai nomino*** kwa sababu neno kuu linalotangulia katika fungu hilo ni nomino.

1. <u>Mtoto mmoja</u> alizaliwa jana.
2. <u>Sahani hizi</u> zitauzwa sokoni.
3. <u>Kobe huyu</u> hutembea polepole sana.
4. <u>Msichana yule mrembo</u> ameshinda <u>tuzo zuri.</u>
5. <u>Nyanya mzee</u> alisuka <u>kikapu kizuri</u>.

*Je, ugunduzi wenu ni upi?*

***Kirai*** ni kipashio cha kisarufi kinachoundwa kwa neno moja au zaidi na huwa hakina mwingiliano wa kimuundo wa kiima na kiarifu. Aina za virai ni kama vile: *kirai nomino, kirai kivumishi, kirai kielezi, kirai kiunganishi n.k.*

**Mifano ya virai:**

1. ***Watoto wawili*** wameanguka chini. (Kirai nomino)
2. ***Mtoto na mama yake*** wanaenda kanisani. (Kirai nomino)
3. Mtu ***mwenye maringo mengi*** amenunua gari. (Kirai kivumishi)
4. Wachezaji ***warefu sana*** wameingia uwanjani. (Kirai kivumishi)
5. Rais aliwasili ***jana jioni***. (Kirai kielezi)
6. Sisi tutaondoka ***asubuhi na mapema***. (Kirai kielezi)

## Zoezi la 6

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, jadilini tofauti kati ya sentensi kamili na kirai.*

**Kwa mfano:**

1. Mwalimu mpole anaandika ubaoni.
2. Mwalimu mrefu mpole.
3. Mtoto mmoja amefika shuleni.
4. Mtoto mmoja mrefu.

**Jibu:** i) Nambari ya 1 na ya 3 ni sentensi kamili kwa sababu zina kiima na kiarifu.

ii) Nambari ya 2 na 4 ni virai wala si sentensi kamili kwa sababu hazina vitenzi. Hivi ni ***virai nomino***.

## Maelezo muhimu

• Fungu la maneno ambalo neno lake kuu ni nomino huitwa ***kirai nomino***.
**Kwa mfano:** ***Redio na runinga*** *hutumiwa katika mawasiliano.*

• Fungu la maneno ambalo neno lake kuu ni kivumishi huitwa ***kirai kivumishi***.

**Kwa mfano:** *Wanyama* ***wakali mno*** *waliwavamia wanakijiji.*

• Fungu la maneno ambalo neno lake kuu ni kielezi huitwa ***kirai kielezi***.
**Kwa mfano:** *Mtoto anatembea* ***polepole sana***.

• Kundi la maneno au neno moja lililo na maana kamili huitwa ***sentensi***.
**Kwa mfano:** *Mtihani huu umesahihishwa na mwalimu.*

## Zoezi la 7

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, chunguzeni mafungu ya maneno yafuatayo kisha muainishe iwapo ni sentensi au kirai.*

1. Mwalimu alihakiki hadithi fupi. (Sentensi au Kirai?)
2. Watoto wawili warefu na kijana mfupi. (Sentensi au Kirai?)
3. Bakame na Simba waliitisha mkutano. (Sentensi au Kirai?)
4. Ushirikiano mwema na watu katika shughuli za porini. (Sentensi au Kirai?)
5. Mara baada ya tukio hilo porini. (Sentensi au Kirai?)

## Maelezo muhimu

Tofauti kati ya sentensi na kirai ni:

- Sentensi huundwa kwa vipashio viwili ambavyo ni kiima na kiarifu.
- Kirai huundwa kwa neno moja au zaidi bila ya kuwa na kiima na kiarifu.
- Sentensi haiwezi kuwa kamili bila ya kitenzi.
- Kirai huweza kuwa kamili bila ya kitenzi.

Kwa mfano:

1. *'Gasimba anacheza uwanjani'* ni sentensi kamili. Ina kiima na kiarifu.
2. *'Mvulana mmoja mrefu'* ni kirai nomino. Ina nomino na vivumishi viwili.

## Zoezi la makundi

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tambueni virai nomino katika sentensi hizi.*

**Kwa mfano:** Maziwa na mito hutupa maji mazuri.

**Jibu:** '*Maziwa na mito'* ni kirai nomino

*'maji mazuri'* ni kirai nomino

1. Mchungaji wa nyumba aliongoza mkutano.
2. Walimu wetu hutupatia mitihani mara kwa mara.
3. Babaye mlinzi wa pori alipewa zawadi nzuri.
4. Rais wa Rwanda alisafiri jana usiku.
5. Msichana mrefu mwembamba ameajiriwa kazi.

# Somo la 3: Utanzu wa riwaya

## 3.1 Sura moja ya riwaya kuhusu uchaguzi wa viongozi

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tazameni picha hii kisha msome sura moja ya riwaya ya '**Utengano**' (iliyoandikwa na Said A. Mohamed) inayofuata na baadaye mjibu maswali ya ufahamu.*



### Uwanja wa uhuru ...

Ilikuwa siku ya watetezi kujielezea. Uwanja umejaa, wake kwa waume, wadogo kwa wakubwa. Asiye mwana labda alieleka jiwe. Watu wamefika hapa mapema. Wa ng'ambo na wa mjini. Wote walikuwa na hamu ya kuwasikia watetezi wao wakijitambulisha na kujieleza. Kulipambazuka. Miale mikali ya jua ilianguka juu ya migongo yao. Umma mkubwa. Kuna waliokaa kitako na waliosimama. Na hivi, kwa mbali, ukitazama wingi wa vichwa vyao utadhani sisimizi weusi wamebeba chicha. Wanaume, kofia kwenye tosi zao, na wanawake vitambaa vya mabuibui na leso. Wachache waliviamini vichwa vyao kwa jua.

Wengi wamekaa chini kwenye majani ambayo sasa yameshakauka umande. Wengine wamekaa juu ya mabodi ya gari, ndogo na kubwa. Wengine wamesimama na baiskeli zao. Wengine kwenye miti. Joto na jasho. Mchanganyiko wa sauti, nene na nyembamba, minong'ono na mingurumo ilihanikiza. Vicheko, vikohozi, miayo. . . kila mtu alikuwa akingojea kwa hamu. Ilikuwa siku muhimu kwa kila mtu; hasa kwa Bwana Maksuudi. Saa tatu ikaingia. Watu hawakungojea sana kama kawaida ya mikutano kama hii ambayo pengine hata ilichukua masaa sita ya kungojea kwa machofu bila mtu kuthubutu kuondoka.

Lakini leo viongozi walifika mapema kwa sababu leo ni siku ya kubembeleza kura. Wengi waliofika hapa walikuwa na mawazo ya mchanganyiko. Mzee Japu alikuwa kakaa kwa hamasa. Moyoni mwake mlikuwa na hasira, na aliwaza, 'Maksuudi. . . aaa, alipokuwa Mkuu wa Wilaya, alikula pesa ngapi za mke wangu alipotaka kununua kiwanja cha kujengea nyumba. Sahihi yake tu Mkuu wa Wilaya aliiuza shilingi mia mbili. Leo anataka mimi na mke wangu tumpe kura. Ainuke zaidi maana yake, azidi kutukalia vichwani. Tumechoka kuchezewa na watu kama hawa. Kura yangu nitampa Siwa, kijana huyu amepata sifa miongoni mwa wananchi. Sifa zake zimeenea. Kijana mkakamavu, siye yule dhalimu Maksuudi, au Zanga. . .' Kuna waliodiriki kubwata maneno waziwazi bila ya kificho.

Kiboda asiyejua kuficha dukuduku lake alimpasukia mwenzake, 'Maksuudi, Maksuudi, Maksuudi gani nazo bibi we. Tumechoka bibi, na leo hakuna uwongo utakaofaa, maana uwongo ndiyo kazi yao. Hilo ndilo wanalolijua. Lakini akili kichwani mwangu shoga.''Aaa, mimi mtetezi wangu nimeshamjua babu,' Biti Shomari alijibu kwa kelele hata wale waliokuwa wamekaa karibu naye waligeuka, wakakenua. Wakati uliwadia. Watetezi wote walifika na mkutano ulianza. Alisimama Katibu wa tawi la chama kuwajulisha watu madhumuni ya mkutano huo, na baadaye shughuli ilianza. Mtetezi wa mwanzo kujitetea ni kijana Siwa.

Aliinuka katikati ya shangwe na hoihoi, makofi, mikono juu, vigelegele na vishuo. Watu wote takriban walisimama. Siwa alipungia watu mikono na wote waliokuwa wamekaa mwanzo, walikaa tena. Siwa hakuwa na mengi. "Wananchi, mimi sina mengi. Hapana katika nyinyi asiyenielewa juu chini. Sina kubwa la kusema ila nakukumbusheni kuwa mnahitaji kiongozi atakayeshughulikia maslahi yenu na maslahi ya taifa zima. Nyinyi ndio mtakaoamua kati yetu ni yupi anayestahili kura zenu kwa sababu sote mnatuelewa." Shangwe za watu, 'Siwa, Siwa, Siwa, Siwa ...' "Je, liko suala lolote?" Aliuliza Siwa baada ya shangwe. "Hakunaaaaa," sauti ya umma ilikuja juu.

Zamu ya mtetezi wa pili. Huyu alikuwa Bwana Zanga. Mtu mzima. Sasa alikuwa akiinuka kwa kicheko. Watu fulani haba waliokuwa wamekaa usoni walipiga makofi. Hakukuwa na zaidi. Zanga ni mmojawapo wa viongozi halisi ambaye kwake cheo ni ujeuri, majivuno na kujiona. Makofi yale machache yaliyopigwa yalimvunja moyo na toka hapo ana kigugumizi, Zanga hakusema neno la maana. "Mu. . . mu. . . mukinipa mimi kura zenu, nitajenga njia, nitawapa watu kazi, nitajenga skuli zaidi, na maisha yenu yatakuwa katika raha." Hakukuwa na makofi. Kimya kiliingia kikamtenga Zanga na wasikilizaji wake. Hatimaye, "Liko la kuuliza?" Alikuja juu kwa hamaki na uchungu. Kimya kingine.

Mzee Bakari alijibu moyoni, 'Njia, kazi, skuli zaidi, raha. . . haya ndiyo mliokuwa mkituambia muda wote huu; watetezi gani nyinyi? Hata hamjui kuwa nchi yenu

maskini haina uwezo wa kutimiza ahadi mnazotoa...' Mama Miraji, alinong'ona, 'Paulizwe nini na kila mtu anayajua yote?' Zamu ya Maksuudi ilifika. Alisimama kwa heba kubwa, kicheko mdomoni na bashasha zinamfufurika. Alijipa moyo kuona vile alivyozowea midani hii. Jukwaa analijua uzuri, kusema anasema kwa furaha, heba yake, utu uzima wake, uhalisi wake katika chama, yeye muasisi. Isitoshe msingi wa ukoo wake, mfanyakazi na mkulima halisi, alikuwa na sababu za kushinda.

Alikikabili kikuza sauti. Akaanza. "Mabibi na mabwana. . . Maksuudi si mgeni kwenu…" Aliendelea na hotuba yake refu kama alivyoipanga, na mwisho alimaliza, "Mnahitaji mtetezi kama mimi." Hakukuwa na mashangilio, makofi wala vigelegele toka mwanzo mpaka mwisho wa hotuba yake, isipokuwa kwa kikundi kidogo kilichokuja juu muda hata muda. Maksuudi alipata kihoro, moyo ulimtibuka. Alijua kuwa wananchi hawamtaki na kura zake siku ya uchaguzi zingalikuwa haba. "Ni wajibu wenu wananchi kuuliza," alisema kwa masikitiko yaliyochanganyika na hasira, "au kusema lolote, lakini nakukumbusheni ukubwa busara. . ."

Alisimama hivyo hapo mbele ya kikuza sauti akiangalia wapi ungalizuka mkono, lakini hakukuwa na mkono. Alihimiza tena, "Hakuna. . ." "Mimi," alikatwa kauli na sauti ya mwanamke. Alipoangalia aliona mkono juu umeinuliwa na kidogo kidogo bibi mmoja mwingi wa mwili, jamili wa sura na mrembo wa kuvutia, aliinuka. Maksuudi hakuchukua muda kumtambua yule ni nani. "Wananchi wenzangu," alianza Kazija kwa sauti ya juu ya hamasa, "haifai kuiacha fursa hii. Hawa mahaini walitupa nafasi tuwasubu na sisi tulinyamaza kimya. Nani asiyemjua Zanga hapa? Nani asiyejua hali aliyokuwa zamani? Leo mtazameni yeye nani. Vazi amebadilisha. Mwendo amebadilisha. Ana magari matatu. Ana nyumba tatu, moja yake, moja ya mkewe, na moja ya wanawe.

Kazini hapatikani ila na watu wakubwa kama yeye na kwake sasa hawaendi watu ovyo. Lugha yake ni ujeuri. Mkabala wake na watu ni wa majivuno na zaidi hana imani wala fikra kwa wale ambao wamemnyanyua. Haya ni machache tu." "Kweli, kweli, kweli," umma ulitatarika. "Na Maksuudi. . . huyu aliyewahi kuwa Mkuu wa Wilaya, akataka kuifisidi nchi hii kwa kuwadhulumu wananchi, na ambaye baada ya kugundulikana na kusamehewa amekuwa ahasi. . ." "Ndiyo, pasuaaaaa mama," zogo jingine. "Huyu Maksuudi ambaye ameshindwa kuiendesha nyumba yake ataweza kuangalia maslahi yetu? Leo, mwanawe mwanamume hawajaonana mwaka.

Mtoto wake mwanamke hamjui alipo, amemtoroka, amestahabu kupigwa na ulimwengu. Maksuudi aliyemwacha mkewe kwa kisa cha kumtorosha mwanawe ati. Na huyu huyu Maksuudi aliyekuwa akimwendea kinyume mkewe. Mbali na mali aliyojilimbikia, nyingine ya unyang'anyi kwa wake zake. Amemnyang'anya mkewe mmoja, Mwanasururu, mali yake na mwisho akamwacha na kusababisha kifo

chake. Mengi, mengi . . .” “Kweli, ndiyo, waambie, waelezeeeee!” Uma sasa ulikuwa umeshanyanyuka unasogea mbele kidogo kidogo kule walikokuweko watetezi.

Kwa Maksuudi, kiwingu cha haya, aibu na fedheha kilikuwa kimemwangukia. Na juu ya hayo aliingiwa na woga na hofu. “Kazija . . . Kazija . . .” lakini sauti haikutoka. Aliogopa jambo moja zaidi asije akalisema mwanamke huyu. Zogo lilikuwa limeshakaribia pale penye kiriri; aliyefinyanga ngumi, aliyeshika bakora, aliyeinua jiwe __ wote wamesawijika kwa ghadhabu wanataka kulipiza kisasi. Umma ulikuwa tayari kulipa kani zao. Katikati ya zogo hili alionekana Inspekta Fadhili na askari wakipenyapenya na kwa ujasiri mkubwa, hatimaye walifika mbele. Askari wake waliwazingia watetezi wawili, Maksuudi na Zanga, huku Inspekta Fadhili akiwanyamazisha watu.

Na kwa Inspekta Fadhili haikumchukua muda kwa sababu ya umaarufu wake miongoni mwa wananchi. Kwa kweli ni kwa ajili yake tu, ndio wakasita. “Wananchi,” aliambia watu Inspekta, “ zaidi na mliyoyasikia hapa ya mabwana hawa wawili, watetezi wetu, Maksuudi na Zanga wana kesi za jinai na kwa hivyo iwachieni sheria itekeleze wajibu wake.” Muda si muda Maksuudi na Zanga walikuwa wakiongozwa na polisi huku wametiwa pingu. Huku nyuma, wananchi walimbeba Siwa, wakaenda naye kwa shangwe: “Siwa, Siwa Siwa...” Njiani mazungumzo yalikuwa ya mwanamke Kazija aliyekuwa na ujasiri kuliko wanaume. Yeye ndiye aliyethubutu leo kumpa kweli kiongozi.

## Maswali ya ufahamu

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, someni tena sura moja ya riwaya mliyosoma kisha mjibu maswali yafuatayo.*

1. Taja wahusika wadogo wanaopatikana katika sehemu ya riwaya mliyosoma.
2. Inspecta Fadhili alikuwa na majukumu gani katika mkutano husika?
3. Mbona Bwana Maksuudi na Zanga walitiwa pingu na kupelekwa na askari polisi?
4. Taja jina la mkewe Bwana Maksuudi lililomo katika riwaya uliyosoma.
5. Siku hiyo ya mkutano wa watetezi watu walikusanyika kufanya nini?
6. Zanga alikuwa na kasoro gani?
7. Mbona Zanga hakupigiwa makofi alipotoa hotuba jukwaani?
8. Eleza sababu za Mzee Japu kumwita Bwana Maksuudi ‘dhalimu’.
9. Kijana Siwa alipokewa vipi na washiriki katika mkutano huo?
10. Eleza sifa za Bwana Maksuudi.

## 3.2 Msamiati kutokana na sura moja ya riwaya husika

### Zoezi la 1

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tafuteni msamiati mpya kutoka katika sehemu ya riwaya mliyosoma hapo awali kisha mweleze maana zao na kutunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno hayo. Zingatieni muktadha wa kifungu husika na mnaweza kutumia kamusi inapohitajika.*

**Kwa mfano:**

***Ghadhabu*** - *hali ya kukasirika; hasira, hamaki.*

***Matumizi katika sentensi:*** Ameshikwa na ***ghadhabu*** kubwa aliposalitiwa na mkewe.

### Zoezi la 2

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, chagueni maana sahihi ya msamiati uliopigiwa mistari kutoka kwenye mabano.*

**Kwa mfano:** Katikati ya **zogo** hili alionekana Inspekta Fadhili. (ghasia/furaha)

**Jibu:** ghasia

1. Mbali na mali ***aliyojilimbikia***, nyingine ya unyang'anyi kwa wake zake. (aliyoiba/aliyokusanya)
2. ***Watetezi*** wetu, Maksuudi na Zanga wana kesi za jinai. (wanaopigania wengine/wanaelimisha watu)
3. Alisimama kwa ***heba*** kubwa. (tamko/ishara)
4. Lugha yake ni yenye ***ujeuri***. (hasira/kiburi)
5. Aliyeshika ***bakora*** na aliyeinua jiwe. (kitu/fimbo)
6. ***Siwa*** alipunga mikono na watu wote waliokuwa wamekaa mwanzo, walikaa tena. (Jina la kiumbe/Jina la kiongozi maalum)
7. Wanaume, kofia kwenye tosi zao, na wanawake vitambaa vya ***mabuibui*** na leso. (nguo za wanawake/nguo za vijana)
8. ***Mkabala*** wake na watu ni wa majivuno na zaidi hana imani wala fikra. (Ukamilifu/Uhusiano)
9. Kimya kiliingia ***kikamtenga*** Zanga na wasikilizaji wake. (kikamweka kando/kikamhusisha)

## 3.3 Matumizi ya lugha: Sifa bainifu za riwaya

Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, jadilini:

a) *Sifa bainifu za riwaya.*

b) *Tofauti kati ya riwaya na hadithi fupi.*

### Maelezo muhimu

- Riwaya ni utanzu wa fasihi andishi.
- Riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni ambayo huchukua muda mrefu kuandikwa na huwa na wahusika wengi na wa aina nyingi. (wakuu na wadogo)
- Mhusika mkuu ndiye huwakilisha mawazo muhimu ya mwandishi.
- Katika riwaya, matukio mara nyingi huwa ni tata.
- Mtunzi wa riwaya hajui maoni ya wasomaji, yaani anajitenga na hadhira.
- Riwaya huwa na maneno mengi sana, zaidi ya kurasa sitini.

### Zoezi la 3

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, someni tena sura moja ya riwaya mliyosoma hapo awali kisha mtathmini aina za wahusika na matukio katika kifungu hicho.*

## 3.4 Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano kuhusu maudhui

### Zoezi la 4

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadilini mawazo muhimu yaliyopatikana katika sura moja ya riwaya mliyosoma hapo awali kisha myalinganishe mawazo hayo muhimu na maisha yenu ya kila siku.*

### Zoezi la 5

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadilini tabia za wahusika kutoka kwenye sura moja ya riwaya mliyosoma hapo awali kwa kulinganisha tabia zao na maisha yenu ya kila siku. Kila kundi liwasilishe ufupisho wa majadiliano yao darasani mbele ya wanafunzi wenzao.*

## 3.5 Sarufi: Kirai kivumishi

A. *Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, chunguzeni sehemu zilizopigiwa mistari katika sentensi zinazofuata kisha mwelezane sehemu hizo ni za aina gani na zimeundwa kwa maneno yapi.*

**Kwa mfano:** Msichana yule mrembo ameimba vizuri.

**Jibu:** Maneno yaliyopigiwa mstari ni vivumishi viwili, hivyo vinaunda ***kirai kivumishi*** cha vivumishi viwili.

1. Babu alitusimulia hadithi nzuri kabisa.
2. Msichana mwenye sauti laini ametuzwa.
3. Alijenga nyumba yenye kuta ndefu.
4. Dada yangu ana nywele ndefu sana.
5. Wananchi wenye kutukana viongozi watachukuliwa hatua kali.
6. Mwanafunzi mwenye kuhifadhi sheria za shuleni atatuzwa.
7. Baba alitafuta hoteli nyingine yenye huduma nzuri.
8. Kuku huyu ni mzuri wa kuuzwa.
9. Mtu mpungufu wa akili hastahili kuja hapa.

*Jadili ugunduzi wenu.*

B. *Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, onyesha kwa kutumia mifano tofauti kati ya kirai kivumishi na kirai nomino.*

**Kwa mfano:**

***Kirai kivumishi:*** Mtoto mfupi mnene amefika. (*kivumishi* + *kivumishi kingine*)

***Kirai nomino:*** Mtoto mfupi mnene amefika. (nomino + kivumishi + kivumishi)

### Maelezo muhimu

Fungu la maneno yenye muundo ambao umekitwa katika kivumishi huitwa ***kirai kivumishi***.

**Muundo wa kirai kivumishi:**

1. ***Kivumishi pamoja na kielezi chake:***

**Mifano**: a) Habari niliyopewa ni njema kwelikweli.

Kirai kivumishi '***njema kwelikweli***' kimeundwa kwa *kivumishi* + *kielezi.*

b) Nguo aliyonunuliwa ni nzuri kabisa.

Kirai kivumishi ***'nzuri kabisa'*** kimeundwa kwa *kivumishi* + *kielezi.*

2. ***Kivumishi pamoja na kirai nomino:***

**Mifano:** a) Mwimbaji mwenye sauti laini ameshinda tuzo.

Kirai kivumishi ***'mwenye sauti laini'*** kimeundwa kwa (*kivumishi* + *kirai nomino*)

b) Mhudumu mwenye kazi nzuri ameongezewa mshahara.

Kirai kivumishi ***'mwenye kazi nzuri'*** kimeundwa kwa (*kivumishi* + *kirai nomino*)

3. ***Kivumishi pamoja na kirai kitenzi:***

**Mfano:** a) Hii ndiyo bunduki yenye kupiga risasi.

Kirai kivumishi ***'yenye kupiga risasi'*** kimeundwa kwa *kivumishi* + *kirai kitenzi*.

b) Huyu ndiye ndovu mwenye kuangusha miti.

Kirai kivumishi ***'mwenye kuangusha miti'*** kimeundwa kwa *kivumishi* + *kirai kitenzi*

4. ***Kivumishi pamoja na kirai kivumishi:***

**Mfano:** a) Niliuziwa ng'ombe mwingine mwenye jicho moja.

Kirai kivumishi kimeundwa kwa *kivumishi* + *kirai kivumishi*.

b) Nitamtuza mwanafunzi mwingine mwenye viatu vyeusi.

Kirai kivumishi kimeundwa kwa *kivumishi* + *kirai kivumishi*.

## Zoezi la 6

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, onyesheni virai vivumishi katika sentensi zifuatazo kisha mwelezane virai vivumishi hivyo vimeundwa kwa maneno gani.*

**Kwa mfano:** Yeye ni kiongozi mwenye ujeuri mwingi.

**Jibu:** Sehemu yenye kirai kivumishi ni '*mwenye ujeuri mwingi*' ambayo imeundwa kwa *kivumishi* + *kirai nomino*.

1. Maksuudi alikuwa fisadi sana.
2. Alileta maembe mengine yenye utamu.
3. Babu mwenye kuuza matunda anakaa wilayani Nyamagabe.
4. Mrembo wetu amesuka zile nzuri kweli.
5. Tajiri mwenye gari kubwa alifariki jana.
6. Wachezaji warefu sana wamekaa jukwaani.
7. Watoto wanyonge wote wamepewa msaada.
8. Mwembamba wao alishinda mbio zile kabisa.
9. Yeye mwenyewe ameharibu mpango wao.
10. Maembe matamu matano yamenunuliwa.

## Zoezi la 7

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tungeni sentensi tano sahihi zenye miundo mbalimbali ya virai vivumishi.*

**Kwa mfano:** Mlevi ***mwenye hasira nyingi*** ameondoka.

**Jibu:** Sehemu yenye kirai kivumishi ni '***mwenye hasira nyingi***' iliyoundwa kwa kutumia kivumishi (*mwenye*) pamoja na kirai nomino (*hasira nyingi*).

# Somo la 4: Utanzu wa tamthilia

## 4.1 Sura moja ya tamthilia

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, tazameni mchoro huu kisha msome sura moja ya tamthilia ya* ***Kijiba cha Moyo*** *(iliyoandikwa na Timothy Arege) na baadaye mjibu maswali ya ufahamu yanayofuata.*



*(Baadaye siku ile ile. Nyumbani kwa wazazi wake Sele. Zainabu yuko ukumbini ameketi kwenye kochi huku akifuma kitambaa. Kuna mbisho mlangoni.)*

**Bi. Rahma**: (*Anaubisha mlango.)* Hodi! (*Kimya. Baada ya muda anabisha tena.*) Hodi! (*Kimya vile vile. Mara ya tatu anabisha kisha sauti yake inasikika.*) Hodi! Wenyewe mpo? (*Zainabu anaondoka mbio kwenda kuufungua mlango.*)

**Zainabu**: (*Akielekea mlangoni.*) Karibu. (*Anaufungua mlango. Anachangamka anapomwona Bi. Rahma.*) Shangazi, karibu ndani. Karibu!

**Bi. Rahma**: Asante. Asante mwanangu (*Wakisalimiana kwa mikono.)* Hii ilikuwa hodi ya mwisho. Nilipoita ya pili pasi kuitikiwa niliona hamna mtu lakini alhamdulilahi, nashukuru nimekupata.

**Zainabu**: (*Akimwelekeza penye kiti.)* Karibu shangazi. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya na uzima. (*Wanaketi kutazamana.)* Nyumbani hawajambo?

**Bi. Rahma**: Hawajambo mwanangu. Niliona mmenyamaza sana hivyo nikaamua niwajulie hali.

**Zainabu**: Umefanya vizuri shangazi kuja kutujulia hali.

**Bi. Rahma**: Vipi watoto?

**Zainabu**: Hawana neno ila Sele kidogo ametutia wasiwasi.

**Bi. Rahma**: (*Kwa mshangao.)* Wasiwasi?

**Zainabu**: Si… ni kama … kama wasiwasi niseme.

**Bi. Rahma**: Anaumwa?

**Zainabu**: Hata sijui. Sisi tunamwona kama anayeumwa lakini yeye anasema haumwi.

**Bi. Rahma**: Wala ugonjwa haumlazi ndani?

**Zainabu**: Hata kidogo! Ila mara nyingi huwa mumo humo ndani peke yake. (*Kimya.)* Ni kama anayejitenga na watu…

**Bi. Rahma**: Kumbe ndiyo maana kwangu hatii guu!

**Zainabu**: Ingawa halalamiki kuumwa popote, hamu ya chakula imemwisha. Mara nyingi anakitazama tu na kama akila basi atakigusagusa mara mbili tatu na kukiacha…

**Bi. Rahma**: Hamu ya chakula nayo wajua wakati mwingine hutegemea mpishi. Nyinyi siku hizi hamna muda kukiandaa chakula. Mnafukuzilia hekaheka nyingi. Na hao wanawake wa kisasa ndo basi. (*Kimya.)* Hata muda wa kuandaa mapishi ya kisawasawa hawana. Umeliwa na hizi nenda rudi zenu nyingi. Watavilaje vyakula vya kuharakishwa? Heri huvutwa kwa subira mama. Vyakula visivyopata kutua sufuriani, vipi vitatua moyoni?

**Zainabu**: Shangazi, ni kweli zipo shughuli nyingi lakini zenyewe hazinizuii kuiandalia familia yangu chakula kizuri. Hata huyo Aisha mwenyewe siwezi kusema hafanyi inavyomjuzu. Anajitahidi sana. (*Kimya.)*

**Bi. Rahma**: Au labda mkono ni ule ule mmoja wa upishi. Usisahau kuwa mchele mmoja lakini mapishi mengi. Hili hukipa upya na ugeni chakula.

**Zainabu**: Hilo hatujalisahau. Aisha huandaa biryani akiwa na muda wa kutosha. Mara nyingine wali mweupe, mara nyingine pilau au hata chapati. Nani anayemshinda hapa katika upishi wa vitumbua au hata viazi karai? (*Kimya.)* Kuridhika kwa familia ndiyo raha yetu. Ila Sele naye ana mienendo ya ajabu siku hizi. Si kwa sababu ya chakula! La hasha!

**Bi. Rahma**: Nini basi? Labda ni kitoweo.

**Zainabu**: Hata kitoweo chabadilishwa. Kama si pojo ni nyama; si ya kuku, si ya ng'ombe au samaki... mara wa kupaka, mara wa kukaanga...

**Bi. Rahma**: Tafi!

**Zainabu**: Si tafi tu. Hata kambare. Wakati mwingine pweza.

**Bi. Rahma**: Hata vidagaa si vibaya.

**Zainabu**: Hivyo ndo hali kabisa basi. Anavichukia.

**Bi. Rahma**: Havipendi?

**Zainabu**: Anasema anavipenda sana…

**Bi. Rahma**: Basi mpikie hivyo na sima. Si chapati na wali tu mwanangu!

**Zainabu**: Shangazi, Sele ana tabia za ajabu sana siku hizi kama nilivyokueleza. Anasema eti anawaonea dagaa huruma kuliwa na papa na yeye pia awale. (*Kimya.)* Anasema huku ni kuonewa maradufu. Anasema… anasema… eti tena kuwa hapendi vinavyoliwa huku vinatazama tu.

**Bi. Rahma**: (*Amekinaishwa na maelezo haya.)* Basi mgonjwa kweli. Vipi mtu akihurumie kitoweo? (*Kimya. Ana wazo jipya.)* Mbona basi usimpikie papa alipize kisasi kwa niaba ya vidagaa? (*Wote wanacheka. Kisha kimya.)* Sasa utafanya nini? Basi mpikie hao papa.

**Zainabu**: Hao hataki kuwaona kabisa!

**Bi. Rahma**: Nao wana nini tena?

**Zainabu**: Sasa hao nao anadai wana nafsi zisizo zao. Eti wanaishi kwa kutegemea nafsi za vidagaa na hivyo kuwala si tofauti na kuvila vidagaa. Hivyo vidagaa vitakuwa vimeliwa mara ya pili! Hapendi hili kabisa.

**Bi. Rahma**: Hiyo sasa itakuwa nafsi ya vidagaa katika papa au ni pepo za hao vidagaa katika papa?

**Zainabu**: Yeye haonyeshi tofauti. Leo atasema ni nafsi lakini kesho atasema ni pepo. *Kimya kirefu kiasi.)*

**Bi. Rahma**: Basi Sele ni mgonjwa. Apelekwe kwa mganga apate dawa.

**Zainabu**: Dawa gani kwa mtu asiyeumwa?

**Bi. Rahma**: (*Anamtazama Zainabu kwa makini. Kwa sauti ya chini.)* Zamani kidogo angefaa kufanyiwa kafara. Siku hizi kafara ni haba maana mashetani wamepungua. (*Kimya. Kama anayekumbukia kitu.)* Bora zaidi apungwe kuwaondoa pepo. Kafara tu haitoshi. Kama kweli ni pepo waliomwingia ni lazima yeye kupungwa.

**Zainabu**: Haina neno kumtafuta mganga. Unamfahamu mganga mzuri?

**Bi. Rahma**: (*Baada ya kufikiri.)* Hawapo tena wa kama zamani lakini huenda wapo. (*Anamtazama Zainabu usoni.)* Hata hivyo, mchunguze Sele kwa makini. Huenda tatizo lake ni yeye. Labda hajielewi. Au labda yote mawili. Na ikiwa ni yote mawili basi ni hatari zaidi. Kama uliyonieleza ni kweli, basi namwona kama ambaye anafukuzana na kivuli chake. Kwa kuwa sasa ana mke, mwachie alichunguze tatizo lake kwa

makini. Tusifanye halahala. Hata mwenyewe nitataka kusema naye mara kwa mara. Kwa sasa tuanze na huyo mke wake.

**Zainabu**: Haya! Nitamwambia Aisha…

**Bi. Rahma**: Huenda itasaidia.

**Zainabu**: Huenda itasaidia ndiyo, ila huyo mkewe naye haelekei kutoa habari za kutupa mwelekeo wowote. Watoto wa siku hizi wanapenda kuyaweka siri mambo yawahusuyo. Si kama wakati wetu. Hatukuwaficha wazee wetu hata moja wala hatukuwapinga katika maamuzi na ushauri waliotupa. Hawa wa leo ni mpaka mbishane. Nidhamu tuliyokuwa nayo hawana tena. (*Anarejelea kufuma.)*

**Bi. Rahma**: Hawa hiyo ndiyo dunia yao. Wewe ulikuwa na yako wakati wako. Mimi vile vile. Na hiyo ndiyo dunia. Mfano wa mto. Maji yaliyoujenga mto jana ni tofauti na yanayoujenga leo. Vivyo hivyo ya kesho yatakuwa tofauti lakini bado mto utakuwa ni ule ule. Tofauti hatuioni ila kwa mwenye moyo wa kupembua. (*Mara anaingia Aisha mbio. Anamsalimu Bi. Rahma haraka haraka.*)

**Aisha**: (*Akimsalimu.)* Aah Bibi. Shikamoo!

**Bi. Rahma**: Marahabaa! Marahabaa mama. Hali gani mjukuu wangu?

**Aisha**: Nzuri. Hamna neno. (*Baada ya kumsalimu anaelekea upande wa pili wa chumba. Anaanza kuchakura vitabu pembeni. Muda huu wote, wote wawili wamemtazama.)*

**Zainabu**: Aisha!

**Aisha**: Beee! (*Ameinamia rundo la vitabu bado.)*

**Zainabu**: Tabia gani hii? Hata kama ulikuwa hapa mapema watoka utokako unafululiza moja kwa moja hadi penye vitabu! Humwoni bibi hapa? Kuna nini?

**Aisha**: (*Akiendelea na shughuli zake.)* Hamna kitu.

**Zainabu**: Hamna kitu?

**Bi. Rahma**: Aisha, desturi gani hii? Mtoto utoke kule nje sisi wazee wako tuko hapa kisha utupuuze na kuelekea kwenye vitabu! Ndivyo elimu yenu hii ya Kizungu inavyowatuma kufanya? Huo ndio ustaarabu kwenu?

**Aisha**: Si hivyo. Kuna jambo ambalo aliniambia Sele nami nikawa silielewi vizuri. Nikataka nilifuatilie na kupata usuli wake kabla sijasahau.

**Zainabu** : (*Kwa ukali.)* Jambo tu la kuambiwa ndilo linalokufanya utuone sisi kama vitu tu! Linakufanya utuvunjie heshima sisi wazee wako! Eeh!

**Bi. Rahma**: (*Kwa Zainabu.)* Jambo gani ambalo asingetuuliza sisi tukampa ufafanuzi? (*Kwa Aisha.)* Elimu hiyo mnayoitafuta na kuilipia vitabuni sisi mnatudharau ndo tunayo hapa. (*Aisha anamtazama.)* Wameitoa kwetu wakaitia humo na nyinyi sasa inawafanya kuwa na kiburi bila kufahamu kuwa waliyochota kutoka hapa (*Anaashiria kichwa.)* ni kidogo tu. Ni kama kisima. Kila mtu atachota na kila kiumbe kunywa kipendavyo lakini maji yake hayaishi.

**Aisha**: Sivyo bibi. (*Kimya.)* Baada ya kusema na Sele kuna jambo alilosema nami nikahisi kama nimelisikia au nimelisoma mahali ila sikuwa na hakika. Nikaona kuwa nikiliachia litanichenga na kunitoka akilini maana ninahisi kama ninayechezewa mchezo fulani wa mawazo na maneno yake. Na mimi fikra zikanielekeza katika maandishi fulani ambayo sikumbuki vizuri kama yalikuwa kitabu au kitumeme. Ndiyo sababu ya kunifanya nije moja kwa moja mpaka hapa. Samahani sana. (*Kimya.)*

**Zainabu**: Jambo gani hilo hasa?

**Aisha**: Jambo dogo.

**Bi. Rahma**: Dogo ilhali linakufanya utupuuze sisi? Usipochunga utakuja tumwa kwangu nikutie skuli. Haya!

**Aisha**: Ni kama dogo si dogo; kubwa si kubwa. Mara nahisi ni dogo mara kubwa. (*Kimya. Anasonga kando na kuanza kuzungumza peke yake.)* Kama lililotiwa hamira, linafura na kujaa fikirani. Kichwa kinakuwa kizito kama nanga. Hapa naona panahitaji upekuzi. (*Kimya. Anarejea alipokuwa mwanzo.)*

**Zainabu**: Aisha!

**Bi. Rahma**: (*Anashituka*) Naam mama!

**Zainabu**: Na wewe umekuwa kama huyu mume wako?

**Aisha**: Hata kidogo!

**Bi. Rahma**: Mambo ya watoto! Wala hamna jambo dogo na kubwa. Ukubwa na udogo wa jambo hutegemea namna lilivyomtua mtu moyoni. Hiyo ndiyo tofauti ya ukubwa au udogo wa jambo.

**Zainabu**: Haswa! Aisha, hebu tuambie kimasomaso mbele ya bibi yako tatizo la mwenzako. Hivi anakuambia ana nini? (*Anaonekana mwenye fikra nyingi.)*

**Aisha**: Hasemi. Huwa tunazungumza tu ingawa siyaelewi mengi ya yale anayosema. Ni kama haya hivi yaliyonileta hapa. (*Wote wanamtazama kwa muda.)*

**Bi. Rahma**: Ni yepi hayo yaliyokuleta huku?

**Aisha**: (*Baada ya muda.)* Kuhusuuu… kuhu… kuhusu papa.

**Zainabu**: (*Kama aliyeshtuka.)* Papa tena?

**Bi. Rahma**: Papa upanga au papa ndege? (*Kimya.)*

**Aisha**: Papa tu.

**Bi. Rahma**: Basi kamuulize.

**Aisha**: Ningemuuliza, ila hapendi maswali mengi.

**Bi. Rahma**: Basi mrai. Mwanamke ni ulimi. Lakini utayajuaje haya kama mwenendo ndio huu unaotuonyesha? (*Anageuka kumtazama Aisha.)* Moyo wa mtu nyumba na mambo ya nyumba kweli kunga. Lakini siri za nyumba azijuaye mwenyewe. Usipozijua wewe atazijua nani? (*Kimya.)* Utie ulimi asali na atakueleza kila kitu. Utamtoa nyoka pangoni mama. Hapana jambo kubwa kwa mwanamke kulipata. Ulimi wa nini basi?

**Aisha**: Lakini bibi huyo alikuwa mwanamke wa jana! Mwanamke wa siku hizi tofauti. Anakwenda na majira ya usasa. Hana tofauti na mwanamume.

**Zainabu**: Bi mkubwa wasichana wetu hawa si kama zamani tena. Wanashindana na wanaume…

**Bi. Rahma**: Sisi hizo ndizo kunga tulizofundishwa. (*Kwa Zainabu huku akiinuka.)* Mimi naenda kumtazama nione hali yake hiyo. Na wewe mwanangu anza kutapatapa ukatafuta waganga. (*Anageuka na kumtazama Zainabu.)* Umesikia mwanangu?

**Zainabu**: Nimesikia.

**Bi. Rahma**: Haya! Usikawie sana. Utakuja chekwa.

**Zainabu**: Tayari wamekuja madaktari hapa wakamwona ila Sele mwenyewe haamini kama anaumwa. Wala hao madaktari nao hawaelezi waziwazi kama Sele ana nini. Sijui kama kwa kupenda au kushindwa kueleza.

**Bi. Rahma**: Madaktari si wajinga. Usiwaone wametulia vile. Washindweje nao ndo manyakanga?

**Zainabu**: Nini basi?

**Bi. Rahma**: Mimi nitajuaje? Wanajua wao wenyewe. (*Anaondoka.)*

**Zainabu**: (*Kwa Aisha.)* Aisha!

**Aisha** : Beka!

**Zainabu**: Mwandalie bibi chai na vile vitumbua vilivyobaki asubuhi. Usimsahau Sele. Labda akimwona bibi yake atakula kidogo.

**Aisha**: Nitawaandalia. (*Anaondoka. Zainabu anarejelea kufuma kitambaa.)* *(Giza)*

## Maswali ya ufahamu

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, someni tena sura moja ya tamthilia mliyosoma hapo awali kisha mjibu maswali yafuatayo.*

1. Onyesho hili lina wahusika wangapi?
2. Eleza uhusiano uliopo kati ya Bi Rahma na Zainabu.
3. Eleza uhusiano uliopo kati ya Aisha na Bi Rahma.
4. Sele ana matatizo gani?
5. Ni mambo gani yanayowafanya wanawake wa zama hizi wasishughulike na huduma za nyumbani?
6. Jadili sifa za Zainabu.
7. Jadili mawazo makuu yanayojadiliwa katika sura ya tamthilia mliyosoma.
8. Aisha na Sele wana uhusiano gani?
9. Eleza sifa za Aisha.
10. Bi Rahma ana itikadi gani kuhusu matibabu ya Sele?

## 4.2 Msamiati kutokana na sura moja ya tamthilia husika

### Zoezi la 1

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, tafuteni msamiati mpya kutoka katika sura ya tamthilia mliyosoma hapo awali kisha mweleze maana zao na kutunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno hayo. Zingatieni muktadha wa sura husika na mnaweza kutumia kamusi inapohitajika.*

**Kwa mfano:**

***papa*** - samaki wa baharini asiye na magamba, mwenye ngozi nene.

***Matumizi katika sentensi:*** Sele alikataa kula ***papa***.

## Zoezi la 2

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, tumieni mshale kwa usahihi kuonyesha maana za msamiati wa maneno katika sehemu ya A.*

| Sehemu A. (msamiati) | Sehemu B. (Maana) |
|---|---|
| 1. punga | A. fanyia mgonjwa tiba |
| 2. upekuzi | B. salamu ya heshima |
| 3. dagaa | CH. kuwa katika utulivu |
| 4. bisha | D. neno la kumfanya mtu asikilize |
| 5. tua | E. shindana |
| 6. kafara | F. taarifa ya kueleza chanzo cha kitu |
| 7. tafi | G. ishara ya kusalimia, pepea |
| 8. eti | H. samaki wadogowadogo |
| 9. shikamoo | I. hali ya kutafutatafuta kitu |
| 10. usuli | J. sadaka inayotolewa kwa mizimu |

## 4.3 Matumizi ya lugha: Sifa bainifu za tamthilia

## Zoezi la 3

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, jadilini:*

a) *Sifa bainifu za utanzu wa tamthilia.*

b) *Tofauti kati ya utanzu wa tamthilia na utanzu wa riwaya.*

### Maelezo muhimu

- ***Tamthilia*** ni mchezo wa kuigiza unaochorwa kwa mazungumzo baina ya wahusika na huwa na sura, matendo na maonyesho mbalimbali.
- Mwandishi hufafanua mandhari au sehemu ambapo vitendo vitaigiziwa.
- Maonyesho yake yanalenga kuibua hisia za hadhira.
- Tamthilia huwa na dhamira kuu na dhamira ndogo pamoja na mhusika mkuu na wahusika wadogo.
- Ni muhimu maonyesho ya tamthilia yawe na udhati, yaani, yaashirie hali halisi ya mambo katika jamii. Mara nyingi, tamthilia huwa haionyeshi vitendo vya kiajabuajabu kama vile: mtu kuwa na mbawa na kupaa angani n.k.
- Mwandishi hulipanga jukwaa lake vizuri ili msomaji au mtazamaji aweze kuelewa vizuri kila kitendo na kila onyesho.

## Zoezi la 4

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, someni tena sura ya tamthilia mliyosoma hapo awali kisha mwelezane iwapo mwandishi wa sura hiyo alizingatia sifa bainifu za tamthilia kama zilivyoelezwa hapo juu kwenye maelezo muhimu.*

**Mfano:** Katika sura hii tuliyosoma, kuna mazungumzo baina ya wakusika Aisha, Zainabu na Bi. Rahma.

## Zoezi la 5

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, jadilini mchango wa tamthilia ya Kinyarwanda '**Urunana**' yenye wahusika kama vile: Aline, Nadine, Stefano n.k. katika kuimarisha hatua za kujikinga dhidi ya ugonjwa wa Ukimwi.*

*Kila kikundi kiwasilishe majadiliano yao mbele ya wanafunzi wenzao darasani.*

## 4.4 Kusikiliza na kuzungumza: Maigizo

## Zoezi la 6

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, someni tena onyesho moja la tamthilia mlilosoma hapo awali kisha mjaribu kuliigiza jukwaani. Hakikisheni kuwa mnafuata mpangilio wa mazungumzo na matukio ya mwandishi.*

## Zoezi la 7

*Kwa kurejelea tamthilia ya '**Urunana**', katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadilini mambo yafuatayo:*

a) Tabia za wahusika: Stefano, James na Nadine.

b) Je, tamthilia ya '***Urunana***' inaweza kuwasaidia vijana katika kujikinga dhidi ya ugonjwa wa Ukimwi? Jadili kwa kutoa mifano ya kutosha.

### Maelezo muhimu

- Wahusika wasiobadilika kutoka mwanzo hadi mwisho wa hadithi huitwa ***wahusika bapa***. Kwa mfano: mhusika mbaya anabakia kuwa mbaya kutoka mwanzo hadi mwisho wa hadithi.
- Kuna aina mbili za wahusika bapa:

  a) Wahusika ambao huonyesha msimamo wao kulingana na masimulizi ya msanii huitwa ***wahusika bapa-sugu***.

b) Wahusika ambao msimamo wao hutambulika kulingana na majina yao huitwa ***wahusika bapa-vielelezo***.

**Kwa mfano:** Mhusika Rehema ni mwenye huruma na neema kutoka mwanzo hadi mwisho wa hadithi.

- Wahusika duara hubadilika kitabia katika fasihi. Hawa huwa hawana msimamo thabiti. Wao hubadilika kulingana na maudhui na mazingira. Wahusika hawa huitwa ***wahusika duara***.

**Kwa mfano:** Msichana aliyeanza akiwa mpole na mwadilifu anapobadilika na kuwa mtovu wa nidhamu, kahaba na asiyeshirikiana na mtu yeyote.

- Wahusika ambao huwa katikati ya wahusika bapa na wahusika duara huitwa ***wahusika wafoili***. Hawa wanaweza kuchukua msimamo fulani katika masuala fulani lakini pia wanaweza kubadilisha msimamo huo wakati mwingine kulingana na hali. Wahusika hawa hutegemea wahusika duara na wahusika bapa ili kutoa sifa zao.

**Kwa mfano:** Wahusika hawa wakiishi na mhusika bapa, wanaweza kuchukua msimamo wa mhusika huyo lakini wakihama na waishi sana na mhusika mwengine, wanabadilika. Wahusika hawa aghalabu huwakilisha uhalisi wa binadamu.

## Zoezi la 8

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, someni tena sura ya tamthilia mliyosoma hapo awali kisha mjadili tabia za wahusika:* ***Aisha, Zainabu na Bi. Rahma*** *huku mkilinganisha tabia zao na maisha yenu ya kila siku.*

## 4.5 Sarufi: Kirai kitenzi

A. *Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, chunguzeni sehemu zilizopigiwa mistari katika sentensi zinazofuata kisha mwelezane sehemu hizo ni za aina gani na zimeundwa kwa maneno yapi.*

**Kwa mfano:** Msichana huyu ameimba vizuri.

**Jibu:** Maneno yaliyopigiwa mstari ni kitenzi na kielezi, hivyo yanaunda ***kirai kitenzi***.

***FAHAMU:*** Neno kuu katika kirai kitenzi ambalo hutangulia huwa ni ***kitenzi***.

1. Babu alikuwa akitusimulia hadithi.
2. Mwalimu angali anafundisha darasani.
3. Mutoni anacheza vizuri.

4. Wakulima wanalima shamba kubwa.
5. Kaka yake anafua nguo zao.
6. Kwa nini unampiga mbwa huyo?
7. Mimi siwezi kula nyama.

*Jadili ugunduzi wenu.*

B. *Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, onyesheni kwa kutumia mifano tofauti kati ya kirai kitenzi na kirai nomino.*

**Kwa mfano:**

***Kirai kitenzi:*** Mtoto mwerevu amepita mtihani. (*kitenzi* + *nomino)*

Neno kuu ni kitenzi.

***Kirai nomino:*** Mtoto mwerevu amepita mtihani. (*nomino* + *kivumishi*)

Neno kuu ni nomino.

## Maelezo muhimu

Fungu la maneno yenye muundo ambao umekitwa katika kitenzi huitwa ***kirai kitenzi***.

**Muundo wa virai vitenzi:**

1. Kitenzi pamoja na kitenzi kingine au vingine:

   **Mifano**: a) Nyanya alikuwa hajamaliza kula. (*kitenzi* + *vitenzi viwili*)

   b) Neza anataka kukimbia (*kitenzi* + *kitenzi kingine*)

2. Kitenzi pamoja na kielezi:

   **Mifano:** a) Mwimbaji huyu anaimba vizuri. (*kitenzi* + *kielezi*)

   b) Babu anatembea polepole. (*kitenzi* + *kielezi*)

3. Kitenzi pamoja na nomino au kirai nomino:

   **Mfano:** a) Baba analima shamba. (*kitenzi* + *nomino*)

   b) Baba analima shamba kubwa. (*kitenzi* + *kirai nomino*)

4. Kitenzi pamoja na Kirai kielezi:

   **Mfano:** a) Mchezaji alikimbia upesi sana. (*kitenzi* + *kirai kielezi)*

   b) Mtoto alilia vibaya sana. (*kitenzi* + *kirai kielezi)*

## Zoezi la 9

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, onyesheni virai vitenzi katika sentensi zifuatazo kisha mwelezane virai vitenzi hivyo vimeundwa kwa maneno gani.*

**Kwa mfano:** Kalisa anakimbia upesi sana.

**Jibu:** Sehemu yenye kirai kitenzi ni '*anakimbia upesi sana*' ambayo imeundwa kwa kitenzi + kirai kielezi (vielezi viwili '*upesi sana*').

1. Mvua iliendelea kunyesha usiku kucha.
2. Mwalimu aliwafundisha wanafunzi kukariri mashairi.
3. Wakulima walipalilia mimea yao.
4. Msichana mrefu alikuwa akipika wali.
5. Wasafiri waliabiri basi jipya.

## Zoezi la10

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, tungeni sentensi tano sahihi zenye miundo mbalimbali ya virai vitenzi.*

**Kwa mfano:** Tajiri mwenye mali nyingi <u>ameondoka haraka</u>.

**Jibu:** Sehemu yenye kirai kitenzi ni '*ameondoka haraka*' iliyoundwa kwa kutumia kitenzi (*ameondoka*) pamoja na kielezi (*haraka*).

# Somo la 5: Utanzu wa ushairi

## 5.1 Shairi kuhusu kuyalinda mazingira

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tazameni picha na michoro hii kisha msome shairi linalofuata kuhusu kuyalinda mazingira yetu na baadaye mjibu maswali yanayofuata kuhusu shairi hilo.*
















### TUYALINDE MAZINGIRA

Mashamba yetu yalindwe, serikali yahukumu,
Popote pale yalimwe, sisi wote tujikimu,
Wanyama nao wafugwe, mazao yake muhimu,
Biashara ifanyiwe, twajua hilo jukumu,
Sote tusimame wima, tuyalinde mazingira.

Kukata miti kusiwe, mimea hiyo muhimu,
Hazina hii yenyewe, ifanya ngambo timamu,
Ulinzi wake ukazwe, tusije kujidhulumu,
Waharibu wasiachwe, miti iwepo kudumu,
Sote tusimame wima, tuyalinde mazingira.

Maziwa yetu yalindwe, nguru na dagaa adimu,
Sangara naye mwenyewe, ni haba kila sehemu,

Mharibu akemewe, ikiwa hana elimu,
Akiwa kweli mkongwe, adhabu ndiyo muhimu,
Sote tusimame wima, tuyalinde mazingira.

Usafi kote upewe, kipao mbele muhimu,
Michafu kote ifutwe, maisha yawe matamu,
Nchini kwetu tusiwe, michafu kila sehemu,
Adui wake avutwe, atiwe fasi maalumu,
Sote tusimame wima, tuyalinde mazingira.

Mabonde nayo yapewe, kuzaa hewa timamu,
Mahindi mengi yapandwe, kote milimani humu,
Njaa na ukame vyangushwe, tufurahi mumu humu,
Ukanda wote ulimwe, kila fasi tabasamu,
Sote tusimame wima, tuyalinde mazingira.

Mazingira ni ya wewe, na kwa kila binadamu,
Mpinzani si mwenziwe, yeye hana la mwalimu,
Atajiua mwenyewe, mbele kuna mashutumu,
Hatajua hata kamwe, kwamba yeye ni dhalimu,
Sote tusimame wima, tuyalinde mazingira.

## Maswali ya ufahamu

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, someni tena shairi mlilosoma hapo awali kisha mjibu maswali yafuatayo.*

1. Andika kibwagizo cha shairi hili.
2. Eleza faida mbili za kilimo kwa binadamu.
3. Jadili faida mbili za ufugaji kwa binadamu.
4. Shairi hili lina beti ngapi?
5. Taja aina tatu za samaki kutokana na shairi ulilosoma.
6. Eleza maana ya ‘Hazina’ kama lilivyotumika kwenye shairi husika.
7. Andika vina vya katikati na vina vya mwisho vya shairi hili.
8. Shairi hili lina mishororo mingapi?
9. Eleza mawazo makuu yanayoangaziwa katika shairi hili.
10. Onyesha mizani katika ubeti wa kwanza wa shairi hili.

## 5.2 Msamiati wa shairi kuhusu kuyalinda mazingira

### Zoezi la 1

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tafuteni msamiati mpya kutoka katika shairi mlilosoma hapo awali kisha mweleze maana zao na kutunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno hayo. Zingatieni muktadha wa shairi husika. Mnaweza kutumia kamusi inapohitajika.*

**Kwa mfano:**

***Ukame -*** hali ya nchi kuwa kavu kiasi cha kutowezesha kupata mavuno.

***Matumizi katika sentensi:*** Ukame umesababisha uhaba wa chakula kijijini.

### Zoezi la 2

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tumieni mshale kuonyesha maana sahihi ya msamiati ulio katika sehemu A kutoka katika sehemu B.*

| Sehemu A: Msamiati | Sehemu B: Maana |
|---|---|
| 1. mashamba | A. mtu mwenye tabia ya ukatili |
| 2. dhalimu | B. mtu aliyeishi miaka mingi |
| 3. mazingira | CH. ardhi iliyolimwa na kupandwa mazao |
| 4. wima | D. sehemu ya nchi iliyopo baina ya milima |
| 5. timamu | E. chache, siyotosheleza, pungufu |
| 6. mabonde | F. mtu aliye dhidi yako |
| 7. hazina | G. yale yote yanayomzunguka binadamu |
| 8. haba | H. kamili, sawasawa |
| 9. adui | I. nyookeka kuelekea juu |
| 10. mkongwe | J. mali, fedha, utajiri wa nchi |

## 5.3 Matumizi ya lugha: Sifa bainifu za shairi

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadilini:*

a) *Sifa bainifu za utanzu wa ushairi.*

b) *Tofauti kati ya utanzu wa ushairi na utanzu wa riwaya.*

## Zoezi la 3

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadilini vina, kibwagizo, beti, mizani, mishororo na mawazo makuu yaliyoangaziwa katika shairi mlilosoma hapo awali.*

## Maelezo muhimu

Sanaa ya lugha teule na lugha ya kisanaa inayotumia mpangilio na uteuzi maalum wa maneno na sauti ili kupitisha ujumbe fulani huitwa ***shairi***.

Shairi huwa na vipashio vifuatavyo:

- ***Vina*** - silabi za mwisho wa kila kipande katika mshororo.
- ***Mizani*** - idadi ya silabi katika maneno ya kila mshororo.
- ***Mshororo*** - mstari mmoja wa maneno katika ubeti wa shairi.
- ***Ubeti*** - kifungu cha mishororo kadhaa.
- ***Mloto*** - mshororo wa pili katika ubeti
- ***Kimalizio/ Kiishio*** - mshororo wa mwisho katika ubeti usiorudiwarudiwa katika kila ubeti.
- ***Kibwagizo*** - mshororo wa mwisho katika ubeti unaorudiwarudiwa kila ubeti.
- Mshairi hufupisha au kurefusha maneno ili kutosheleza idadi ya mizani.

## 5.4 Kusikiliza na kuzungumza: Kukariri shairi

## Zoezi la 4

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, karirini shairi mlilosoma hapo awali kwa kutumia mahadhi tofauti tofauti. Kila mwanafunzi alighani shairi hilo mbele ya wanafunzi wengine darasani.*

## 5.5 Sarufi: Maana ya kishazi

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, chunguzeni sentensi zifuatazo kisha mwonyeshe sehemu za sentensi hizo ambazo zinaweza kuwa sentensi kamili bila ya kuwepo kwa maneno mengine na sehemu zisizoweza kuwa sentensi kamili bila ya kuwepo kwa maneno mengine.* **Kwa mfano:**

i) *Baba amerudi lakini mama amebaki huko.*

**Jibu:** a) Sehemu ya '*baba amerudi*' ni sentensi kamili.

b) Sehemu ya '*mama amebaki huko*' pia ni sentensi kamili.

**FAHAMU:** Sehemu hizi mbili zimeunganishwa kwa kiunganishi '*lakini*'. Kwa hivyo, sehemu hizo mbili ni ***sentensi kamili*** au ***vishazi huru***.

ii) *Embe lililooza litatupwa kwenye jaa la takataka.*

**Jibu:** a) Sehemu ya '*embe lililooza'* haiwezi kuwa sentensi kamili bali lazima pawepo na maneno mengine ili ikamilike. Hiki ni ***kishazi tegemezi***.

b) Sehemu ya '*embe litatupwa kwenye jaa la takataka'* ni sentensi kamili hivyo hiki ni ***kishazi huru***.

**FAHAMU:** Sehemu moja inajitegemea yenyewe (kishazi huru) ilhali sehemu nyingine haiwezi kujitegemea yenyewe (kishazi tegemezi).

1. Andazi lililotiwa hamira linafura na kujaa vizuri.
2. Wanafunzi waliotia bidii mwaka jana walipita mtihani.
3. Shati alilonunua limefuliwa na dadake.
4. Kalisa anasoma Hisabati ilhali Gatete anachora michoro.
5. Nitawajibika nawe utafaidika.

Kundi la maneno ambalo lina ujumbe uliokamilika au usiokamilika likiwa ndani ya sentensi kuu huitwa ***kishazi***.

Kuna kishazi chenye sentensi moja huru au sentensi mbili huru zinazounganishwa kwa kiunganishi au kishazi chenye sentensi mbili zinazosaidiana kutoa maana kamili.

## Zoezi la 5

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, chunguzeni sentensi zifuatazo kisha mwonyeshe vishazi vinavyojitokeza katika sentensi hizi.*

1. Mwanamke aliyeishi hapa naye alipoteza mtoto wake.
2. Mtoto aliyepoteza maisha jana amepokelewa mbinguni.
3. Gisa alipomaliza masomo ya chuo mwaka jana alipata shahada ya kwanza.
4. Watoto wanacheza na wazazi wamekaa sebuleni.
5. Wavulana walishinda mabao mengi lakini refa amewaonea sana.
6. Kamana alifua nguo zake.
7. Mutoni ataondoka kesho.
8. Ninawapenda wote.
9. Waziri alizindua mkutano.
10. Mwenyekiti alisoma hotuba nzuri sana.

## Zoezi la 6

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, chagueni kitenzi sahihi kutoka kwenye kisanduku hiki kisha mjaze nafasi zilizoachwa wazi kwenye vishazi vifuatavyo.*

aliwadharau, aliyefyatua, angewahi, kutupatupa, alimwandalia, kukabidhiwa, nitamweleza, atapelekwa, tutafurahia, alipigwa kalamu

1. Angelala mapema ________________ kuamka.
2. Aliyekuwa mwenyekiti wetu ________________ jana.
3. Iwapo atapenda kuishi hapa, ________________ kumpokea.
4. Ikiwa nitamwona jioni ________________ makosa yake.
5. Asipotulia tuli, ________________ gerezani.
6. Alifurahi baada ya ________________ cheti cha uzalendo.
7. Mkewe alipofika nyumbani, ________________ chakula kizuri.
8. Aisha alipoingia nyumbani ________________ wazee wote.
9. Waliingia baadaye wakaanza ________________ vitabu vyote huku na kule.
10. Sijajua askari ________________ risasi.

## Zoezi la 7

*Jigaweni katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha mwelezane aina za vishazi mnavyovifahamu pamoja na kuvitungia sentensi sahihi kwa kila aina ya kishazi.*

Kuna aina mbili kuu za vishazi:

a) Vishazi huru
b) Vishazi tegemezi

- Vishazi huru ni sentensi zinazojitegemea, zenye maana kamili.

**Mifano:** *Wanafunzi wanafanya mtihani **na** walimu wanasahihisha karatasi.*

- Vishazi tegemezi ni vipande katika sentensi kuu ambavyo vikiondolewa katika muktadha wa sentensi kuu, haviwezi kusimama peke yake kama sentensi kamili.

**Mfano:** *Akifunga bao* wote watafurahi.

Sehemu ya '*akifunga bao*' haiwezi kuwa sentensi kamili pekee yake hadi iambatanishwe na maneno mengine.

## Zoezi la 8

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, chunguzeni sentensi zifuatazo kisha mwonyeshe vishazi huru na vishazi tegemezi.*

**Kwa mfano:** Pikipiki iliuzwa lakini gari imerudishwa kiwandani.

**Jibu:** Sehemu ya '*pikipiki iliuzwa*' ni kishazi huru (sentensi kamili) na sehemu ya '*gari imerudishwa kiwandani*' ni kishazi huru (sentensi kamili) pia. Sehemu hizi zimeunganishwa kwa kiunganishi '*lakini*'.

1. Kalisa aliandika vitabu na mkewe aliona asimulie hadithi.
2. Wanawake walianzisha biashara lakini watoto wao hawasomi.
3. Watumishi waliondoka na wake zao walibaki hapa.
4. Tamthilia iliigizwa lakini mwalimu alikuwa nje.
5. Umenitukana tena unanipiga.
6. Sichezi wala sifanyi kazi.
7. Walipoingia walishangaa sana.
8. Angeshinda mtihani huo angepewa ajira.
9. Aliyefundisha si mwalimu wetu.
10. Angaliwekeza kwenye miradi mingi angalipata pesa nyingi.

# Tathmini ya mada ya 1

## Zoezi la 1

1. Jadili sifa bainifu za:
   - a) Utanzu wa riwaya
   - b) Utanzu wa ushairi
   - ch) Utanzu wa tamthilia
   - d) Utanzu wa hadithi fupi

## Zoezi la 2

1. Jadili tofauti zilizopo kati ya:
   - a) Utanzu wa riwaya na utanzu wa hadithi fupi
   - b) Utanzu wa tamthilia na utanzu wa ushairi
2. Eleza tofauti kati ya maudhui na dhamira katika fasihi.

## Zoezi la 3

*Tambua virai katika sentensi zinazofuata kwa kufuata maelekezo yaliyo kwenye mabano.*

**Kwa mfano:** Paka na panya wanachukiana. (*Tambua kirai nomino*)

**Jibu:** '*paka na panya*' ni kirai nomino

a) Mtoto mrefu ameshinda mbio. (*Tambua kirai kitenzi*)
b) Nataka unipe kisu kikali. (*Tambua kirai nomino*)
ch) Sima na wali ni chakula kitamu. (*Tambua virai nomino*)
d) Kalamu yenye rangi ya kijani iko wapi? (*Tambua kirai kivumishi*)
e) Wazee wenye kondoo hawa wamekuja. (*Tambua kirai kivumishi*)
f) Wanafunzi waliondoka alfajiri na mapema. (*Tambua kirai kielezi*)
g) Mama alikuwa amelala. (*Tambua kirai kitenzi*)

## Zoezi la 4

Tambua aina za vishazi katika sentensi zifuatazo.

a) Mama alifika leo alasiri.
b) Mjomba alifika asubuhi lakini hakutuletea mkate.
ch) Wachezaji ambao ni shupavu walishinda.
d) Waziri alifika baada ya watu kuondoka.
e) Tunda lililo tamu litaliwa.

## Zoezi la 5

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadilini umuhimu wa fasihi kwa wanajamii.*

## Zoezi la 6

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, chunguzeni sentensi zifuatazo kisha mchague na kubainisha sentensi zisizo kamili. Elezeni sababu za upungufu wa sentensi mtakazozichagua.*

a) Sisi kama wananchi wazalendo.

b) Waandishi mashuhuri wa fasihi ya Kiswahili Afrika Mashariki.

ch) Kumbukumbu ya siku ya kuzaliwa kwa dada yangu ni leo.

d) Kwa nini hicho pekee?

e) Mbona wewe huli?

## Zoezi la 7

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, bainisheni sehemu kuu za sentensi hizi.*

**Kwa mfano:** Chakula hiki kimepikwa vizuri.

**Jibu:** '*Chakula hiki*' ni kiima na '*kimepikwa vizuri*' ni kiarifu

a) Mwanafunzi mwerevu na mpole ametuzwa na mwalimu mkuu.

b) Shule yetu ya sekondari ina wanafunzi wengi sana.

ch) Choo chao kimesafishwa na topasi yule.

d) Mama na baba wanatazama runinga waliyonunuliwa jana.

e) Mimi na yeye tuna bidii katika masomo yetu.

## Faharasa

**tabasamu:** jaa furaha, kuwa na sura yenye furaha

**shutumu:** laumu

**nguru:** samaki mkubwa mwenye nyama nyingi na rangi nyeupe sehemu za tumbo

**hazina:** fedha au mapato, idara inayosimamia fedha zote za serikali

**imarisha:** fanya madhubuti

**ngiri:** mnyama mwitu wa jamii ya nguruwe mwenye meno mawili marefu yaliyochomoza

**nungu:** mnyama mdogo ambaye mwili wake umefunikwa na miba mingi

**twiga:** mnyama mrefu zaidi wa Bara la Afrika mwenye rangi ya kahawia na mabatomabato meusi, miguu na shingo ndefu

**pembezoni:** kandokando ya mahali

**msanii:** mtu mwenye ujuzi wa kuchora, kutunga au kuchonga

**sanaa:** uhodari wa kuwasilisha hisia za binadamu kwa maandishi, michoro au uchongaji

**mshororo:** mstari katika ubeti wa shairi

**changamoto:** jambo lililomkabili mtu kulifanya

**sarafu:** vipande vya fedha au shaba ambavyo hutumika kama pesa

**fisidi:** tumia kitu au mali vibaya

**shangwe:** shamrashamra na tamasha za shughuli za sherehe

**kani:** shangwe za kusherehekea jambo la furaha

**kigugumizi:** usitaji katika kuongea au kusoma

**hamaki:** hasira

**umande:** unyevu au majimaji yanayoanguka juu ya ardhi wakati wa usiku

**ujasiri:** utendaji wa jambo bila kuogopa; ushujaa

**chicha:** mabaki ya nazi iliyokunwa baada ya kukamuliwa tui

**hamasa:** hamu na shauku ya kufanya jambo

**kochi:** kiti cha kutosha mtu mmoja au kirefu cha wati zaidi chenye sehemu ya kuwekea mikono pembeni

**pojo:** punje ndogondogo za jamii kunde zenye rangi ya kijani

**maradufu:** mara mbili kwa idadi, nguvu, ubora, umbo n.k.

**papa:** samaki mkubwa wa baharini anayeogopewa na samaki wengine

**hisi:** tambua kwa njia ya ngozi au milango ya fahamu

# SURA YA PILI

**MADA KUU 2:** **FASIHI KATIKA KISWAHILI**
**MADA NDOGO:** **Uhakiki wa tanzu za fasihi andishi**

## Somo la 6: Uhakiki wa fasihi

### 6.1 Kifungu kuhusu fasihi katika Kiswahili

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tazameni michoro hii kisha msome kifungu cha habari kifuatacho kuhusu tanzu mbalimbali za fasihi na baadaye mjibu maswali ya ufahamu.*







Fasihi huelezwa na watu mbalimbali kwa maana tofauti. Hata hivyo, lengo kuu ni kuweka wazi fasili zote za dhana hii. Fasihi ni sanaa inayotumia lugha kama malighafi yake makuu kwa lengo la kueleza maisha ya binadamu kwa njia ya usanii na ufundi unaothiri na kusisimua msomaji na mtazamaji. Ni sanaa kwa kuwa fasihi hutumia lugha kwa njia ya kipekee na kufundisha ujumbe hasa kwa lugha ya kitamathali kama vile: methali, jazanda, stiari, istiara, takriri, misemo, nahau na matumizi mengineyo.

Fasihi hugawanyika katika makundi mawili: Fasihi andishi na fasihi simulizi. Fasihi andishi ina tanzu zifuatazo: tamthilia, riwaya, hadithi fupi na ushairi. Riwaya huandikwa kwa njia ya nathari, huwa ndefu, ina wahusika wengi, mandhari mapana, matumizi mengi ya lugha kutokana na maudhui yake mengi na wahusika wake huwa wameelezwa kwa kina. Tamthilia ni mchezo wa kuigizwa na hujikita sana kwenye matendo na mbinu za kidrama. Hadithi fupi huhusisha matukio machache yanayoendeshwa na wahusika wachache ikilinganishwa na riwaya. Ushairi nao hutumia lugha teule kupitisha ujumbe kwa njia ya kisanaa.

Fasihi simulizi ina matawi mengi. Hii ndiyo fasihi kongwe sana ulimwenguni. Mifano ya tanzu za fasihi simulizi ni kama vile: hadithi, maigizo, ushairi na semi. Kila mojawapo wa tanzu hizi ina vipera vyake. Vipera vya hadithi ni pamoja na: hadithi za kubuni na hadithi za kihistoria. Vipera vya maigizo ni pamoja na: miviga, michezo ya jukwaani, ngomezi, utani, majigambo, vichekesho, ulumbi na ngonjera. Ushairi huhusisha: nyimbo, maghani, sifo, ngonjera n.k. Huu ni utanzu ambao vipera vyake vina vijipera vingi sana. Kwa mfano, kipera cha nyimbo kina vipera kama vile: bembelezi, nyiso, hodiya, mbolezi, nyimbo za harusi, nyimbo za jadiya, nyimbo za mapenzi n.k.

Utanzu wa semi una vipera vifutavyo: methali, vitanza ndimi, misimu, misemo, lakabu, nahau na mafumbo. Kama tulivyosema awali, fasihi simulizi ni pana na yenye vitanzu vingi mno.

Fasihi andishi na fasihi simulizi huwa na dhima kuu kwa jamii husika. Fasihi huwazindua wanajamii kupigania haki zao kupitia michezo ya kuigizwa, methali na vipera vingine. Kupitia kwa nyimbo, watu huhimizwa kupigania haki za kujitawala kiuchumi na hata kijamii. Aidha, fasihi huhimiza uzalendo na uananchi kwa wanajamii. Kwa mfano, kupitia kwa methali '*mjenga nchi ni mwananchi'*. Lengo hapa ni kuhimiza mtu kuipenda nchi yake na kujitolea kwayo.

Fasihi huhifadhi historia na utamaduni wa jamii. Kwa mfano, '*mwacha mila ni mtumwa'* ni methali inayomhimiza mtu kuhifadhi utamaduni wake. Fasihi pia ina dhima ya kuelimisha jamii.

Fasihi hukosoa na kuwakanya wanajamii dhidi ya tabia fulani zisizokubalika katika jamii. Kwa mfano, methali, '*usiache mbachao kwa msala upitao'* ni methali inahimiza watu wasikimbilie mambo mapya na kusahau waliyoyazoea na ambayo wamekuwa nayo tangu zamani. Mbali na kuburudisha kupitia kwa nyimbo, vitendawili na vitanza ndimi, fasihi pia huweza kukuza umoja ama ushirikiano baina ya watu katika jamii. Nyimbo na maagizo huweza kuwaleta watu pamoja na kuwafanya wawe na ushirikiano.

Maudhui ni muhimu katika kazi yoyote ya fasihi. Maudhui ni jumla ya mambo yote yanayozungumziwa katika kazi ya fasihi. Kila utanzu ama kipera huzungumzia kitu fulani na humo ndimo kuna funzo. Kwa mfano, kutokana na methali '*usimwage mtama penye kuku wengi*', maudhui haya yanazungumzia ukulima na ufugaji. Kuna ukulima wa mtama na ufugaji wa kuku. Tunaweza kuelewa ya kwamba hii ni jamii ya wakulima na wafugaji. Haya yaliyozungumziwa ndiyo yanayoitwa ***maudhui***.

Wahusika ndio hutumiwa kuendeleza na kukuza maudhui na dhamira katika kazi ya fasihi. Wahusika ni viumbe katika kazi ya fasihi wanaosema na kutenda matendo kwa niaba ya jamii husika. Wahusika wanaweza kuwa binadamu, wanyama, vitu,

sauti n.k. Wahusika huwa na dhima ya kuzungumza kwa niaba ya mwandishi ama jamii. Usimulizi huwahusu wao pamoja na tabia zao ili kudhihirisha mafunzo yanayolengwa na mtunzi wa fasihi husika.

Wahusika huweza kuainishwa kwa njia mbalimbali. Kimsingi, tuna wahusika wakuu na wahusika wadogo. Wahusika wakuu ni wale ambao hukuza migogoro na mengi katika fasihi husika yanawahusu wao. Wahusika wadogo huwasaidia wahusika wakuu kutekeleza majukumu yao. Ndiyo maana kuna wahusika wasaidizi. Wahusika pia wanaweza kuainishwa kikazi. Kikazi, tunaweza kuwa na wahusika kama vile: wahusika nguli, wapinzani, wasaidizi, bapa n.k. Mhusika nguli ni yule anayesimamia maadili na masuala muhimu ambayo jamii husika inawakilisha. Mhusika mpinzani ni yule ambaye humpinga mhusika nguli na kumwekea vikwazo.

## Maswali ya ufahamu

1. Jadili maana ya fasihi.
2. Taja tanzu mbili kuu za fasihi.
3. Kulingana na kifungu ulichosoma, vipera vya hadithi ni ______________ na ______________.
4. Taja vipera viwili vya utanzu wa ushairi.
5. Fafanua tanzu za fasihi andishi.
6. Kulingana na kifungu ulichosoma, riwaya ina sifa gani? Eleza sifa tatu.
7. Eleza umuhimu wa fasihi kwa jamii kulingana na uliyoyasoma kwenye kifungu husika.
8. Fafanua maudhui huhusisha nini katika fasihi.
9. Eleza maana ya wahusika.
10. Wahusika wana majukumu gani katika fasihi?

## 6.2 Msamiati kuhusu fasihi katika Kiswahili

### Zoezi la 1

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tafuteni msamiati mpya kutoka katika kifungu cha habari mlichosoma hapo awali kisha mweleze maana zao na kutunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno hayo. Zingatieni muktadha wa kifungu hicho. Mnaweza kutumia kamusi inapohitajika.*

**Kwa mfano:**

***Sanaa*** - ufundi wa kuwasilisha hisia na mawazo ya binadamu kwa maandishi, michoro au uchongaji.

***Matumizi katika sentensi:*** Mwanafunzi aliombwa na mwalimu kueleza maana ya ***sanaa*** ya ufinyanzi.

## Zoezi la 2

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, chagueni jibu sahihi kutoka kwa yaliyo hapa chini kujazia nafasi zilizoachwa wazi katika sentensi zinazofuata.*

***uongozi mzuri, fasihi, fasihi andishi, kuhakiki, vina, mizani, wahusika***

**Kwa mfano:** Maudhui makuu katika riwaya tuliyosoma ni ________________ .

**Jibu:** Maudhui makuu katika riwaya tuliyosoma ni ***uongozi mzuri***.

1. Kuna ___________ ya aina mbili; fasihi simulizi na fasihi andishi.
2. Riwaya, tamthilia, novela na hadithi fupi ni tanzu za ________________.
3. Mwalimu alisoma na ___________ kazi ya fasihi na wanafunzi wake.
4. ___________ na ___________ hupatikana katika utanzu wa ushairi.
5. ___________ hutumiwa na mwandishi kuyasimulia matukio mbalimbali.

## 6.3 Matumizi ya lugha: Uhakiki wa maudhui katika fasihi

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, jadilini:*

1. *Maudhui katika riwaya yoyote ambayo mumewahi kuisoma.*
2. *Fani katika riwaya yoyote ambayo mumewahi kuisoma.*

### Maelezo muhimu

a) Ujumbe au mawazo makuu ya mwandishi au mtunzi wa kazi ya fasihi kwa wasomaji au watazamaji wake huitwa ***maudhui***.

Mifano ya maudhui: umaskini, elimu, uongozi, ufisadi, uhifadhi wa mazingira na ukulima.

b) Matumizi ya lugha kwa njia tofauti tofauti ili kupitisha ujumbe kwa wasomaji au watazamaji huitwa ***fani***.

Mifano ya matumizi ya lugha huhusisha: matumizi ya methali, nyimbo, chuku, jazanda, tashbihi, takriri, majazi n.k.

## 6.4 Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadilini:*

1. *Tofauti kati ya fasihi andishi na fasihi simulizi.*
2. *Tofauti kati ya tanzu za fasihi andishi na tanzu za fasihi simulizi.*

### Zoezi la 3

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadilini umuhimu wa fasihi simulizi katika jamii.*

## 6.5 Sarufi: Maana ya kitenzi

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, chunguzeni maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi zinazofuata kisha mwelezane maneno hayo ni ya aina gani.*

1. Mpishi alipika chakula kitamu.
2. Yusufu anamsomea babake barua.
3. Mtoto anacheza uwanjani.
4. Nyanya ni mgonjwa sana.
5. Huyu ndiye baba yangu.
6. Babu alikuwa na furaha tele.
7. Paka alikunywa maziwa ya mtoto.

*Je, mmegundua nini?*

### Maelezo muhimu

Neno ambalo hueleza kuhusu kinachofanywa, kilichofanywa na kitakachofanywa huitwa ***kitenzi***. Wingi wake ni ***vitenzi***.

**Mifano ya vitenzi** *kula, cheza, soma, ruka, lala, samehe, onja, pakua, kimbia, andika, fua* n.k.

***Mifano katika sentensi:***

a) Mfanyakazi alilipa deni lake la mwezi uliopita.
b) Mwanafunzi anachora picha ya nyumba yao.

## Zoezi la 4

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tungeni sentensi sahihi kwa kutumia vitenzi vifuatavyo.*

**Kwa mfano:** kuwa

**Sentensi:** Ndovu yule ali***kuwa*** mgonjwa.

1. kuja
2. nyesha
3. ndicho
4. ogopa
5. tembea
6. ongea
7. vuka
8. chokoza
9. onja
10. ni

## Zoezi la makundi

***Mnyambuliko wa vitenzi***

A. *Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, chunguzeni vitenzi vilivyopigiwa mistari katika sentensi zifuatazo kisha mwelezane ugunduzi wenu wa kauli ya vitenzi hivyo.*

i) Mama ana<u>pika</u> chakula cha mtoto.
ii) Mimi nina<u>shona</u> nguo ya dadangu.
iii) Mwanafunzi ana<u>chora</u> picha ya babake
iv) Kaka ana<u>andika</u> barua ya mjomba wake.
v) Ngabo ana<u>soma</u> kitabu cha mwalimu.

B. *Katika makundi yenu, jaribuni kubadilisha vitenzi hivi viwe katika hali ya mtu kumfanyia au kumtendea mtu mwingine kitendo husika.*

**Kwa mfano:** i) Mama anam***pikia*** mtoto chakula.
ii) Mimi ninam***shonea*** dadangu nguo.

*Je, mmegundua mabadiliko gani katika vitenzi vilivyopigiwa mistari hapo juu?*

## Maelezo muhimu

*Hali ya kuongeza herufi maalum au viambishi mwishoni mwa mizizi ya vitenzi ili kupata maana ya ziada iliyo tofauti na ile ya asilia huitwa **mnyambuliko wa vitenzi**. Kuna hali tofauti za kunyambua vitenzi kama vile:*

a) **Hali ya kufanyia au kutendea:**

Katika hali hii, vitenzi huongezwa viambishi na kupata maana ya kutenda kwa niaba ya.

Kwa mfano:

| Hali ya kufanya/kutenda | Hali ya kufanyia/kutendea |
|---|---|
| pika | pikia |
| shona | shonea |
| imba | imbia |
| andika | andikia |

**Mifano katika sentensi:**

1. Nilimw***andikia*** mama barua.
2. Maria alimw***imbia*** mtoto wimbo akalala.

## Zoezi la 5

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, chunguzeni mabadiliko katika vitenzi vilivyo kwenye jedwali lifuatalo. Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa jibu sahihi.*

| Hali ya kufanya/kutenda | Hali ya kufanyia/kutendea |
|---|---|
| kata | katia |
| leta | ___________ |
| ita | itia |
| ___________ | somea |
| uza | uzia |
| ruka | rukia |
| tembea | tembelea |
| cheza | ___________ |

## Zoezi la 6

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, badilisheni vitenzi hivi viwe katika kauli ya kufanyia/kutendea.*

**Mfano:** lala – lalia

1. fuma
2. vuta
3. kimbia
4. futa
5. pangusa

## Zoezi la 7

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, andikeni sentensi hizi upya kwa kubadilisha vitenzi vilivyopigiwa mstari kuwa katika hali ya kufanyia/kutendea.*

**Mfano:** Mchungaji anawa***chunga*** mbuzi wa jirani.

**Jibu:** Mchungaji anam***chungia*** jirani mbuzi.

1. Msichana anachora picha ya mtoto.
2. Gasimba anakimbia kuelekea shuleni.
3. Mama anafuma fulana ya Mutoni.
4. Mimi ninaandika barua ya babangu.
5. Kesho nitafuta ubao wa darasa letu.

## Zoezi la 8

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, elezeni maana inayojitokeza katika sentensi hizi:*

a) Mama anamchotea maji baba yake.
b) Nitakupigia mpira.
ch) Nyanya anatupikia chakula.
d) Mimi sitawaandikia barua.
e) Kiranja wa darasa letu anamfutia mwalimu ubao.

## Zoezi la 9

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, badilisheni vitenzi hivi viwe katika hali ya kufanya/kutenda.*


**Mfano:** kimbilia – kimbia

a) samehea
b) ondokea
ch) zungumzia
d) limia
e) chumia

# Somo la 7: Wahusika katika fasihi andishi

## 7.1 Hadithi fupi kuhusu urithi wa mali

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tazameni mchoro huu kisha msome hadithi fupi iitwayo '**Kasma Yangu**' (iliyoandikwa na Dumu Kayanda) inayofuata na baadaye mjibu maswali ya ufahamu.*



Sululu kaamka leo moyo ukimtwetatweta. Leo ni leo asemaye kesho ni mwongo. Anapapasapapasa alikoiweka kaptura yake usiku wa kuamkia leo. Vidole vyake vilivyorishai jasho vinakumbana na kaptura yenyewe. Imeanguka kwenye sakafu karibu na mvungu wa kitanda. Anainuka mara moja kitandani na kuivaa kaptura yenyewe, kaptura kuukuu ya kaki iliyoona miaka na mikaka, inayompwaya na yenye viraka vya kila sampuli makalioni na *matamvua* kwenye pindo. Apapasapo tena anakumbana na shati lake lisilokuwa na vifungo. Analivaa mara moja. Mwenyewe katika nyakati za ucheshi wake akiliita shati la marehemu George; akimaanisha Mzungu yeyote wa kule ughaibuni aliyewahi kulivaa shati hilo kabla halijarushwa kwenye mtumba wa nguo kuukuu kuja kuuzwa kwao Chenjeni kwa bei ya kutupa. Lakini leo, Sululu hana ucheshi. Leo si siku ya masihara. Leo ni siku ya kufa na kupona, siku ya patashika nguo chanika na watu kuanguka na kuangukiana, leo ni siku ya siku.

Sululu anamtazama mkewe ambaye bado amejikunja kitandani kama upinde *akiforota*. Analikumbuka joto alilolifaidi kwa kulala pembeni mwa mkewe huyo, mwaka huu wa tano sasa. Miaka mitano iliyobarikiwa kwa vitoto viwili ambavyo vilikuwa vimelala sakafuni kwenye kigunia kichakavu, navyo vinaforota. Miaka mitano ya kupanda na kushuka, ya raha na karaha ya kuishi na mwanamke huyu. Miaka mitano ya kupumbaa kwa hari ya kulala karibu na mwanamke huyu, joto la kiwiliwili cha mwanamke aliyejisabilia kwake na kumnyenyekea yeye kama mume anavyostahili kunyenyekewa. Leo Sululu hana hakika kama haya yataendelea kuwa

yalivyo maana leo ni siku ya siku. Leo nadhari ya Sululu imetua kwenye *kero*, kero ambayo chanzo chake si mwanamke huyu. La! Mwanamke huyu aliyelala pale kitandani akiforota ana kero zake vilevile, kama vile usununu usiokuwa na maana wala msingi, kudai yasiyowezekana, kumnyamazia kwa siku, majuma hata miezi. Lakini baina ya kero na faraja apatazo kwa mkewe, faraja *zinazipiku* kero. Leo lakini lililomkaa moyoni zaidi ni kero kutoka kwa babake mzazi.

Licha ya yeye kuwa mwanamume mzima ambaye ameoa, baba bado amekataa katakata kumkatia kipande cha shamba. Shamba lenyewe kubwa. Wengine huliita 'shamba maddal basari'. Kwa nini mzee huyu hataki kunipa shamba au kunipa urithi wangu? Mbona mimi ni mwanawe kindakindaki ati? Au hana hakika juu ya hilo. Mbona kijiji kizima cha Chenjeni kila kinywa kinasema nashabihiana naye kama shilingi kwa ya pili, sio shilingi ya Kibaki na shilingi ya Moi, ni shilingi ya Kibaki na shilingi ya Kibaki au shilingi ya Moi na shilingi ya Moi! Sasa asiponipa shamba ndio kusema kwa nini alinizaa? Kwa nini kunileta duniani nami hilo sikuomba nifanyiwe – kisha kuja kunihini urithi wangu halali... kwa nini?

Sululu akili zinamduru. *Anavitambukia* vitoto vyake viwili vilivyojilaza sakafuni, vinafaidi *ubwabwa wa mama mtamu*. Anapapasa tena karibu na kizingiti cha mlango na kupata alichokuwa anakitafuta. Vyanda vyake vinakutana na upande wa mafutuni wa panga lililojipanga vizuri mithili ya mundu. Anafungua mlango taratibu na kujitosa nje huku hamaki zimesakama, anapumua na kupuma kama mkimbiaji wa mbio za nyika mwishoni mwa mashindano. Anaelekea kwenye nyumba ya babake.

Nyumba ya babake si nyumba ya kupigiwa mfano. Si jumba la fahari, si kasri lakini imeezekwa mabati, japo yameota kutu, ni mabati tu hata yakiwa na kutu. Ukutani kuna matofali ya kufyatuliwa na kuchomwa ingawa saruji haikutumiwa katika ujenzi. Katika hatua ya kupunguza gharama, Mwalimu Kauka, kama alivyojulikana hata baada ya kustaafu, aliamua kutumia udongo kushikamanisha tofali na jingine.

Sululu alipoitazama hiyo nyumba, aliingiwa na gere. Si nyumba ya msonge yenye kuta za mbavu za mbwa kama alimoishi yeye na aila yake changa.

Kama baba angenikatia shamba, ningeacha kuchapa mtindi, niache kulewalewa, kuvaa miwani kama wengine wasemavyo, nijikalifu kulima kilimo chenye tija nipate angalao mtaji wa kujenga nyumba ya maana. Ningelima miwa, mahindi, muhogo, mawele, mtama, nyanya, njugu, wimbi, ilmuradi mambo yangu yangetengenea. Ningefuga ng'ombe, farasi, mbuzi, kondoo, nguruwe na kuku.

Sululu alifika mlangoni kwa wazee wake na kubisha kwa hamaki.

"Fungua!"

"Nani?" Alijibu mama mtu.

"Nimesema fungua!" Aliwika Sululu.

Mlango ulifunguka muda mfupi baadaye na Sululu akauona uso wa mamake mzazi. Kwa kumwona mwanawe alivyolikamata panga na uso umepiga makunjo, mama mtu *aliachama*.

"Sululu kulikoni mwanangu?"

"Wapi baba?" Sululu aliuliza kwa ukali.

"Sululu!"

"Nasema wapi baba?"

"Kwani kuna nini?"

"Kama baba hawezi kusikia kwa maneno sasa atasikia kwa panga."

"Mwanangu siku hizi unatuvutia bangi?"

"Kasumba au bila kasumba mimi nataka shamba!" Alifoka Sululu. "Mnataka niseme mara ngapi? Nataka *kasma* yangu ya shamba."

"Sululu, umemshikia babako panga kwa ajili ya shamba?"

"Mbona hanipi fungu langu? Enh?"

"Na kwa sasa umejenga nyumba wapi?"

"Kwa shamba la baba."

"Nani kakupa ruhusa kujenga?"

"Yeye."

"Sululu, umekuwa punda unashukuru kwa mateke?"

"Sasa hivi viekari viwili anavyonipa nikajenga nyumba na ninakolima kila mwaka vinanitosha nini?"

"Basi wacha kupaza sauti kama mwehu mwanangu, babako unajua tena hali yake taabani."

"Hapana, nataka shamba, nataka ekari kumi na nipewe na *hatimiliki*."

"Shamba hili lina ekari ishirini tu, sasa nduguzo Ayubu, Toili na Matayo watapata nini? Ehe! Wao na familia zao?

"Sitaki kujua. Mimi ndiye mkubwa nastahiki fungu kubwa. Tena nipewe hatimiliki yenye jina langu. Iandikwe Sululu Kauka. Tena kwa herufi kubwa."

"Na isipokuwa hivyo?"

"Nitamwua mtu. Nitampasua huyu mzee tumbo lake kubwa kwa panga hili."

"Hebu sikiza Sululu," alisema mama kwa upole. "Sisi wazazi wako *tumejisabilia* kwako si haba. *Tumejikusuru* kukupeleka shule Teremi ukakataa kusoma mwenyewe. Karo tuliyolipa *ikaenda arijojo*. Wadogo zako walitumia vyema fursa zao shuleni, sasa wana makazi ya maana."

"Sasa *unanisimbulia*?"

"Nasema utundu wako umezidi, mtoto husaidiki."

"Nitamwua mtu."

"Basi kama upo tayari kuua, anza nami hapa mamako, niliyekubeba tumboni miezi tisa, nikakuosha, nikakunyonyesha, nikakuongoa, nikakuuguza, nikakupakata…"

"Acha *masimbulio*!" Alipaza tena sauti.

"Ee! Wajua babako mgonjwa, usimpigie kelele namna hiyo. Amekesha akiugua."

"Sasa anataka kufa kabla hajanipa shamba?"

"Sululu!"

"Mimi nitammaliza!"

"Kizingiti hiki hupiti mwanangu. Utaniua mimi kwanza kabla kumwua babako."

"Mama Sululu!" Sauti ya baba mtu ilisikika kutoka chumbani. "Mwachie, aje animalize kama hiyo ni azma yake. Mwachie aje."

Kimya kikajiri kitambo. Punde si punde Sululu aliona mlango unafunguka wazi na babake anapishwa na mama na kutoka nje. Baba alikabiliana mkabala na Sululu. Mzee uso umetulia ingawa anatembea kwa *kuchechea*.

"Sululu!" Alimwita mwanawe kwa uanana.

"Nipe kasma yangu ya shamba."

"Ndiyo sababu unataka kunikatakata kwa panga!"

Baba alimkaribia mwanawe na kumtazama kitambo.

"Basi nipo hapa nikate vipande vipande jinsi unavyotaka."

Kimya.

"Nasema nikate kama unavyotaka shamba hili likatwe!"

"Niue mimi, umwache mume wangu," mama alijaribu kuingilia kati.

"Sululu," baba alitoa kauli tena. "Hili shamba unalotaka kuniulia nimerithi kutoka kwa nani?"

"Sijui."

"Je, kanirithisha babu yako?"

Sululu alitikisa kichwa.

"Nimelinunua kwa jasho langu mwenyewe, kwa kipato kidogo cha ualimu. Kwa *kudunduliza*. Kwa kujihini. Kujinyima kila raha ili wanangu wawe na pahala pa kupaita pao."

"Ninataka pangu!"

"Hutaki penu?"

"Petu si pangu."

"Mbona usifuate nyayo zangu basi kama walivyofanya wadogo zako?"

"Sikuelewi."

"Kwa hiyo wataka kuniua tu bila kunielewa? Hivyo ndivyo hekima yako inavyokuongoza?"

Mwalimu Kauka akauingiza mkono kwenye mfuko wake wa koti. Hapo Sululu alishtuka na kurudi kinyumenyume.

"Ala! Baba unataka kunipiga risasi?" Alilalama Sululu.

Baba mtu alicheka tu.

"Tangu lini umeniona na bunduki Sululu mwanangu?"

Kisha baba akatoa bahasha na kumwambia Sululu asome stakabadhi zilizokuwa ndani. Mwanzoni Sululu alisita. Mama naye alikuwa amesimama pale anatazama sinema hiyo kwa zingatio. Hatimaye, Sululu alijipa ujasiri akamsogelea babake na kuichukua bahasha ile. Akaitoa barua ya kwanza. Ilikuwa hati ya kiapisho iliyotiwa saini na nduguze wadogo na hakimu pamoja na kupigwa muhuri rasmi wa mahakama. Sululu alisoma kwa ghibu mara mbili mbili:

*Sisi wafuatao, Toili Kauka, Ayubu Kauka na Matayo Kauka, tunathibitisha kwa saini zetu kwenye hati hii ya kiapisho mbele ya mahakama ya Chenjeni kwamba hatuna nia yoyote kudai kasma yetu kwenye ploti nambari 341 eneo la Chenjeni, shamba la baba yetu Albert Kauka. Kama baba akiona sawa anaweza kumpa ndugu yetu Sululu Kauka kasma zetu.*

Ujumbe unapomtua Sululu akilini, anaingiwa na kitetemeshi na kudondokwa na machozi. Alipoichomoa hatimiliki ya kasma yake na ya ndugu zake, hatimiliki yenye jina lake, katika herufi kubwa, macho yake yalikuwa hayaoni tena kwa gharika ya machozi. Pu! Panga lake likabwagika chini bila ya habari.

Siku hiyo watu wa Chenjeni walikuwa na kazi kubwa ya kumzuia Sululu kujitosa kwenye *uketo* wa mto Chenjeni alikotaka kujifia.

## Maswali ya ufahamu

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, someni tena hadithi fupi iitwayo '**Kasma Yangu**' mliyosoma hapo juu kisha mjibu maswali yafuatayo.*

1. Kwa nini Sululu hakuwa na ucheshi alipoamka siku hiyo?
2. Jadili ndoa ya Sululu na mkewe ilivyokuwa.
3. Eleza namna nyumba ya babake Sululu ilivyokuwa.
4. Jadili tabia za mhusika Sululu.

5. Kwa nini Sululu aliingilia tabia ya ulevi?
6. Jadili suala la urithi wa ardhi linavyoshughulikiwa katika hadithi hii. Linganisha suala hili na namna linavyoangaziwa katika jamii yenu.
7. Taja ndugu zake Sululu.
8. Eleza sifa za mamake Sululu.
9. Jadili maudhui mawili kutokana na hadithi fupi uliyosoma.
10. Eleza lengo la mwandishi wa hadithi uliyosoma hapo awali.

## 7.2 Msamiati kutokana na hadithi fupi husika

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tafuteni msamiati mpya katika hadithi fupi mliyosoma hapo awali kisha mweleze maana zao. Zingatieni muktadha wa hadithi hiyo. Mnaweza kutumia kamusi inapohitajika.*

**Kwa mfano:**

***akiforota*** – *akikoroma usingizini*

### Zoezi la 1

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, elezeni maana ya msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi zifuatazo kisha mtunge sentensi sahihi kwa kutumia msamiati huo.*

**Kwa mfano:** hatimiliki

**Matumizi katika sentensi:** Baba alimpa Sululu ***hatimiliki*** ya ardhi yake.

1. Moyo wangu uli*tweta* nilipomwona simba akinijia.
2. Mama alim*papasa* mtoto wake aliyekuwa analia.
3. Kamana alivaa *kaptura* yake mpya.
4. Watu wengi wanampenda Uwase kwa sababu ya *ucheshi* wake.
5. Upigaji kelele darasani ni *kero* kwa wanafunzi wengine.
6. Bidhaa hizi *zinazipiku* ulizonunua wiki iliyopita.
7. Mwalimu mkuu alishikwa na *hamaki* Neza alipomtusi.
8. Mabati ya paa la nyumba yetu yana *kutu*.
9. Nyumba yao ya *msonge* ilibomolewa.
10. Mama *aliachama* alipomwona mwanawe amebeba upanga.

## 7.3 Matumizi ya lugha: Aina mbalimbali za wahusika

*Katika makundi ya wanafunzi watano watano, jadilini:*

1. Aina mbalimbali za wahusika katika fasihi andishi.
2. Tabia na sifa za wahusika katika hadithi fupi mliyosoma hapo awali kama vile: Sululu, mamake Sululu, mke wa Sululu, babake Sululu n.k.

**Kwa mfano:**

Sululu ndiye mhusika mkuu katika hadithi hii. Matukio yote yanamhusu yeye. Wazazi wa Sululu pamoja na mke wake ni wahusika wadogo na wajenzi kwa sababu wanatumika kuzijenga tabia za Sululu.

### Zoezi la 2

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, jadilini tabia na sifa za rafiki yako.*

### Maelezo muhimu

Viumbe wa kisanaa ambao hutumiwa katika kazi ya fasihi kuupitisha ujumbe wa mwandishi huitwa ***wahusika***. Wahusika ndio msingi wa hadithi yoyote ile kwa sababu hadithi huwahusu wao. Wahusika wanaweza kuwa: binadamu, wanyama, mazimwi, vitu, sauti n.k.

Kuna aina mbalimbali za wahusika kama vile: *Wahusika wakuu, wadogo, nguli, bapa, kielelezo, bapa sugu* n.k.

## 7.4 Kusikiliza na kuzungumza: Tabia na sifa za wahusika

*Katika makundi ya wanafunzi watano watano, jadilini kuhusu aina mbalimbali za wahusika pamoja na tabia na sifa zao kwa kusoma riwaya moja teule, kwa mfano riwaya ya '**Siku Njema**' (iliyoandikwa na Ken Walibora). Kila kundi liwasilishe ufupisho wa majadiliano yao mbele ya wanafunzi wenzao.*

### Zoezi la 3

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, jadilini uhusiano wa mada au kichwa cha riwaya ya **SIKU NJEMA** na maudhui yaliyoangaziwa katika riwaya hiyo.*

## 7.5 Sarufi: Kauli ya kufanyiwa/kutendewa

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwenzako ajaribu kukufanyia au kukutendea kitendo fulani, kwa mfano: kubebewa vitabu vyako, kuchongewa penseli, kuinuliwa begi lako la vitabu, kupangusiwa kiti ili uketi n.k. Andika sentensi sahihi zinazoeleza vitendo alivyokufanyia mwenzako.*

**Kwa mfano:**

a) Mutoni *alibebewa* vitabu vyake.

b) Neza *alipangiwa* nguo na viatu vyake.

### Zoezi la makundi

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, geuzeni sentensi zifuatazo ziwe katika hali ya mtu kufanyiwa au kutendewa kitendo fulani.*

**Kwa mfano:** Bahati *anapika* chakula cha mama.

**Jibu:** Mama *anapikiwa* chakula na Bahati.

1. Baba anaandika barua ya mama.
2. Mimi nitafua nguo za babu na nyanya.
3. Gasimba amenunua vikombe vya wageni.
4. Mama atamtembelea shangazi yetu.
5. Dereva anasafisha gari la mwajiri.

*Je, mmegundua nini kutokana na mabadiliko hayo?*

### Zoezi la 4

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, chunguzeni mabadiliko katika vitenzi hivi kisha mjaze kwa usahihi nafasi zilizoachwa wazi katika jedwali hili.*

| **Hali ya kufanya** | **Hali ya kufanyiwa/kutendewa** |
|---|---|
| chonga | chongewa |
| chunga | ____________ |
| daka | dakiwa |
| ____________ | elezewa |
| fagia | fagiliwa |
| haribu | ____________ |
| inua | inuliwa |
| ____________ | kamatiwa |

### Maelezo muhimu

- Kauli inayoleta maana ya kitendo kufanywa kwa niaba ya nomino au kwa ajili ya nomino fulani huitwa ***kauli ya kutendewa/kufanyiwa***.
- Silabi za mwisho katika vitenzi vilivyo katika kauli ya kutendewa ni: ***-iwa, -ewa, -liwa*** na ***-lewa***.

**Mifano:**

1. Mama ali<u>pigiwa</u> makofi na wageni waalikwa.
2. Mwalimu ali<u>bebewa</u> vitabu hadi ofisi mwake.
3. Mjomba ali<u>tembelewa</u> na wageni wiki iliyopita.
4. Nyumba ime<u>fagiliwa</u> vizuri.

## Zoezi la makundi

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, jadilini kuhusu vitendo mbalimbali ambavyo tayari umeshavitenda. Tungeni sentensi sahihi kueleza namna ulivyotenda vitendo hivyo.*

**Kwa mfano:**

a) Nimefunga mlango uka<u>fungika</u>.
b) Chakula alichopika kime<u>pikika</u>.

## Zoezi la 5

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, andikeni sentensi hizi upya kwa kubadilisha vitenzi vilivyopigiwa mstari kuwa katika kauli ya kufanyika.*

**Kwa mfano:** Mkulima ana***<u>lima</u>*** shamba.

**Jibu:** Shamba lina***<u>limika</u>***.

1. Akimana <u>alichora</u> picha ya ndovu mkubwa.
2. Dada yangu mdogo <u>aliandika</u> barua ndefu.
3. Mimi <u>nitasoma</u> maandishi yaliyo ubaoni.
4. Sisi <u>tutacheza</u> mchezo mwingine.
5. Mwalimu <u>alifuta</u> ubao kwa kutumia kifutio kipya.

## Maelezo muhimu

- Kauli inayoleta maana ya kitendo kufanyika lakini mtendaji haonyeshwi au hajulikani huitwa kauli ya ***kutendeka/kufanyika.***
- Kauli ya kutendeka/kufanyika pia huleta maana ya kuwepo kwa uwezekano wa kufanyika kwa kitendo fulani.
- Silabi za mwisho kwenye vitenzi katika kauli ya kufanyika/kutendeka huwa: ***-ika, -lika, -eka, -leka.***

**Kwa mfano:**

1. Chakula alichotuletea kilikuwa kime***pikika***.
2. Nguo aliyonunuliwa jana ina***valika***.
3. Kitabu hiki kina***someka*** vizuri.
4. Miti waliyopanda katika shamba lao ina***ng'oka***.

## Zoezi la 6

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, kamilisheni jedwali hili kwa vitenzi vilivyo katika kauli ya kufanya/kutenda au kufanyika/kutendeka.*

| Hali ya kufanya/kutenda | Hali ya kufanyika/kutendeka |
|---|---|
| ________________ | chomeka |
| chunga | ________________ |
| ________________ | temeka |
| orodhesha | ________________ |
| ________________ | pigika |
| omba | ________________ |

## Zoezi la 7

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tungeni sentensi kumi sahihi katika kauli ya kufanyiwa/kutendewa na kauli ya kufanyika/kutendeka kwa kutumia vitenzi vifuatavyo.*

**Kwa mfano:** samehe

***Kauli ya kufanyiwa:*** Uwase alisamehewa dhambi zake.

***Kauli ya kufanyika:*** Dhambi zake zimesameheka.

1. safisha 2. kunywa 3. tibu 4. endesha 5. onja

# Somo la 8:  Maudhui na dhamira katika fasihi andishi

## 8.1 Shairi kuhusu ukulima

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tazameni michoro hii kisha msome shairi linalofuata kuhusu umuhimu wa jembe na baadaye mjibu maswali ya shairi.*







Jembe wangu nifariji, nami nikupe uzima,
Jembe wangu ndiwe taji, twakuenzi zote dhima,
Jembe wewe ni mpaji, wa baba na kina mama,
Jembe ndiwe mtawala, tangu enzi za wahenga.

Jembe wewe msifika, utuonee huruma,
Jembe shamba tukifyeka, njoo ufanye kulima,
Jembe njoo pasi shaka, ukija lete mtama,
Jembe ndiwe mtawala, tangu enzi za wahenga.

Jembe kwetu ukifika, tunapata usalama,
Jembe kote umeshika, ukweli tunausema,
Jembe yakija masika, nawe fika nyuma nyuma,
Jembe ndiwe mtawala, tangu enzi za wahenga.

Jembe jua likitoka, nawe usife mtima,
Jembe usije kuchoka, au kupatwa na homa,
Fanya bila kukongoka, fanya usirudi nyuma,
Jembe ndiwe mtawala, tangu enzi za wahenga.

Mola akupe hakika, usende kamwe mrama,
Nenda upate kufika, kama tunavyokutuma,
Sote huko tukifika, tutaishi kwa neema,
Jembe ndiwe mtawala, tangu enzi za wahenga.

## Maswali ya ufahamu

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, someni tena shairi kuhusu 'Jembe' kisha mjibu maswali yafuatayo.*

1. Shairi hili lina mishororo mingapi?
2. Onyesha vina vya kati na vina vya mwisho katika ubeti wa tatu wa shairi hili.
3. Eleza maana ya mishoro ifuatayo kama inavyojitokeza katika shairi hili:
   a) Jembe wewe ni mpaji, wa baba na mama
   b) Jembe shamba tukifyeka, njoo ufanye kulima
4. Jadili maana ya 'jembe' katika shairi hili.
5. Andika kibwagizo cha shairi hili na ueleze maana inayojitokeza katika kibwagizo chenyewe.
6. Onyesha mifano ya maneno yanayoashiria matumizi ya lugha yafuatayo katika shairi hili:
   a) Mazida
   b) Inkisari
7. Shairi hili lina mizani ngapi?
8. Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi hili.
   a) mtima
   b) kukongoka
   ch) mrama
   d) pasi
9. Eleza ujumbe unaojitokeza katika shairi hili.
10. Jadili ujumbe unaojitokeza katika ubeti wa kwanza wa shairi hili.

### Maelezo muhimu

- Kurefusha maneno katika shairi kwa kuyaongezea silabi ili kutosheleza idadi ya mizani inayotakikana huitwa ***mbinu ya mazida***.

  **Kwa mfano:** '*naifuatile*' (silabi sita) badala ya '*naifuata*' (silabi tano)

- Kupunguza idadi ya silabi katika maneno ya shairi ili kupata idadi ya mizani inayotakikana huitwa ***mbinu ya inkisari***.

  Kwa mfano: *'usende'* (silabi tatu) badala ya *'usiende'* (silabi nne)

## 8.2 Msamiati kutokana na shairi husika

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tafuteni msamiati mpya kutoka katika shairi mlilosoma hapo juu kisha mweleze maana yake na kuutungia msamiati huo sentensi sahihi kisarufi. Zingatieni muktadha wa shairi husika. Mnaweza kutumia kamusi inapohitajika.*

**Kwa mfano:**

***Wahenga***: mjuzi wa mambo ya kale mwenye kutegemewa kutoa ushauri.

***Matumizi katika sentensi:*** Wahenga wa kale walifahamu namna ya kutabiri mambo.

### Zoezi la 1

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, elezeni maana ya msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi zifuatazo kisha mtunge sentensi sahihi kwa kutumia msamiati huo kwa usahihi.*

**Kwa mfano:** fariji

**Matumizi katika sentensi:** Mama alim***fariji*** jirani yetu aliyefiwa.

1. Wakristo huamini kuwa Yesu Kristo aliwafia msalabani ili wapate ***uzima***.
2. Bibi harusi alivalia ***taji*** iliyopendeza.
3. Baadhi ya ***dhima*** za fasihi ni kuelimisha na kuburudisha.
4. Mungu ndiye ***mpaji*** wa uhai kwa viumbe hai.
5. Baba yangu ndiye ***mtawala*** wa mkoa wetu.
6. Baada ya mvua kunyesha ***tutafyeka*** shamba letu.
7. Sisi tumepanda ***mtama*** katika shamba letu.
8. Mvua ya ***masika*** inaponyesha huleta uharibifu mwingi.
9. Mwalimu wetu hajafika shuleni leo kwa sababu anaugua ***homa***.
10. Mambo yetu yameenda ***mrama***.

## 8.3 Matumizi ya lugha: Uhakiki wa maudhui na dhamira

*Katika makundi ya wanafunzi watano watano, jadilini:*

1. *Maudhui yaliyoangaziwa katika shairi mlilosoma.*
2. *Dhamira ya mtunzi wa shairi mlilosoma.*

**Kwa mfano:**

1. Shairi tulilosoma limeangazia maudhui ya ***maadili*** katika jamii.

   Kwa kufananishwa na jembe, binadamu wanafaa kuwa wenye bidii katika kazi zao kama lifanyavo jembe wakati wa ukulima.
2. ***Dhamira*** ya mtunzi wa shairi hili ni kuwahimiza binadamu kuwajibika katika kazi zao.

### Maelezo muhimu

1. Mawazo makuu au ujumbe unaojitokeza katika kazi ya fasihi huitwa ***maudhui***. Kwa mfano: *maudhui ya maadili katika jamii, umaskini, ufisadi, uongozi, elimu, siasa, udhalimu, mapenzi, ndoa, utamaduni, usasa, teknolojia, uhifadhi wa mazingira, kilimo na ufugaji* n.k.
2. Sababu, lengo au nia ya mwandishi kubuni kazi ya fasihi huitwa ***dhamira*** ya mwandishi. Dhamira ni kusudi na msukumo unaomfanya mwandishi kuandika kazi ya kifasihi. Kwa mfano: *mwandishi anaweza kudhamiria kuhimiza wanajamii kuhusiana na maadili katika jamii, wahifadhi mazingira, waelimike, wathamini utamaduni wao* n.k.

## 8.4 Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, jadilini kuhusu maudhui na dhamira kwa kurejelea mashairi ambayo mwalimu wenu atawapatia katika makundi yenu. Kila kundi liwasilishe ufupisho wa majadiliano yao mbele ya wanafunzi wenzao.*

### Zoezi la 2

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, karirini shairi mlilosoma hapo awali kuhusu 'jembe'. Mahadhi mbalimbali ya kukariri mashairi yanaweza kutumiwa.*

## 8.5 Sarufi: Kauli ya kufanyisha/kutendesha

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, jaribuni kumsaidia au kumlazimisha mwenzako atende kitendo fulani. Kwa mfano: kumsomesha, kumwimbisha, kumchezesha, kumnywesha n.k. Andika sentensi sahihi zinazoeleza vitendo unavyomsaidia au unavyomlazimisha mwenzako kuvitenda.*

**Kwa mfano:**

a) Mimi *nilimbebesha* Birasa vitabu vyangu.

b) Ngabo *alinipangisha* viti darasani.

*Je, mmegundua nini?*

### Zoezi la makundi

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, chunguzeni mabadiliko ya vitenzi hivi katika kauli ya kutenda na kauli ya kutendesha kisha mjaze nafasi zilizoachwa wazi kwa jibu sahihi.*

| **Kutenda/kufanya** | **Kutendesha/kufanyisha** |
|---|---|
| ______________ | limisha |
| (ku)la | lisha |
| pita | ______________ |
| ______________ | imbisha |
| cheza | ______________ |
| ______________ | chekesha |
| ______________ | itisha |
| andika | ______________ |
| ______________ | somesha |
| choka | chokesha/chosha |
| ______________ | ketisha |

### Zoezi la 3

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tungeni sentensi sahihi katika kauli ya kutendesha/kufanyisha.*

**Kwa mfano:** Shangazi anamchezesha mtoto uwanjani.

### Maelezo muhimu

Hali ya kumsaidia mtu au kumlazimisha mtu kutenda kitendo fulani ndiyo kauli ya ***kutendesha/kufanyisha***. Katika kauli hii, silabi za mwisho humalizika kwa: -***sha***, -***za***, -***sa***, -***fya*** na -***nya***.

**Kwa mfano:**

1. Mama ***alimlisha*** mtoto chakula.
2. Birasa ***alimtembeza*** nyanya uwanjani.
3. Kaka ***alinusa*** nguo aliyopewa.
4. Mungu ***alimponya*** baba yangu aliyekuwa akiugua.
5. Jitu lile ***liliwaogofya*** wanafunzi wakatoroka.

## Zoezi la makundi

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, jaribu kumfanyia mwenzako kitendo fulani naye mwenzako pia akufanyie kitendo hicho hicho. Kwa mfano: kusomeana hadithi, kuandikiana barua, kubebeana vitabu, kuinuana juu, kuimbiana wimbo n.k. Andika sentensi sahihi zinazoeleza vitendo ambavyo mnafanyiana.*

**Kwa mfano:**

a) Mimi na Mutoni ***tulisomeana*** hadithi za kusisimua.

b) Wanafunzi wale wawili ***waliinuana*** juu.

## Zoezi la 4

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, chunguzeni mabadiliko ya vitenzi hivi katika kauli ya kutenda na kauli ya kutendeana kisha mjaze nafasi zilizoachwa wazi kwa jibu sahihi.*

| **Kutenda/kufanya** | **Kutendeana/kufanyiana** |
|---|---|
| ______________ | rukiana |
| andika | ______________ |
| ______________ | pitiana |
| imba | ______________ |
| ______________ | sameheana |
| tembea | ______________ |
| ita | ______________ |
| ______________ | bebeana |
| pika | ______________ |
| ______________ | tembezana |
| lala | ______________ |

## Zoezi la 5

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tungeni sentensi tano sahihi katika kauli ya kutendeana/kufanyiana.*

**Kwa mfano:** Wakulima *walilimiana* mashamba yao.

## Maelezo muhimu

Kauli inayoleta maana kuwa wahusika wawili au zaidi wanatendeana kitendo kile kimoja huitwa ***kauli ya kutendeana/kufanyiana***. Silabi za mwisho kwenye vitenzi katika kauli hii huwa: ***-iana, -eana***.

**Kwa mfano:**

1. Wanafunzi ***wanasomeana*** hadithi za Kiswahili.
2. Kaka na dada ***waliandikiana*** barua wakiwa shuleni.
3. Wakulima ***walilimiana*** mashamba yao.

## Zoezi la 6

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tungeni sentensi tano sahihi katika kauli ya kufanyisha/kutendesha na sentensi tano sahihi katika kauli ya kufanyiana/kutendeana kwa kutumia vitenzi vifuatavyo.*

**Kwa mfano:** tembea

***Kauli ya kufanyisha:*** Mama *alimtembeza* mtoto mjini.


***Kauli ya kufanyiana:*** Mama na rafiki yake *walitembeleana*.


1. panda
2. kunywa
3. piga
4. ogopa
5. onja

# Somo la 9: Mandhari katika fasihi andishi

## 9.1 Sura moja ya tamthilia yenye mandhari mbalimbali

*Katika makundi ya wanafunzi watano watano, tazameni michoro hii kisha msome maonyesho mawili ya Tamthilia ya '**Kijiba cha Moyo**' (iliyoandikwa na Timothy Arege) na baadaye mjibu maswali ya ufahamu.*




### Onyesho la 4 (Mchoro A)

*(Siku hiyo hiyo. Magharibi. Nyumbani kwake Sele. Sele yuko peke yake. Kuna joto kali. Sele ameketi kochini huku akijipepea. Anaonekana mwenye mawazo lakini mtulivu.)*

**Bi. Rahma:** *(Kutoka nje.)* Hodi! Hodi hapa!

**Sele:** Karibu. Pita ndani. *(Bi.Rahma anaingia.)* Nilikuwa ninajiuliza nani huyu tena. Kumbe wewe bibi. Shikamoo!

**Bi. Rahma:** Marahaba mume wangu.

**Sele:** Haya karibu keti. *(Bi. Rahma anaketi.)*

**Bi. Rahma:** Habari za siku nyingi?

**Sele:** Nzuri bibi.

**Bi. Rahma:** Mimi nimepata salamu kuwa Sele mgonjwa.

Nikasema,"Mume wangu mgonjwa na mimi sina habari." Basi nikaona nije nikuone.

**Sele:** Vizuri umefika. Lakini hata sina ugonjwa. Mimi mzima.

**Bi. Rahma:** Mzima?

**Sele:** Mzima mimi. Mzima kama kigongo. Buheri wa afya kabisa.

**Bi. Rahma:** Lakini mamako umemtia wasiwasi. Mimi nimetoka nyumbani kwenu.

Hata mkeo naona hana utulivu. Kwa nini hivyo mume wangu?

**Sele:** Hata! Hamna kitu. Na wote nimeisha kuwaambia kuwa sina neno.

Hawataki kuniamini. Imani yao adimu.

**Bi. Rahma:** Mume wangu, sisi wazee tunaweza kukosa shabaha kwa jiwe lakini sio kwa maneno. Mtu mzima akilisema jambo, basi upo uhakika kuwa kaliona. Ndiyo maana wakasema kuwa ikiwa halipo, basi lipo njiani laja. *(Kimya.)* Sasa umewapa watu nafasi ya kuzua tetesi.

**Sele:** Watu? Watu gani?

**Bi. Rahma:** Wote waliokujua jana wakikuona leo hii.

**Sele:** Wanasema nini?

**Bi. Rahma:** Kuwa umebadilika. Kuwa wewe si yule wa jana. Kuwa wewe umekata tamaa kwa kufutwa kazi…

**Sele:** Bibi, mimi sikufutwa kazi. Wao wanasema wanayotaka kusikia na kuyaona. Mimi nilisimamishwa kazi kama wale wengine. Hata mama aliachishwa.

**Bi Rahma:** Kweli waliachishwa lakini hawakubadilika kama wewe. Na ndiyo maana watu hawawasemi.

**Sele:** Labda wananisema kwa sababu nilikuwa kinara wa walioachishwa kazi. Wao walikuwa wamezoea kuniona katika vyombo vya habari na kwa kuwa hawanioni tena wamekata kauli kuwa mimi mgonjwa. Hata nyinyi sasa mmeanza kuamini hivyo.

**Bi. Rahma:** Lakini baba, watu hawaishi katika kisiwa cha upweke unavyofanya wewe. Mtu pweke ni uvundo. Hata kama azma yenu ya kurudi kazini ilizimwa, haifai hivi unavyofanya wewe.

**Sele:** Sikiliza bibi, hivi ninavyokaa hapa nyumbani si kwamba nimekata tamaa. La hasha! Ninajaribu kutafakari kwa makini uhusiano baina yao na sisi. Na vilevile kudadisi sisi ni kina nani katika uhusiano huo. *(Kimya.)*

**Bi. Rahma:** Wao si tofauti na wewe. Ndugu zenu ndio waliowaachisha kazi na walivyofanya hivyo wana sababu. Sisi hatuwezi kuzifahamu.

**Sele:** Hata si wao waliotuachisha. Wanatuhitaji lakini wamepewa amri na ndugu zetu washirika kupitia mikopo yao. Si habari ya sisi kuchagua. Ni sisi tutii. Tutatii amri zao mpaka lini?

**Bi. Rahma:** Wahenga wanasema, mwenye nguvu mpishe!
Sasa utapigana nao? Usiloliweza unaliacha. Unafungua ukurasa mpya.

**Sele:** Ndio huu ukurasa mpya niliofungua. Kuuangalia upya udugu wetu.
Na baada ya kuuangalia kwa makini ninaanza kujichukia.

**Bi. Rahma:** Mtu hajichukii baba. Thamani ya mtu aijuaye ni mtu mwenyewe.
Ukijithamini wenzako nao watakuthamini. Ushaona?

## Onyesho la 5 (Mchoro B)

*(Siku inayofuata asubuhi. Hospitalini. Katika chumba cha Sele. Sele ameketi pembeni mwa kitanda chake. Anaingia Jamila na vifaa vya kupima ambavyo anaviweka mezani.)*

**Jamila:** *(Akiingia.)* Umelalaje Sele?

**Sele:** Vizuri.

**Jamila:** Vyema. *(Anamtazama huku akipanga vifaa vyake vya kazi.)*
Wala mbu hawakukusumbua?

**Sele:** Mimi sikuwasikia. Labda joto kidogo.

**Jamila:** Kweli siku hizi lipo joto kidogo. *(Akimkaribia.)*
Nitakupima halafu daktari atakuja kukuona.

**Sele:** Tena?

**Jamila:** Umeisha kupimwa leo?

**Sele:** Jamila, jana mmenipima. Hakuna lililobadilika. Najihisi vile vile tu.
Jana mmenipima na hata kunitoa damu.

**Jamila:** *(Anacheka.)* Sikujua Sele bado ndo yule yule wa *Mikanjuni Secondary*.
Mwoga kama zamani!

**Sele:** *(Akitabasamu.)* Wapi? Mimi sikuwa mwoga…

**Jamila:** Afadhali kunguru. Kila ukiwaona watu ulikuwa huwezi kuwatazama.
Kichwa kimeinama macho yanauchimbua mchanga.
*(Wote wanacheka.)*

**Sele:** Mrongo wewe. Unajua vizuri macho yalikuwa ya simba.

**Jamila:** Wapi! *(Wanacheka.)* Usiwe na dukuduku. Huwa tunahitaji damu kidogo tu. Kuna *tests* inatubidi kuzifanya.

**Sele:** Si mtaimaliza damu yangu?

**Jamila:** *(Akicheka.)* Damu haiishi. Tunachukua kidogo kwa ajili ya kupima ili kubaini tatizo hasa ila kwa sasa nitakupima joto tu.

**Sele:** *(Akimridhia.)* Haya nipime. *(Jamila anaanza kumpima. Anakitia* kipimajoto kwapani mwa Sele. Anamtilia kifaa cha kupima mpigo wa damu juu ya mkono. Baada ya muda…)

**Jamila:** Hali si mbaya.

**Sele:** Niliisha kuwaambia hilo ila hamkutaka kukubali.
Na damu mlipata ina nini?

**Jamila:** Ilikuwa ya kupima kama una lolote. Lakini daktari atasema nawe zaidi kuhusu matokeo ya uchunguzi.

**Sele:** Daktari?

**Jamila:** Ndiyo.

**Sele:** Matokeo yangu?

**Jamila:** Yako ndiyo.

**Sele:** Nikidhani uchunguzi huambatana na matokeo! Kwa nini niwe wa mwisho kupewa habari zinazonihusu. Tena kwa kuomba!

**Jamila:** Si hivyo. Ndiyo kanuni ya utabibu. Mimi namfanyia uchunguzi huu daktari mkuu naye ndiye atakufafanulia yote…

## Maswali ya ufahamu

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, someni tena maonyesho mawili ya tamthilia mliyosoma hapo awali kisha mjibu maswali yafuatayo.*

1. Eleza mahali onyesho la 4 linakofanyikia.
2. Jadili hali ya Sele onyesho la 4 linapoanza.
3. Eleza sababu za Bi Rahma kwenda kumtembela Sele.
4. Ni tetesi gani alizokuwa amezisikia Bi Rahma kumhusu Sele?
5. Kwa nini Sele anaonekana kukata tamaa?
6. Onyesho la 5 linafanyikia wapi?
7. Jadili umuhimu wa mgonjwa kutolewa damu na daktari.
8. Eleza uhusiano uliopo kati ya Sele na Jamila.
9. Daktari huwapima wagonjwa kwa kutumia kifaa kipi?
10. Jadili maudhui yanayojitokeza katika maonyesho mawili ya tamthilia mliyoyasoma hapo awali.

## 9.2 Msamiati kutokana na maonyesho ya tamthilia husika

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tafuteni msamiati mpya kutoka katika maonyesho mawili ya tamthilia mliyosoma hapo awali kisha mweleze maana zao na kutunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno hayo. Zingatieni muktadha wa maonyesho husika. Mnaweza kutumia kamusi inapohitajika.*

**Kwa mfano:**

***Kipimajoto:*** kifaa ambacho hutumiwa na daktari kupima joto la mwili wa binadamu

***Matumizi katika sentensi:*** Jamila alitumia ***kipimajoto*** kupima joto la Sele.

### Zoezi la 1

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, elezeni maana ya msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi zifuatazo kisha mtunge sentensi sahihi kwa kutumia msamiati huo kwa usahihi.*

**Kwa mfano:** Dada yangu anasomea kozi ya utabibu katika chuo kikuu.

**Maana:** ***utabibu*** - uhodari wa kazi ya kutibu magonjwa hospitalini

**Sentensi:** Kanuni ya ***utabibu*** ni kuwa mgonjwa hupimwa kwanza ili kutibiwa.

1. Baba ameketi ***kochini*** akisoma gazeti.
2. Mwalimu wetu wa Kiswahili ni ***mtulivu*** sana.
3. Nimesikia ***tetesi*** kuwa mume wako ni mlevi.
4. Baba ***alikataa tamaa*** baada ya kufutwa kazi.
5. Akimana ***aliachishwa kazi*** baada ya kuiba pesa.
6. Sijawahi kumwona ***kunguru*** mkubwa kama huyu.
7. Mama ameketi jikoni ***akitafakari*** kuhusu ugonjwa wa Sele.
8. Bi harusi ameketi ***akijipepea***.
9. Hapa pana ***uvundo*** wa takataka na vitu vilivyooza.
10. ***Nawathamini*** sana wazazi wangu.

## 9.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano kuhusu mandhari

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, jadilini mandhari mbalimbali ambako maonyesho ya tamthilia yoyote ile yanaweza kutendekea. Mnaweza kurejelea tamthilia zozote ambazo mumewahi kuzisoma. Kila kikundi kiwasilishe majadiliano yao mbele ya wanafunzi wenzao.*

### Maelezo muhimu

- Wakati, hali au mahali ambapo tukio linaelezewa kutokea katika fasihi huitwa ***mandhari***.
- Mandhari yanaweza kuwa ya kihalisia (kweli) kama vile: *mtoni, hospitalini, nyumbani, shambani, barabarani* n.k.
- Mandhari pia yanaweza kuwa ya kidhahania (ya kufikiria tu) kama vile: *hewani, angani, kuzimu, kwenye jua* n.k.

## 9.4 Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, jadilini mandhari mbalimbali yanayojitokeza katika tamthilia ya* ***Urunana****.*
*Kila kundi liwasilishe ufupisho wa majadiliano yao mbele ya wanafunzi wenzao.*

## 9.5 Sarufi: Kauli ya kufanywa/kutendwa

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, jaribu kutenda kitendo fulani kisha mwenzako ataeleza mtendaji wa kitendo hicho. Kwa mfano: vitabu* ***kubebwa*** *na Kalisa, madawati* ***kupangwa*** *na Birasa, mlango* ***kufungwa*** *na Mutoni, ubao* ***kufutwa*** *na mwalimu n.k. Andika sentensi sahihi zinazoeleza watendaji wa vitendo alivyofanya mwenzako.*

**Kwa mfano:** a) Madarasa *yalisafishwa* na wanafunzi.

b) Insha *ziliandikwa* na wanafunzi.

*Je, mmegundua nini?*

### Zoezi la makundi

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, chunguzeni mabadiliko ya vitenzi hivi katika kauli ya kutenda/kufanya na kauli ya kutendwa/kufanywa kisha mjaze nafasi zilizoachwa wazi kwa jibu sahihi.*

| Kutenda/kufanya | Kutendwa/kufanywa |
|---|---|
| 1. ____________ | pandwa |
| 2. ____________ | lishwa |
| 3. ruka | ____________ |
| 4. ____________ | vunjwa |
| 5. soma | ____________ |

| | |
|---|---|
| 6. ______________ | chekwa |
| 7. ______________ | itwa |
| 8. piga | ______________ |
| 9. ______________ | bebwa |
| 10. chora | ______________ |

## Zoezi la 2

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tungeni sentensi sahihi katika kauli ya kutendwa/kufanywa.*

**Kwa mfano:** Mpira una*chezwa* uwanjani.

## Maelezo muhimu

Hali ya kutufahamisha kuhusu mtendaji wa kitendo fulani huitwa kauli ya ***kufanywa/kutendwa***. Mara nyingi katika kauli hii, silabi za mwisho humalizika kwa: -***wa***.

**Kwa mfano:**

a) Chakula kime*pikwa* na mama.
b) Mtoto ali*tembezwa* na Birasa.
ch) Viatu vili*nuswa* na baba kabla ya kuvivaa.
d) Mgonjwa aliponywa kwa dawa alizopewa.
e) Jitu lile linao*gopwa* na kila mtu.

## Zoezi la 3

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tungeni sentensi tano sahihi katika kauli ya kufanywa/kutendwa kwa kutumia vitenzi vifuatavyo.*

**Kwa mfano:** lima

***Kauli ya kufanywa:*** Shamba li***limwa*** na wafanyakazi wake.

1. panda
2. pita
3. omba
4. choma
5. vuta

## Zoezi la 4

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, jazeni nafasi zilizo wazi kwa kutumia kitenzi sahihi kutoka kwenye mabano katika hali ya kutendwa/ kufanywa.*

**Kwa mfano:** onya

**Sentensi:** Kaka ali***onywa*** dhidi ya kutembea usiku.

1. Gari lili__________ vibaya na dereva yule. (*endesha*)
2. Nyama ili__________ vipande vidogovidogo. (*kata*)
3. Kwa nini sebule yenu ime__________ hivi? (*panga*)
4. Barua ya kuomba msamaha ili________ na mwanafunzi. (*andika*)
5. Mungu hu_______ na binadamu wote. (*omba*)

# Somo la 10: Uhakiki wa mbinu za lugha katika fasihi

## 10.1 Sura moja ya riwaya yenye mbinu za lugha

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tazameni mchoro huu kisha msome sura moja ya Riwaya ya* ***'Utengano'*** *(iliyoandikwa na Said A. Mohamed) inayofuata na baadaye mjibu maswali ya ufahamu.*



Maimuna anakumbuka siku ile alipoamka asubuhi. Alijihisi mwepesi baada ya machofu ya pilkapilka za usiku uliopita. Akijua kuwa kishatoka kwenye ujahili wa babake na kuingia kwenye imani ya mtu asiyemjua ndewe wala sikio. Aliona yuko katika hifadhi na usalama. Kweli ulimwengu haukosi uovu, ila haukosi wema pia. Mwenyeji wake Bi Farashuu alimwendea taratibu akamwambia: 'Nimewaza na kufikiri sana. Sikulala. Hatimaye nimeona leo nikusafirishe. Hii leo kabla ya kesho. Nikupeleke Pumziko. Huko utayapenda maisha yake, maana Pumziko ni jiji. Maisha yake matamu. Pia nakukimbiza mikononi mwa babako; na hilo ndilo kubwa.'

'Mama, lakini ...'

'Hapana cha lakini... hii ni kwa usalama wako na wangu, na zaidi, huko utanafasika. Utafanya unavyotaka.'

'Haya...' alikubali Maimuna.

Jioni, Maimuna na Farashuu waliingia kwenye basi na baada ya safari ya siku mbili walifika kwa Mama Jeni. Walipofika tu, Farashuu na Mama Jeni walikwenda chemba. Walipotoka kunong'ona Farashuu hakuwa na mkao.

'Mimi nitarejea nyumbani kwa lile basi lililotuleta. Wewe utakaa hapa na bibi huyu. Usiogope wala usiwe na wasiwasi. Ukiwa umo mikononi mwake, ndio umo mikononi mwangu. Na hapa pana ndugu zako kama wewe. Tutaonana baadaye nitakapokuja kukuchukua. Najua utapapenda hapa. Kwaheri.'

Hata na yeye Maimuna alidhani atapapenda pahala hapo, hasa ule uzuri wa jiji na starehe alizohadithiwa na Bi Farashuu. Angalipenda kuutumia vilivyo uhuru alioupata. Afanye kazi ya maana. Atembee, aone mambo mbalimbali. Lakini leo alilazimishwa kupenda mambo ambayo asingalipenda kuyasikia, sikwambii kuyafanya. Hila nyingi zilifanywa na Mama Jeni kumtia yeye katika shengesha. Lakini Maimuna alikataa. Ndipo leo Mama Jeni alipomfungia ndani Maimuna na Bwana huyu mlevi. Napo Maimuna alifuzu kujitetea.

Kule chumbani Maimuna alijitupa kwenye kitanda cha mbao. Aliuzamisha uso wake kwenye mto akaunywesha machozi. Alilia chini kwa chini, kwa muda mrefu, halafu aligutuka ghafla alipohisi mkono ukimtambalia mgongoni.

'Unalia nini *darlin?'* Alikuwa Mama Jeni ambaye aliingia humo kwa kunyatia bila ya Maimuna kujua. 'Hupapendi hapa? Hukufurahi na yule bwana? Hukumpenda?. . . Nini basi?'

Maimuna hakujibu neno. Alivuta kwikwi za kilio. Kwa hakika hakuwa na jibu la suala hilo, maana amelijibu mara nyingi, lakini bibi mtu mzima huyu kaganda. Moyoni mwake alikuwa na hakika moja tu— huo haukuwa uhuru alioutaka. Pengine alijuta. Lakini….a-a, hakujuta. Hiyo ilikuwa afadhali kwake kuliko kurejea kwao.

'Inuka,' Mama Jeni alimvuta mkono Maimuna, 'shika pesa hizi, shilingi mia tatu na hamsini. Twende dukani ukanunue nguo na viatu, na vitu vingine unavyotaka. Na kama hizi hazikutoshi tutafanya mashauri mazuri. Haya inuka 'ma.'

'Pesa? Za nini?' Maimuna aliemewa akilini.

'Ukanunue nguo na vitu unavyotaka,' aliisikia sauti ya Mama Jeni ikimwambia kwa mbali.

Ulipita muda. Hatimaye alikata shauri kuinuka. Akamtazama Mama Jeni. Yule yule, hakubadilika — pandikizi la nyama lisilotambulikana kiuno, kifua wala shingo; alikuwa na nywele changa, macho manene, pua tapanyiko, midomo mikubwa na kidevu kisichobaguka na manyama ya uso uliotutumka. Alikuwa kakaa ubavuni pake, kavaa kaniki nyeusi iliyogeuka kijivujivu ambayo alikuwa kajifunga nayo kifuani. Mkononi katia usinga.

'Twende *darlin,*' alizidi kubembeleza Mama Jeni.

Maimuna alisalimu amri hatimaye. Na baada ya Mama Jeni kwenda kuvalia alikuwa tayari kumchukua Maimuna madukani. Kutoka chumbani, walipita kwenye ujia unaogawa vyumba vya huku na huku mle ndani. Kutoka ukumbini alichomoza mwanamke mmoja aliyekuwa akimwongoza mwanamume. Mwanamke huyu mwembamba alikuwa kavaa skati na blauzi ya manjano iliyoandikwa TOYOTA. Shingoni mkufu wa shaba ulimning'inia. Walipopishana, huyu mwanamke alichekacheka, akamwamkia Mama Jeni.

'Shikamoo.'

'Marahaba *darlin,*' aliitikia Mama Jeni kwa shangwe.

'Ah, lini shoga utachangamka?' alimtazama Maimuna.

Maimuna hakujibu kitu. Alimtazama kwa mshangao huyo mwanamke akielekea chumbani na nyuma yake akifuatwa na bwana mmoja mwenye hashuo. Hatimaye yule mwanamke alijichoma chumbani na bwanake akafuatia huku akiufunga mlango kwa nguvu. Halafu Maimuna na Mama Jeni walimsikia huyo mwanamke akikaripia kwa kelele.

'Usinivunjie mlango ukanilaza nje, una nini?'

Mama Jeni alitikisa kichwa, 'Ah, kila siku namwambia Dora, aache rafu, lakini wapi. Yeye mwenyewe, na watu wake wanaokuja wote wana fujo. Kazi yao rafu.'

Maimuna hakujali kitu. Hakuacha kusonya ndani kwa ndani kwa ule mtazamo aliotazamwa na yule bwana aliyeingia ndani na Dora.

'Ni hatari tupu siku hizi, tunasakwa kila upande, basi hizi kelele zitatuchongea wenyewe.'

Maimuna hakufahamu chochote Mama Jeni aliposema 'tunasakwa.'

Teksi iliwachukua kutoka nyumbani kwa Mama Jeni mpaka Toweni striti ya biashara, maduka huku na huku, katikati barabara. Maduka yenyewe yameandamana meli unusu, na takriban yote yanaendeshwa na Wahindi.

Maimuna alipokwisha teremka gari, alipata nafasi ya kuona mengi katika mji huo mkubwa. Kote kuliwepo majumba makubwa makubwa ya kisasa.

'Majumba makubwa enn, he!' Maimuna alishangaa, huku akifuata hatua za mchapuko za Mama Jeni.

'Ndiyo *darlin,* huu ni mtawalia wa majumba makubwa, Mashariki na Magharibi, Kaskazini na Kusini. Mashihofu! Ndiyo pumbaziko hii, na vichochoro huku. Hakuna karo zenye kububuja maji ovyo. Mtu anayetaka kuishi Toweni sharti ajue kuyauma meno maisha ndio aweze kupumzika. Tazama, teksi ile tuliyopanda, toka nyumbani mpaka hapa, mwendo wa robo saa kama hivi, ni shilingi arubaini. Na zaidi utaona ughali wa vitu huku madukani. Maskini tumo taabuni.' Sauti ya Mama Jeni ilikuwa ile ile. Imezoea kukokotwa, kulegezwa na kubiruliwa kwa madaha na mizungu ya kike.

Mpaka sasa, kwa Maimuna pesa haikuwa na maana kama aijuavyo Mama Jeni. Ughali na urahisi wa vitu au ulaini na ugumu wa maisha ulikuwa vitu vya mawazo vinavyotajwa kwa mdomo na kusahauliwa. Maisha bado yalikuwa mapya kwake na yeye alikuwa mpya wa maisha. Msitu mpya na komba wapya. Angalikuwa mkukuu, angalielewa uzuri Pumziko.

Pumziko, pumziko kweli. Kwa wale walioweza kuzidhibiti mbinu za maisha, wale waliokuwa mahodari kunyang'anya, ama kwa siri au kwa dhahiri, Pumziko kwao palikuwa pahala pa pumziko kweli. Licha ya ukubwa wake ambao ungalikadiriwa na jiji lolote la kisasa, lina uzuri wa sifa na mastakimu ya kustarehea. Vilabu vya usiku, na nyumba za siri zimejaa na ingawa serikali na magazeti hupiga kelele dhidi yazo, biashara hiyo inaendeshwa chini kwa chini. Tena kuna sinema, mbali na *drive ins'* mbali na mahoteli makubwa, majumba ya kukodi ya kulala na kula.

Mandhari ya Pumziko daima ni ghasia, mbio, pupa na zogo. Mchana na usiku maskini walipiga mbio kutafuta kuutengeneza ulimwengu wao, nao haukutengenea.

## Maswali ya ufahamu

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, someni tena sura moja ya riwaya mliyosoma hapo juu kisha mjibu maswali yafuatayo.*

1. Taja wahusika katika hadithi hii.
2. Jadili maudhui mawili yaliyoangaziwa katika hadithi hii.
3. Je, unadhani dhamira ya mwandishi wa hadithi hii ilikuwa ipi?
4. Taja semi moja iliyotumika katika hadithi hii.
5. Jadili mambo yaliyomshangaza Maimuna mjini Pumziko.
6. Eleza maisha ya mjini Pumziko yalivyokuwa.
7. Kwa kutoa mfano, eleza namna mbinu ya majazi imetumika katika hadithi hii.
8. Taja tanakali za sauti zilizotumika katika hadithi hii.
9. Unadhani kwa nini Maimuna alitoroka kutoka kwao na kuja Pumziko?
10. Jadili kwa kutoa mifano, namna mwandishi wa hadithi hii alivyotumia mbinu ya utohozi wa maneno fulani.

## 10.2 Msamiati kutokana na sura ya riwaya husika

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tafuteni msamiati mpya kutoka katika sehemu ya riwaya ya '**Utengano**' mliyosoma hapo awali kisha mweleze maana zao na kutunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno hayo. Zingatieni muktadha wa kifungu husika. Mnaweza kutumia kamusi inapohitajika.*

**Kwa mfano:**

***pilkapilka:*** hali ya mtu kuwa na shughuli nyingi kuliko kawaida

***Matumizi katika sentensi:*** Mama alikuwa na ***pilkapilka*** nyingi wageni walipofika.

## Zoezi la 1

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, elezeni maana ya msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi zifuatazo kisha mtunge sentensi sahihi kwa kutumia msamiati huo kwa usahihi.*

**Kwa mfano:** Dada yangu amevaa <u>blauzi</u> mpya.

**Maana:** ***blauzi*** – vazi la kike mfano wa shati

**Sentensi:** Nitamnunulia mama yangu ***blauzi*** nyingine.

1. Mtoto <u>*alipohisi*</u> usingizi alilala.
2. Mbwa <u>*alimnyatia*</u> paka na kumkamata.
3. Dora <u>*alimkaripia*</u> rafiki yake.
4. Birasa hapendi tabia ya <u>*kubiruliwa*</u> midomo na wasichana.
5. Sisi <u>*tunasakwa*</u> na polisi kwa kuchuuza bidhaa mjini.
6. Wezi walizua <u>*zogo*</u> katika benki moja kule mjini.
7. Mwili wa Mama Jeni <u>*uliotutumka*</u> umepakwa mafuta.
8. Baba na mama <u>*wananong'ona*</u> kule sebuleni.
9. <u>N*dewe*</u> ya sikio langu imepata jeraha.
10. <u>*Teksi*</u> iliyombeba Maimuna imepata ajali.

## 10.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano kuhusu mbinu za lugha

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadilini mbinu mbalimbali za lugha ambazo zimetumika katika sehemu ya riwaya ya '**Utengano**' mliyoisoma hapo awali. Kwa kutoa mifano, elezaneni:*

1. Matumizi ya tanakali za sauti
2. Matumizi ya semi
3. Matumizi ya mbinu ya majazi
4. Matumizi ya mbinu ya kuchanganya ndimi
5. Matumizi ya mbinu ya uhaishaji

**Kwa mfano:**

1. Matumizi ya tanakali za sauti, mfano: *kwikwi za kilio*
2. Matumizi ya semi, mfano: *pandikizi la nyama*
3. Matumizi ya mbinu ya majazi: *jina la mji wa Pumziko kuliko na starehe*
4. Matumizi ya mbinu ya kuchanganya ndimi, mfano: *Unalia nini **darlin**?*
5. Matumizi ya mbinu ya uhaishaji, mfano: *Maimuna aliuzamisha uso wake kwenye mto **akaunywesha** machozi.*

**Maelezo muhimu**

Matumizi ya lugha kwa njia ya kipekee katika fasihi ndiyo fani au mbinu za lugha. Mbinu za lugha ni kama vile:

1. Matumizi ya methali
2. Matumizi ya tashbihi
3. Matumizi ya majazi
4. Matumizi ya mbinu rejeshi
5. Matumizi ya semi, istiara, tanakali za sauti n.k.
6. Matumizi ya jazanda, uhaishaji, utohozi, kuchanganya ndimi n.k.

## 10.4 Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano ya mbinu za lugha

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, jadilini matumizi ya mbinu mbalimbali za lugha (fani) yanayojitokeza katika riwaya ya '**Siku Njema'**. Kila kundi liwasilishe ufupisho wa majadiliano yao mbele ya wanafunzi wenzao.*

### 10.4.1 Uhakiki wa waandishi mashuhuri wa fasihi ya Kiswahili

*Katika makundi ya wanafunzi watano watano, jadilini kuhusu waandishi mashuhuri wa fasihi ya Kiswahili ambao mnawafahamu na mwelezane namna kazi zao za fasihi zinavyohusiana na maisha na matarajio ya Wanyarwanda.*

**Maelezo muhimu**

Mwandishi wa kazi za kifasihi huwa ni mtu mwenye ubunifu wa kiwango cha juu sana. Yeye hubuni visa kwa kurejelea maisha ya wanajamii wake pamoja na matarajio yao. Baadhi ya waandishi mashuhuri wanaofahamika kupitia kwa kazi zao za kifasihi ni kama vile: Said A. Mohamed (Tanzania), Ken Walibora (Kenya) miongoni mwa wengine kutoka maeneo mbalimbali.

Waandishi hawa wamezungumzia masuala ya ushirikiano wa wanajamii pamoja na maadili mema katika jamii na taifa kwa jumla. Waandishi wengi kutoka nchini Rwanda wameandika kazi zao kwa lugha ya kifaransa kama vile Maggy Correa, Marie Umutesi, Yolanda Mukagasana miongoni mwa wengine. Baadhi ya kazi zao zinatafsiriwa kwa Kiswahili.

## 10.5 Sarufi: Kauli ya kufanyua/kutendua

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, jaribuni kutenda kitendo fulani kisha mwenzako afanye kinyume cha kitendo ulichofanya. Kwa mfano: ku**panga** vitabu kisha mwenzako akavi**pangua** vitabu hivyo, kuvi**tia** vitabu kwenye mkoba kisha mwenzako akavi**toa** vitabu hivyo kwenye mkoba huo huo n.k. Andika sentensi sahihi zinazoeleza vitendo unavyofanya na ambavyo mwenzako anafanya kinyume yavyo.*

**Kwa mfano:**

a) Mimi nili***panga*** vitabu kwenye kabati kisha Uwase akavi***pangua***.

b) Nilivi***tia*** vitabu kwenye mkoba kisha nikavi***toa*** jioni.

*Je, mmegundua nini?*

### Zoezi la makundi

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, chunguzeni mabadiliko ya vitenzi hivi katika kauli ya kutenda na kauli ya kutendua kisha mjaze nafasi zilizoachwa wazi kwa jibu sahihi.*

| Kutenda/kufanya | Kutendua/kufanyua |
|---|---|
| fuma | fumua |
| choma | ______________ |
| ______________ | fungua |
| shona | ______________ |
| ______________ | tegua |
| bandika | ______________ |
| ______________ | toa |
| waza | ______________ |
| ______________ | pakua |
| anika | ______________ |
| chimba | ______________ |
| ______________ | fumbua |

### Zoezi la 2

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tungeni sentensi tano sahihi katika kauli ya kutendua.*

**Kwa mfano:** Shangazi ame<u>fumua</u> kitambaa alichokuwa ame<u>fuma</u>.

### Maelezo muhimu

Hali ya kuonyesha kinyume cha kitendo huwa ni kauli ya ***kutendua***. Katika kauli hii, silabi za mwisho humalizika kwa: ***-ua***, na ***-oa*** .

**Kwa mfano:**

1. Dereva ali***pakua*** mizigo iliyokuwa imepakiwa kwenye gari lake.
2. Shangazi ali***anua*** nguo zilizokuwa zimeanikwa nyuma ya nyumba yetu.

## Zoezi la 3

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tungeni sentensi tano sahihi katika kauli ya kutendua kwa kutumia vitenzi vifuatavyo.*

**Kwa mfano:** shona

***Kauli ya kutendua:*** Fundi wa nguo ali*shonoa* nguo aliyokuwa ame*shona*.

1. pakia
2. kunja
3. anika
4. funika
5. funga

## Zoezi la 4

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, elezeni maana inayojitokeza katika sentensi hizi:*

a) Fundi wa nguo anafumua fulana ya mteja wake.

b) Neza alipangua viti vyote sebuleni.

ch) Nyanya alifumbua mafumbo yote tuliyomuuliza.

d) Siwezi kuipakua mizigo hii kutoka garini kwani ni mizito sana.

## Tathmini ya mada ya 2

### Zoezi la 1

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jibuni maswali yafuatayo ya utanzu wa ushairi.*

1. Eleza maana ya shairi.
2. Muundo katika shairi huhusisha nini?
3. Eleza maana ya:
   a) Mishororo
   b) Mizani
   ch) Vina
   d) Kibwagizo

### Zoezi la 2

*Kamilisha jedwali lifuatalo kwa vitenzi sahihi katika hali ya kufanyika/kutendeka.*

| **Kutendea** | **Kutendeka** |
|---|---|
| kimbilia | ____________ |
| chomea | ____________ |
| lia (chakula) | ____________ |
| pandia | ____________ |
| kalia | ____________ |

### Zoezi la 3

*Kamilisha jedwali hili kwa usahihi kulingana na kauli za vitenzi husika.*

| **Kutendea** | **Kutendeka** | **Kutendewa** | **Kutendua** |
|---|---|---|---|
| pakia | ________ | pakiwa | ________ |
| ________ | chomeka | ________ | chomoa |
| tendea | ________ | ________ | ________ |
| fyatia | ________ | ________ | ________ |
| chimba | ________ | ________ | ________ |

## Zoezi la 4

*Jibu kwa usahihi maswali yafuatayo kuhusu utanzu wa tamthilia.*

1. Eleza maana ya tamthilia.
2. Taja sifa zozote bainifu za utanzu wa tamthilia.
3. Jadili tofauti zozote tano baina ya utanzu wa riwaya na tamthilia.

## Zoezi la 5

*Jibu kwa usahihi maswali yafuatayo kuhusu utanzu wa riwaya.*

1. Eleza maana ya riwaya.
2. Jadili sifa tano bainifu za utanzu wa riwaya.
3. Eleza umuhimu wa wahusika katika riwaya.

## Zoezi la 6

*Jibu kwa usahihi maswali yafuatayo kuhusu utanzu wa hadithi fupi.*

1. Eleza maana ya hadithi fupi.
2. Jadili sifa tano bainifu za utanzu wa hadithi fupi.
3. Eleza tofauti zilizopo kati ya riwaya na hadithi fupi.

## Zoezi la 7

*Jadili tofauti zilizopo kati ya fasihi andishi na fasihi simulizi.*

## Faharasa

**sanaa:** ufundi wa kuwasilisha hisia na mawazo ya binadamu kwa maandishi, michoro au uchongaji

**maudhui:** jumla ya masuala yanayozungumziwa katika kazi ya fasihi

**fasihi:** sanaa ya lugha inayoelezea tajriba ya maisha ya binadamu

**utanzu:** tawi la fasihi

**wahakiki:** wachanganuzi wa kazi ya fasihi

**mandhari:** mahali pa tukio katika kazi ya kifasihi

**upeo:** kilele cha masimulizi kabla ya mporomoko

**wahusika:** viumbe wanaotumika kuwasilisha maudhui katika kazi ya fasihi

**kinathari:** ya mfululizo

**kubuni:** kufanya wazo ambalo halikuwepo kuwepo

**msuko:** namna vitendo katika kazi ya fasihi vinavyofuatana; ploti

**fani:** hurejelea matumizi ya tamathali mbalimbali za lugha. Kwa mfano: methali, majazi, takriri n.k.

**ubeti/beti:** kifungu chenye idadi fulani ya mishororo

**vina:** silabi za mwisho katika vipande vya mshororo

**mshororo:** mistari katika ubeti wa shairi

**mizani:** silabi zinazotamkika kwa mpigo mmoja (kama sauti moja) katika shairi

**kibwagizo:** mshororo unaorudiwarudiwa katika shairi zima

**tamthilia:** mchezo wa kuigiza unaoweza kusomwa au kutazamwa na kusikilizwa

**jukwaani:** mahali ambapo waigizaji huigizia michezo yao. Inaweza kuwa ukumbini ama mahali pengine

**waigizaji:** wachezaji ama washiriki katika tamthilia wakati wa maonyesho katika jukwaa. Huwa siyo wahusika wa ndani ya tamthilia

**hadhira:** viumbe wanaotazama mchezo kwenye jukwaa ama wasomaji. Pia wanaweza kuwa wahusika ndani ya tamthilia hai

**ndewe:** sehemu ya chini ya sikio

**hashuo:** hali ya kujionyesha au kujishaua mbele ya watu

**mastakimu:** mahali anapoishi mtu; nyumbani

**zogo:** hali ya ukosefu wa utulivu; ghasia, fujo


# SURA YA TATU

**MADA KUU 3:** UBUNAJI
**MADA NDOGO:** Hotuba na ufupisho

## Somo la 11: Sehemu kuu za hotuba

### 11.1 Hotuba kuhusu usafi

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tazameni michoro hii kisha msome kifungu cha hotuba kinachofuata kuhusu usafi na baadaye mjibu maswali ya ufahamu.*




Mkuu wa Mkoa wa Kusini, wageni wote waalikwa, wazazi, walimu na wanafunzi, hamjambo? Natumai mko salama na buheri wa afya. Namshukuru Mola kwa kutupa uhai na afya njema. Jina langu ni Bwana John Gatete. Mimi ni Afisa wa Afya katika Mkoa wa Kusini. Namshukuru Mkuu wa Mkoa wetu Bwana William Ntawiyanga kwa nafasi hii aliyonipa ili kuja kuzungumza nanyi. Ningependa kuzungumza kwa ufupi kuhusiana na usafi kwa ujumla.

Kwanza, usafi ni hali ya kuwa nadhifu. Ni muhimu kwa binadamu wote kufahamu umuhimu wa usafi ili kuepuka kupatwa na madhara mengi. Kwa leo, nitaangazia usafi wa mazingira, mwili, vyakula na maji ya kunywa pamoja na usafi wa fikira. Najua wengi wameshangaa kusikia kuwa kuna usafi wa fikira. Msiwe na hofu kwani nitazungumzia usafi huo wa fikira katika dakika chache zijazo.

Usafi ni muhimu kwa binadamu hasa kwa sababu humwepusha na magonjwa mbalimbali yanayoweza kumwangamiza kabisa. Usafi pia ni muhimu kwa vile humwepusha binadamu kutokana na kuwa na harufu mbaya inayoweza kuwaathiri walio karibu naye.

Usafi wa mazingira ni muhimu sana kwa binadamu na hata kwa viumbe wengine wenye uhai. Mazingira safi husababisha kuwepo kwa hewa safi ya kupumua, maji safi ya kutumiwa na viumbe wote na hata mahali safi pa kuishi. Baadhi ya shughuli za kusafisha mazingira ni kama vile: kutotupa takataka ovyoovyo, kutomwaga kemikali na uchafu kwenye vianzo vya maji yetu, kukata nyasi ndefu zilizo karibu na maskani yetu, kuchimba mitaro ya kupitisha maji hasa nyakati za mvua ili yasituame na kuleta mbu, kutochoma takataka na mabaki ya mavuno shambani baada ya kuvuna ili kuzuia moshi hatari kuchafua hewa tunayopumua n.k.

Ningependa kuwahimiza kuwa tununue au tutengeneze vyombo vya kutumika kama majaa au mapipa ya kutupia takataka ili kuzuia utupaji ovyo wa takataka kila mahali. Hili ni jukumu la kila mmoja wetu ili tuweze kuyaweka mazingira yetu kuwa safi. Takataka zilizojaa kila mahali huleta nzi wengi pamoja na wadudu wengine wanaoweza kusababisha maradhi makali kwa binadamu. Viwanda ambavyo humwaga kemikali zao kwenye vianzo vya maji vinaombwa kutafuta njia mbadala za kuziharibu kemikali hizo. Nyasi zinapomea kupita kiasi karibu na maskani yetu huwa makao ya mbu ambao huzaana hapo na kusambaza ugonjwa wa malaria kwa binadamu. Fahamu kuwa ugonjwa huu wa malaria ni hatari sana kwa sababu unaweza kuwaua watu wengi sana kwa muda mfupi tu. Tunahimizwa kusafisha nyumba zetu, kufagia takataka zilizo katika nyua zetu, kusafisha madarasa ya wanafunzi, kusafisha makanisa na misikiti yetu pamoja na kusafisha masoko yetu na maduka makuu yanayouza bidhaa mbalimbali. Katika nyumba zetu tuzingatie usafi wa vyombo vya kupikia, malazi yetu, vyakula tunavyokula, maji tunayokunywa pamoja na vifaa vingine vya nyumbani.

Pili, ningependa kuzungumza kuhusu usafi wa mwili wa binadamu. Jambo moja ningependa mfahamu ni kuwa miili yetu iliumbwa kwa udongo kama tunavyosoma kwenye vitabu vya dini, kumaanisha tusipooga kwa muda mrefu bila shaka tutanuka. Harufu ya mtu ambaye hajaoga huwa mbaya sana. Mnajua hilo kweli? Ningependa kuwahimiza tutilie maanani sana usafi wa miili yetu kwa kuoga kila siku, kupiga mswaki kila siku, kuvaa nguo safi kila siku, kunyoa nywele zinazofaa kunyolewa, kuchana nywele za kichwani, kukata kucha na kulala kwenye malazi yaliyo safi. Madhara ya kutozingatia usafi wa mwili ni pamoja na kupatwa na magonjwa hatari yanayoweza kutuangamiza. Mtu asipokata kucha zake au kuziweka kuwa safi atapatwa na magonjwa hasa ya tumbo kwa sababu kucha hizo huhifadhi uchafu mwingi sana ambao husambazwa kwenye vyakula vyetu tunapokula. Nywele zisiponyolewa zinaweza kuingiwa na wadudu hatari wanaoitwa chawa ambao hufyonza damu ya binadamu na hii ni hatari sana kwa afya yetu. Kutosafisha malazi yetu kunaweza kupelekea kuwepo kwa wadudu waitwao kunguni ambao pia hufyonza damu ya binadamu na kumdhoofisha sana. Usafi wa mwili pia unahusisha

kunawa mikono kila mara baada ya kuingia msalani na kabla ya kula chakula. Hakikisha kuwa kila wakati unanawa mikono kwa kutumia maji na sabuni.

Aina ya mwisho nitakayozungumzia kwa sababu ninaona muda wangu umeisha ni usafi wa fikra. Najua wengi wenu mmeshangazwa na aina hii ya usafi kwa sababu labda unajiuliza ni vipi mtu anaweza kusafisha fikira zake kwa maji na sabuni. Ninapozungumza kuhusu usafi wa fikira, ningependa ujiulize fikira zako huwa za aina gani, wewe hutazama vipindi gani kwenye runinga, wewe husikiliza nini kwenye redio, wewe husoma nini kwenye mtandao na hata magazeti, majarida na vitabu mbalimbali? Nataka ujiulize maswali hayo. Usafi wa mawazo ni muhimu sana kwa sababu unaweza kujiepusha na mambo mabaya yasiyostahili katika jamii. Kuna watu ambao hutazama filamu chafu ambazo huathiri maadili yao. Unapata mtu aliyekuwa mzuri anabadilika na kuanza kujiingiza katika uhalifu wa kila aina kwa sababu ya mambo aliyoruhusu kuingia akilini mwake. Ningependa kuwahimiza kuwa mjaribu kuchunguza chochote kinachoingia akilini mwako. Jifundishe kusoma, kutazama na kusikiliza mambo yanayokujenga katika maadili ya kidini na hata kijamii.

Mwisho, ningependa kuwahimiza nyote kuwa mkitilia maanani usafi wa aina zote nilizozungumzia, bila shaka utakuwa umejiepusha na madhara mengi. Hutatumia pesa kila mara kwenda hospitalini. Mawazo yaliyo safi humpa mtu amani na utulivu wa akili na hivyo mwili mzima pamoja na kuwa na amani na unaoishi nao.

Nawashukuru nyote kwa kutenga muda kuhudhuria mkutano huu na kwa kunisikiliza. Asanteni sana na Mungu awabariki.

## Maswali ya ufahamu

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, someni tena hotuba kuhusu usafi kisha mjibu maswali yafuatayo.*

1. Mkutano huu ulihudhuriwa na kina nani?
2. Anayezungumza ni nani?
3. Jadili umuhimu wa usafi wa mazingira kwa binadamu.
4. Eleza shughuli zinazoweza kuchafua vianzo vya maji.
5. Kwa nini usafi wa mwili ni muhimu kwa binadamu.
6. Taja wadudu ambao huletwa na uchafu. Eleza madhara ya wadudu hawa.
7. Jadili njia za kuhifadhi usafi wa mwili wa binadamu.
8. Aya ya kwanza ya hotuba uliyosoma inazungumzia nini?
9. Eleza nafsi iliyotumika katika kutoa hotuba hii.
10. Mzungumzaji amehitimisha vipi hotuba yake?

## 11.2 Msamiati wa hotuba kuhusu usafi

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tafuteni msamiati mpya kutoka katika hotuba mliyosoma hapo awali kuhusu usafi kisha mweleze maana zao. Zingatieni muktadha wa hotuba hiyo. Mnaweza kutumia kamusi inapohitajika.*

**Kwa mfano:**

**usafi** – hali ya kuwa nadhifu

### Zoezi la 1

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, elezeni maana ya msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi zifuatazo, kisha mtunge sentensi sahihi kwa kutumia msamiati huo kama ulivyotumika katika hotuba mliyosoma kuhusu usafi.*

**Kwa mfano:** Kitanda chake kina *kunguni* wengi.

**Maana:** ***Kunguni*** – mdudu mdogo ambaye hujificha kitandani na hufyonza damu ya binadamu anapolala

***Matumizi katika sentensi:*** Nitanunua dawa ya kuwaua ***kunguni*** walio kitandani mwangu.

1. Wageni ***waalikwa*** waliandaliwa chakula kitamu.
2. ***Natumai*** utafika salama nyumbani.
3. Huyu ndiye mkuu wa ***mkoa*** wetu.
4. Nani atazungumza kwenye ***mkutano*** unaoandaliwa?
5. Ukosefu wa usafi huweza kusababisha ***madhara*** mengi hasa kwa binadamu.
6. Viwanda vinahimizwa kukomesha umwagaji wa ***kemikali*** katika vianzo vya maji.
7. Watu wanashauriwa kuchimba ***mitaro*** ya kupitisha maji hasa nyakati za mvua.
8. ***Majaa*** ya kutupia takataka yatazuia utupaji ovyo wa takataka.
9. Usafi wa fikira huboresha ***maadili*** yetu.
10. Uchafu katika ***vianzo*** vya maji husababisha magonjwa mengi kwa binadamu.

### Zoezi la 2

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, chunguzeni picha zifuatazo kisha mwelezane madhara yake kwa binadamu na wanyama wengine.*








## 11.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, jadilini kuhusu sehemu kuu za hotuba kwa kurejelea mfano wa hotuba mliyosoma hapo awali kuhusu usafi. Kila kikundi kiwasilishe matokeo ya majadiliano yao mbele ya wanafunzi wenzao.*

**Kwa mfano:** Hotuba huwa na utangulizi ambao uhusisha salamu.

### Maelezo muhimu

**Sehemu za hotuba ni:**

a) Mada au kichwa cha hotuba

Mada ya hotuba hutambulisha jambo linalozungumziwa na mara nyingi huwa haizidi maneno manane.

b) Utangulizi au mwanzo wa hotuba

Utangulizi wa hotuba mara nyingi huwa ni aya moja tu. Huhusisha kuwatambua wanaokusikiliza pamoja na kutoa salamu. Mzungumzaji hujitambulisha hapa.

ch) Mwili wa hotuba

Sehemu hii hubeba ujumbe kamili wa hotuba nzima. Aya kadhaa huandikwa hapa kwa namna ya kutiririsha maudhui yanayozungumziwa kutoka mwanzo hadi mwisho wa hotuba.

d) Hitimisho au mwisho wa hotuba

Sehemu hii huwa na sentensi chache tu katika aya moja. Hitimisho hufupisha yaliyozungumziwa katika mwili wa hotuba. Mzungumzaji huwashukuru wasikilizaji na kuwaaga.

## 11.4 Kusikiliza na kuzungumza: Kutunga hotuba

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, tungeni hotuba kuhusu mada yoyote kwa kuzingatia sehemu za hotuba mlizojadili hapo awali. Kila kundi liwasilishe hotuba yao mbele ya wanafunzi wenzao.*

### Maelezo muhimu

Mwongozo wa kuandika hotuba:

1. Aya ya kwanza huhusu kutambulisha kitakachozungumziwa, salamu na kujitambulisha kwa msemaji.
2. Hotuba huandikwa katika nafsi ya kwanza na huwa katika usemi asili.
3. Hotuba huandikwa katika wakati uliopo.
4. Aya kadhaa zinazofuata utangulizi huhusu ujumbe wa hotuba nzima.
5. Aya ya mwisho huhitimisha hotuba kwa kutoa shukrani na kuwaaga wasikilizaji.
6. Lugha sahihi kisarufi na inayoeleweka hutumika.

### Zoezi la kuandika

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, bunini hotuba kuhusu umuhimu wa maji kwa binadamu na wanyama kwa kuzingatia sehemu kuu za hotuba pamoja na sifa za hotuba mlizofundishwa hapo awali.*

## 11.5 Sarufi: Uambishaji wa vitenzi

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, chunguzeni mabadiliko ya vitenzi vifuatavyo vinaponyambuliwa katika kauli mbalimbali kisha mjaze kwa usahihi nafasi zilizoachwa wazi katika jedwali hili.*

| **Kitenzi (kauli ya kutenda)** | **Kauli ya kutendea** | **Kauli ya kutendeka** | **Kauli ya kutendewa** | **Kauli ya kutendesha** | **Mzizi wa kitenzi** |
|---|---|---|---|---|---|
| *lima* | *limia* | *limika* | *limiwa* | *limisha* | *lim* |
| *chora* | *chorea* | *choreka* | *chorewa* | *choresha* | *chor* |
| *tembea* | *tembelea* | *tembeleka* | *tembelewa* | *tembeza* | *tembe* |
| andika | __________ | andikika | __________ | andikisha | __________ |
| __________ | somea | __________ | somewa | __________ | som |
| samehe | __________ | sameheka | __________ | samehesha | __________ |
| __________ | vunjia | __________ | vunjiwa | vunjisha | __________ |

## Zoezi la 3

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, onyesheni sehemu zinazounda maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi zifuatazo.*

**Kwa mfano:** *Mama <u>anapika</u> chakula cha wageni.*

**Jibu:** Neno lililopigiwa mstari katika sentensi hii ni kitenzi '*anapika*'. Neno hili limeundwa kwa silabi zinazoonyesha *nafsi* na *wakati* pamoja na *mzizi wa kitenzi* na *silabi za kumalizia*. Yaani: ***a+na+pik+a***

1. Mtoto <u>atachora</u> mchoro wa kasri la mfalme.
2. Kijana yule <u>anakimbia</u> upesi kuelekea shuleni.
3. Nyanya <u>alipanda</u> mahindi mengi mwaka uliopita.
4. Mwalimu <u>anawafundisha</u> wanafunzi Hisabati.

## Zoezi la 4

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, chunguzeni vitenzi katika jedwali lifuatalo kwa kuonyesha silabi zinazoviunda. Jazeni kwa usahihi nafasi zilizoachwa wazi.*

| **Kitenzi** | **Kiambishi cha nafsi** | **Kiambishi cha wakati** | **Mzizi wa kitenzi** | **Kimalizio** |
|---|---|---|---|---|
| alicheza | a | li | chez | a |
| ataimba | __________ | __________ | __________ | __________ |
| tutatembea | __________ | __________ | __________ | __________ |
| watapanda | __________ | __________ | __________ | __________ |

*Je, mmegundua nini katika vitenzi mlivyoainisha?*

## Maelezo muhimu

- Hali ya kuongeza herufi maalum au viambishi mwanzoni na mwishoni mwa mizizi ya vitenzi ili kupata maana ya ziada huitwa uambishaji wa vitenzi.

**Mifano:** ***anapenda*** = a+na+pend+a

'a' ni kiambishi cha nafsi ya tatu umoja (yeye)

'na' ni kiambishi cha wakati uliopo

'pend' ni mzizi wa kitenzi 'penda'

'a' ni kimalizio cha kitenzi 'penda'.

- Herufi maalum zinazoongezwa mwanzoni au mwishoni mwa mzizi wa kitenzi huitwa ***viambishi***.
- Sehemu ya kitenzi ambayo haibadiliki baada ya kitenzi hicho kunyambuliwa huitwa ***mzizi wa kitenzi***.

## Zoezi la 5

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, onyesheni mizizi ya vitenzi vilivyopigiwa mistari katika sentensi zifuatazo.*

**Kwa mfano:** Dada yangu ***anakimbia*** sokoni kununua mboga.

**Jibu:** Mzizi wa kitenzi *kimbia* ni ***kimb'.***

1. Mimi ninashona nguo za maharusi.
2. Ngabo anasoma kitabu cha hadithi za kale.
3. Nitamsamehe rafiki yangu aliyenikosea.
4. Kwa nini unaniangalia kwa macho makali hivyo?
5. Hotuba huandikwa katika usemi asili.

## Zoezi la 6

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, ainisheni vitenzi vilivyopigiwa mistari katika sentensi zifuatazo kwa kuonyesha viambishi vinavyoviunda.*

**Kwa mfano:** *Mugabo anatoroka kwa hofu.*


**Jibu:** a+na+torok+a (*nafsi, nyakati, mzizi, kimalizio*)

1. Msichana anachora picha ya mtoto.
2. Gasimba anakimbia kuelekea shuleni.
3. Mama anafuma fulana ya Mutoni.
4. Mimi ninaandika barua ya babangu.
5. Kesho nitafuta ubao wa darasa letu.

# Somo la 12: Sifa za hotuba

## 12.1 Hotuba kuhusu ushirikiano wa kijinsia

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, tazameni michoro hii kisha msome hotuba inayofuata kuhusu ushirikiano wa kijinsia na baadaye mjibu maswali ya ufahamu.*




Mgeni wetu wa heshima, Bi Alice Mukagatare, wageni waalikwa, machifu, manaibu wa machifu, mwenyekiti wa baraza la wazee, wazee wa kijiji na wananchi kwa jumla hamjambo! Hamjambo tena! Ningependa kuwashukuru sana kwa kuitikia mwito wa kuhudhuria mkutano huu kwa wingi. Ni matumaini yangu kuwa kila mmoja wetu anafahamu dhahiri shahiri sababu ya kuwaalika katika mkutano huu. Tumekuwa na visa vingi vya unyanyasaji wa watu hasa wa jinsia ya kike. Wanawake katika kijiji hiki wamedharauliwa na kupuuzwa sana na hivyo, nikaona ni bora tukutane ili tujadiliane kuhusu umuhimu wa kushirikiana kijinsia ili kuboresha maisha yetu kama wanakijiji kimoja.

Kama ilivyo kwenye baadhi ya vitabu vya dini, sote tuliumbwa na Mungu tena kwa malighafi sawa. Hili linamaanisha kuwa tunafaa kuishi kwa kushirikiana pamoja na kwa amani. Kila mtu hapa ana uwezo tofauti. Kwa hivyo tukifanya kazi kwa pamoja bila shaka tutafanikiwa. Kumbukeni kuwa mbele ya Mungu sote tuko sawa, wanaume kwa wanawake. Kwa hivyo ni vyema tuheshimiane. Kila mtu auheshimu uwezo wa mwenzake na maarifa aliyo nayo mwenzake. Ni vyema pia tuhimizane katika shughuli zetu. Mwenzako anaposhiriki katika shughuli yoyote, usimvunje moyo iwapo hakufikia kiwango ulichotarajia bali mtie moyo ili wakati mwingine ajitahidi na kuwa bora.

Juzi kulikuwa na malalamiko katika ofisi yetu kuhusu waajiri ambao hawawaajiri wanawake kwa sababu wanachukulia kuwa wanawake hawajasoma, hawana maarifa yoyote au nguvu za kufanya kazi. Hilo ni kweli? Kwa mfano, katika ofisi yangu,

nimewaajiri wanawake wengi ambao wanafanya kazi zao vizuri tu sawa na wanaume nilioajiri. Kwa kweli hizi ni fikira potovu dhidi ya wanawake ambazo zinafaa zikomeshwe. Tunafaa kufahamu kuwa wanawake wengi siku hizi wamesoma hadi viwango vya juu sana vya elimu na hivyo wana uwezo wa kufanya kazi sawa tu na wanaume. Shule zetu za msingi na sekondari zina idadi karibu sawa za wasichana na wavulana, kumaanisha wote wanasoma kwa pamoja na hivyo wanapata maarifa kwa pamoja. Wanawake sawa na wanaume wana uwezo wa kushiriki katika biashara mbalimbali na wakafaulu. Kama mnavyofahamu, duka kuu la kuuza bidhaa za aina zote lililo katikati ya mji wa Kigali limesimamiwa na mkurugenzi ambaye ni mwanamke. Biashara hiyo inazidi kupanuka kila uchao. Mkurugenzi huyu amewaajiri wafanyakazi wa jinsia zote. Angekuwa na ubaguzi angewaajiri wanawake pekee. Hivyo, yeye ni mfano mwema wa kuigwa kwa kuonyesha kuwa mtu yeyote licha ya jinsia yake anaweza kufanya kazi vizuri na kufaulu maishani. Wanawake wote mliohudhuria mkutano huu leo, fahamuni kuwa mna uwezo wa kuinuka na nyota zenu zikang'aa kote duniani.

Ushirikiano katika ndoa ni muhimu sana. Kuna wanaume wanaodhani kuwa wake zao wanafaa kukaa nyumbani na kufanya kazi za nyumbani pekee bila kufahamu kuwa wake hawa wana uwezo wa kufanya kazi nyingine na kupata ujira. Mume na mke wanaoshirikiana katika shughuli zote mle nyumbani hufaulu, huwa na furaha na ndoa yao hudumu kwa muda mrefu kinyume na familia ambapo mume amemfinyilia chini mke wake. Katika kiwango cha familia, kila mtu ana wajibu wake wa kutekeleza na ushirikiano ni muhimu sana. Tunahimizwa kuzoea kuwasiliana katika ndoa zetu, tusivunje mawasiliano kamwe. Ni vyema kushauriana kila mara na kuonyeshana njia nzuri ya kufuata. Mwenzako anapokosea, mkosoe kwa upendo ila usimzomee na kuidharau jinsia yake. Kumbuka sio wewe uliyemuumba, kwa hivyo mkubali, mpende na umheshimu alivyo.

Namshukuru Mola kwa umoja, amani na ushirikiano aliotupa sisi Wanyarwanda. Nchi yetu inafahamika sana kwa shughuli ya *Umuganda*. Hii huwa ni shughuli ya kuyasafisha mazingira yetu angalau mara moja katika kila mwezi. Katika siku hii, kila Mnyarwanda huziacha shughuli zake za kielimu, kibiashara, kisiasa, kidini na hata kibinafsi na kuungana pamoja katika kuyasafisha mazingira ya tunakoishi. Kila mtu, wanaume kwa wanawake hubeba majembe, fagio, panga, reki, ndoo n.k. kwa ajili ya shughuli ya usafi. Ulimwengu mzima hutamani kuwa kama nchi yetu kwa ajili ya ushirikiano huu. Nawapongeza sana kwa kujihusisha na shughuli ya Umuganda na ningewahimiza tuzidi kushirikiana licha ya jinsia zetu.

Katika siasa, wanaume kwa wanawake wameweza kuchaguliwa kuiongoza nchi yetu katika viwango mbalimbali. Tumekuwa na wanawake ambao wameshikilia nyadhifa kubwa kubwa katika serikali na wameweza kuzidhibiti nafasi hizo vizuri.

Tumeona maendeleo na mafanikio katika vitengo ambapo wanawake ni viongozi. Hili linamaanisha kuwa jinsia haiwezi kumzuia mtu kufanikiwa na kufanikisha wengine. Kwa hivyo, tufahamu kuwa wanaume kwa wanawake wana uwezo wa kukwea katika ngazi ya maendeleo na mafanikio.

Katika shughuli za ukulima na ufugaji, sote tuna uwezo wa kushirikiana ili kuboresha maisha yetu binafsi pamoja na kuendeleza uchumi wa taifa letu. Tukishirikiana sote katika kulima na kupanda mashamba yetu pamoja na kuitunza mifugo yetu bila shaka tutafanikiwa. Nawaomba nyote mliofika hapa leo mhimizike kushirikiana katika shughuli zenu zote. Tunawafahamu wakulima na wafugaji ambao ni wanawake wanaofanya vyema sana na pia tunawafahamu wakulima na wafugaji ambao ni wanaume na pia wanafanya vyema. Tusidharau jinsia yoyote ile.

Katika michezo, wanawake na wanaume wana uwezo na talanta za kushiriki katika riadha na michezo mingine ya mipira. Hapa nchini tuna timu za kandanda, mpira wa nyavu, mpira wa pete, mpira wa magongo n.k. ambazo ni za wanaume na pia kuna timu za wanawake. Timu hizi hushiriki katika mashindano mbalimbali na zote huweza kuibuka na ushindi.

Mwisho, ningependa kuwahimiza nyote kuwa, tujitahidi kadri ya uwezo wetu kuishi vyema na watu wa jinsia zote bila kuwabagua wengine wala kuwadharau. Kama wasemavyo wahenga, umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu. Nashukuru sana kwa kutenga muda wenu kunisikiliza. Natumai mmefaidika. Yeyote atakayepatikana akiwanyanyasa au kuwadharau watu wa jinsia yoyote ile atachukuliwa hatua kali za kisheria. Mungu awabariki. Asanteni.

## Maswali ya ufahamu

1. Eleza sababu ya mkutano huu kuandaliwa.
2. Taja watu waliohudhuria mkutano huu.
3. Utangulizi wa hotuba hii unahusu nini?
4. Watu wanahimizwa kuishi vipi katika ndoa zao?
5. Ni shughuli zipi za kuinua uchumi ambazo wanawake na wanaume wanaweza kushirikiana?
6. Kwa nini wanaume huwadharau wanawake? Toa maoni yako binafsi.
7. Je, mwanamke ana faida katika jamii? Jadili.
8. Eleza shughuli ambazo hufanyika wakati wa *Umuganda*.
9. Hitimisho la hotuba hii linahusu nini?
10. Eleza maana ya '...*sote tuliumbwa na Mungu tena kwa malighafi sawa*'.

## 12.2 Msamiati kutokana na hotuba ya ushirikiano wa kijinsia

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tafuteni msamiati mpya kutoka katika hotuba mliyosoma kuhusu ushirikiano wa kijinsia kisha mweleze maana zake. Zingatieni muktadha wa hotuba mliyosoma. Mnaweza kutumia kamusi inapohitajika.*

**Kwa mfano:**

***malighafi*** – vitu ambavyo hutumika kutengeneza vitu vingine

### Zoezi la 1

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, elezeni maana ya msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi zinazofuata kisha mtunge sentensi sahihi kwa kutumia maneno hayo. Zingatieni matumizi ya msamiati huo katika muktadha wa hotuba mliyosoma. Mnaweza kutumia kamusi inapohitajika.*

**Kwa mfano:** Leo kutakuwa na mkutano wa *baraza* la wazee wa kijiji chetu.

***Maana***: *baraza* – kundi la watu wenye majukumu maalum

***Matumizi katika sentensi:*** ***Baraza*** la wazee liliamua kumsamehe mwanakijiji huyo.

1. ***Mwenyekiti*** wa kamati ya walimu na wazazi wa shule yetu amefika.
2. Nawashukuru kwa kuitikia ***mwito*** wa kuhudhuria mkutano huu.
3. Ni ***dhahiri shahiri*** kuwa nyote mnamfahamu mgeni wetu wa leo.
4. ***Unyanyasaji*** wa wanawake ni hatia nchini mwetu.
5. Watu wa ***jinsia*** zote wanafaa kuheshimiwa.
6. Mwalimu mkuu ***alituhimiza*** tutie bidii katika masomo yetu.
7. Pamekuwepo na ***malalamiko*** mengi kuhusu wizi uliozidi katika kijiji hiki.
8. Kumdharau binadamu yeyote ni fikira ***potovu***.
9. Baba yangu ndiye ***mkurugenzi*** wa kampuni ya kutengeneza unga.
10. ***Ubaguzi*** wa rangi hauruhusiwi katika nchi yetu.

## 12.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano kuhusu sifa za hotuba

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadilini kuhusu sifa za hotuba kwa kurejelea hotuba mliyosoma hapo awali kuhusu ushirikiano wa kijinsia. Kila kikundi kiwasilishe matokeo yake ya majadiliano mbele ya wanafunzi wenzao.*

**Kwa mfano:**

Mojawapo ya sifa za hotuba ni kuwa: huandikwa katika wakati uliopo.

### Maelezo muhimu

Sifa za hotuba:

- Aya ya kwanza huwa utangulizi na hutambulisha kitakachozungumziwa, salamu na msemaji.
- Aya kadhaa zinazofuata utangulizi huhusu ujumbe wa hotuba nzima.
- Hotuba huandikwa katika nafsi ya kwanza na huwa katika usemi asili.
- Hotuba huandikwa katika wakati uliopo.
- Aya ya mwisho huhitimisha hotuba kwa kutoa shukrani na kuwaaga wasikilizaji.

## 12.4 Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadilini kuhusu athari za unyanyasaji wa kijinsia katika jamii na taifa zima kwa ujumla. Kila kikundi kiwasilishe matokeo yake ya majadiliano mbele ya wanafunzi wenzao.*

**Kwa mfano:** Unyanyasaji wa kijinsia husababisha chuki na utengano kati ya watu wa jinsia zinazohusika.

### Zoezi la 2

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, bunini hotuba kuhusu umoja wa Wanyarwanda kwa kueleza shughuli kadhaa ambazo huchangia katika kuwepo kwa umoja huo miongoni mwa Wanywarwanda wote, wadogo kwa wakubwa. Kila kikundi kisome hotuba yake mbele ya wanafunzi wenzao.*

## 12.5 Sarufi: Uambishaji wa vitenzi

1. *Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, unganisheni silabi hizi ili kuunda vitenzi kamili na sahihi.*

   **Kwa mfano:** a+li+pik+a = alipika

   1. tu+ta+wa+funik+a
   2. m+na+tu+chez+e+a
   3. m+si+ni+pig+e
   4. ki+li+cho+chor+w+a
   5. a+li+ye+lim+a

*Je, mmegundua nini katika uchunguzi wenu?*

2. *Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, elezaneni maana inayobebwa na silabi mbalimbali zinazounga maneno yaliyo katika swali la 1.*

**Mfano 1:** *tu+ta+wa+funik+a*

**Jibu:**

- Kiambishi *'tu-'* kinasimamia nafsi ya kwanza wingi
- Kiambishi *'-ta-'* kinasimamia wakati ujao
- Kiambishi *'-wa-'* kinasimamia mtendewa (watakaotendewa kitendo cha kufunikwa)
- Sehemu ya *'-funik-'* ni mzizi wa kitenzi
- Kiambishi *'-a'* ni kimalizio

**Mfano 2:** *m+si+ni+pig+e*

**Jibu:**

- Kiambishi *'m-'* kinasimamia nafsi
- Kiambishi '-si-' kinasimamia kikanushi
- Kiambishi '-ni-' kinasimamia mtendewa (anayetendewa kitendo cha kupigwa)
- Sehemu ya '-pig-' ni mzizi wa kitenzi
- Kiambishi '-e' ni kimalizio katika hali kanushi

**Mfano 3:** ki+li+cho+chor+w+a

**Jibu:**

- Kiambishi *'ki-'* kinasimamia ngeli ya KI-VI
- Kiambishi *'-li-'* kinasimamia wakati uliopita
- Kiambishi *'-cho-'* kinasimamia kirejeshi (kinarejelea nomino husika)
- Sehemu ya *'-chor-'* ni mzizi wa kitenzi
- Kiambishi *'-w'* ni kiambishi cha mnyambuliko (kauli ya kutendwa)
- Kiambishi *'-a'* ni kimalizio

## Zoezi la 3

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, ainisheni vitenzi vilivyopigiwa mistari katika sentensi zifuatazo kwa kueleza maana ya kila kiambishi kinachounda vitenzi hivyo.*

**Kwa mfano:** Gari lililoanguka ni la jirani yetu.

**Jibu:**

- Kiambishi *'li-'* kinasimamia ngeli ya LI-YA
- Kiambishi *'-li-'* kinasimamia wakati uliopita

- Kiambishi *'-lo-'* kinasimamia kirejeshi (kinarejelea nomino '*gari*')
- Sehemu ya *'-anguk-'* ni mzizi wa kitenzi
- Kiambishi *'-a'* ni kimalizio

1. Nguo aliyonunuliwa ilikuwa ndefu sana.
2. Mama alichimbua mihogo mingi jana.
3. Kwa nini unaniangalia hivyo?
4. Mwalimu anafundisha somo la Kiswahili.
5. Rais aliwahutubia wananchi jana katika shule ya Gikondo.
6. Duka la shangazi yetu halijafunguliwa leo.
7. Mimi sitapiga nguo hizo pasi.
8. Kitabu cha hadithi hakijasomwa na mwanafunzi.
9. Babu anamwandikia baba barua ndefu.
10. Tutasafiri kwenda mjini wiki ijayo.

## Maelezo muhimu

- Silabi ambazo huwekwa mwanzoni mwa mzizi wa kitenzi huitwa ***viambishi awali***. Viambishi awali huweza kubeba maana ya: nafsi, nyakati, vikanushi, watendewa, watendwa, virejeshi n.k.

  **Kwa mfano:** *nisiyemtaka* = ('*ni-'* – nafsi, '*-si-'* - kikanushi, *'-ye-'*- kirejeshi, *'-m-'* - mtendewa)
- Sehemu ya kitenzi ambayo huwa haibadiliki baada ya kunyambua kitenzi hicho katika kauli mbalimbali huitwa ***mzizi wa kitenzi***.

  **Kwa mfano:** mzizi wa kitenzi '*ruka'* ni '*ruk'*.
- Silabi ambazo huwekwa mwishoni mwa mzizi wa kitenzi huitwa ***viambishi tamati***. Hivi huweza kuwa na maana ya kuonyesha minyambuliko mbalimbali au kuwa vimalizio au viishio.

  **Kwa mfano:** Katika kitenzi '*alipikiwa*', viambishi tamati ni '-*iw*-' (mnyambuliko) na '-*a*' (kimalizio).

## Zoezi la 4

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tungeni sentensi zenye vitenzi vilivyo na viambishi vifuatavyo.*

**Kwa mfano:** Kiambishi cha ngeli ya LI-YA, kikanushi, kirejeshi, mzizi, mnyambuliko, kimalizio


**Jibu:** *lisiloendeshwa, yasiyoendeshwa, lisilopikika, yasiyopikika, lisilochomolewa, yasiyochomolewa* n.k.

1. Kiambishi cha nafsi, wakati uliopo, mtendewa, mzizi na kimalizio
2. Kiambishi cha ngeli ya I-ZI, wakati uliopita, kirejeshi, mzizi, mnyambuliko, kimalizio
3. Kiambishi cha ngeli ya A-WA, wakati ujao, kirejeshi, mtendewa, mzizi, kimalizio
4. Kiambishi cha nafsi, kikanushi, kirejeshi, mtendewa, mzizi, kimalizio
5. Kiambishi cha ngeli ya PA-KU-MU, wakati timilifu, mzizi na kimalizio

# Somo la 13: Hotuba na insha

## 13.1 Hotuba kuhusu kupigana na umaskini

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tazameni picha na michoro hii kisha msome hotuba inayofuata kuhusu kupigana na umaskini kupitia kwa elimu, biashara na kilimo na baadaye mjibu maswali ya ufahamu.*




Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, wageni waheshimiwa, wageni wengine waalikwa, mabwana na mabibi hamjambo! Habari za asubuhi? Nachukua fursa hii adimu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa leo na kwa kutukirimia afya njema. Nawashukuru nyote mliotenga muda wenu ili kuhudhuria mkutano huu. Ni matumaini yangu kuwa mtafaidika kutokana na mambo machache ambayo nitayazungumzia. Kama tunavyojua, mkoa wetu umekumbwa na umaskini mwingi na hiyo ndiyo sababu Bwana Ngabo, mkuu wa mkoa huu, aliniomba nije kuzungumza na wananchi wa sehemu hii kuhusu mbinu mbalimbali za kupigana na umaskini na kuboresha hali zenu.

Kwanza, umaskini ni hali ya kutokuwa na chakula, mavazi na mahitaji mengine ambayo ni ya kimsingi kwa binadamu. Janga hili la umaskini huwaathiri watu wa makundi mbalimbali, si wazee, si vijana na hata watoto. Ukosefu wa chakula cha kutosha huweza kusababisha magonjwa kama vile utapiamlo, ukosefu wa damu mwilini na magonjwa mengine. Uhaba huu wa vyakula na mahitaji mengine ya kimsingi pia huweza kusababisha vifo.

Ningependa kuzungumzia mbinu mbalimbali ambazo tunaweza kuzihusisha katika harakati zetu za kujikomboa kutoka kwenye hili janga la umaskini. Elimu ni kiungo muhimu sana kinachoweza kuondoa umaskini katika maisha ya binadamu. Katika harakati za utafiti wangu, nilipata takwimu zinazoonyesha kuwa katika mkoa huu kuna watoto wengi ambao wamefikisha umri wa kwenda shule lakini badala ya kupelekwa shuleni wazazi wao, wamewaweka nyumbani ili wawasaidie kufanya

biashara ndogo ndogo. Wazazi wote wanafaa kufahamu kuwa elimu ndio ufunguo wa maisha ya binadamu. Watoto wetu wakielimika basi itakuwa rahisi kwao kupata ajira hapo baadaye au hata kufanya biashara nzuri na hatimaye kuinua kiwango cha uchumi cha jamii zetu. Elimu huwawezesha watu kupata maarifa ya jinsi ya kuanzisha miradi mbalimbali inayoweza kuifaidi jamii kwa kiwango kikubwa. Kwa hivyo, nawaomba hivi, tuwapeleke watoto wetu shuleni ili wapate elimu itakayowasaidia wao wenyewe pamoja na kuisaidia jamii yao katika siku za usoni.

Mbinu nyingine muhimu ya kupigana na umaskini ni kupitia kwa kilimo. Ikiwa watu wengi watajihusisha na shughuli za ukulima na ufugaji, bila shaka patakuwepo na vyakula vya kutosha kuwakidhi wanajamii wetu. Mazao ya shambani pamoja na ya mifugo yakiuzwa, wakulima wataweza kupata fedha za kukidhi mahitaji yao ya kimsingi. Kutokana na kilimo, watu wengi wanaweza kupata ajira mbalimbali kama vile: ajira ya kulima katika mashamba makubwa makubwa, kuvuna, kuuza dawa za kuwanyunyizia mifugo pamoja na mimea, wafanya biashara watapata mazao ya kuuza na wasafirishaji pia watakuwa na kazi ya kufanya miongoni mwa ajira nyingine nyingi. Kilimo kinaweza kuisaidia jamii yetu pamoja na kuifungulia milango ya kuuza mazao yetu katika nchi za ng'ambo na hivyo kupata pesa za kutosha. Pia, tunaweza kuuza mazao yetu katika mikoa mingine na kujipatia kipato. Nawaomba tafadhali, tusiwe wavivu wa kuamka wakati jua tayari lishachomoza bali tujitahidi kurauka mapema na kutafuta shughuli ya kujihusisha nayo ili kupata riziki.

Mbinu nyingine ya kupunguza umaskini katika jamii yetu ni kwa kuwateua viongozi wanaofaa na wanaojali maslahi ya wananchi. Tunahitaji viongozi waliowajibika. Viongozi tunaowachagua huwa na jukumu la kusaidia katika kuboresha maisha ya watu wanaoongoza. Kwa mfano, tukiwachagua viongozi ambao ni fisadi na walafi wanaopenda kujilimbikizia pesa nyingi kutoka kwa serikali basi tutaishia kufa maskini. Viongozi wa aina hii ni hatari kwa sababu badala ya kutumia fedha anazopewa na serikali ili kuyaendeleza maisha ya wanajamii wake, yeye huzitumia fedha hizo kwa mahitaji yake ya kibinafsi. Mwishowe, mwananchi anabakia katika lindi la umaskini ilhali viongozi hao wanaishi maisha ya starehe na anasa tupu. Viongozi wazuri ni wale wanaohakikisha kuwa barabara nzuri zimejengwa hivyo kurahisisha shughuli za kibiashara pamoja na shughuli nyingine zinazohitaji usafiri. Viongozi hawa watahakikisha kuwa hospitali zimejengwa na kupewa vifaa vinavyohitajika pamoja na kuhakikisha kuwa vijana wanapata ajira ili waweze kuisaidia jamii yao. Chini ya uongozi wa viongozi waliowajibika, kodi ambazo wananchi hutozwa zitaweza kutumika kwa njia zinazowafaidi wananchi wenyewe na wala sio kuishia kwenye mifuko ya viongozi walafi. Tafadhali, nawahimiza muwe makini mnapowateua viongozi wenu. Hao ndio madereva wa nchi yetu tunamoishi.

Mahusiano na mataifa mengine pia ni mbinu mojawapo inayoweza kutusaidia kukabiliana na umaskini katika jamii yetu. Kuwepo kwa mahusiano mema na watu wa mataifa mengine huweza kupanua masoko yetu na hivyo biashara zetu kuwanda. Biashara zetu zinapotanda kila mahali watu hupata ajira na faida huwa tele. Wanajamii huweza kuuza bidhaa zao katika nchi nyingine na hata kununua bidhaa wanazohitaji kutoka nchi nyingine kwa bei nafuu. Viongozi wetu ndio wanaofaa kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kuwa mahusiano yetu na mataifa mengine ni mazuri.

Serikali yetu inaweza kubuni mikakati ya wananchi kujitengenezea baadhi ya bidhaa za kutumia nchini badala ya kununua bidhaa hizi kutoka katika mataifa mengine kwa gharama ya juu. Kwa mfano, tunaweza kujitengenezea bidhaa za kimsingi kama vile: sukari, maziwa, mikate, unga, mahindi, nguo n.k. Mbinu hii itaweza kuwasaidia wananchi kupata bidhaa za kimsingi kwa bei nafuu na kwa ukaribu. Pia kupitia kwa shughuli kama hii, ajira nyingi zitapatikana kwa wananchi wetu ambao wataajiriwa ili kufanya kazi katika viwanda hivyo.

Mwisho, ningependa kuwahimiza nyote mliofika hapa kuwa mjitahidi angalau kutafuta shughuli ambayo inaweza kuwapatia pesa za matumizi ya kila siku. Unaweza kujishughulisha na kilimo au ukatafuta ajira au hata ukaanzisha biashara yako mwenyewe iliyo na uwezo wa kukua. Tusipoteze muda wetu katika kunywa pombe na kukaa tu bure bila kufanya kazi. Msemo unasema kuwa ukitaka kuwa tajiri sharti ufanye kazi. Kwa hivyo, kila mtu ajitahidi kufanya kazi. Asanteni kwa kunisikiliza. Mungu awabariki nyote.

## Maswali ya ufahamu

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, someni tena hotuba kuhusu kupigana na umaskini kisha mjibu maswali yafuatayo.*

1. Eleza utangulizi wa hotuba hii unahusu nini.
2. Kwa nini msemaji wa hotuba hii alikuwa amealikwa kuwahutubia wanakijiji?
3. Jadili namna elimu inavyoweza kuwasaidia wanajamii kupigana na umaskini.
4. Eleza umuhimu wa kilimo katika kupigana na umaskini.
5. Kwa nini wanakijiji wanahimizwa kuwa makini wanapowateua viongozi wao?
6. Jadili umuhimu wa biashara katika jamii.
7. Mahusiano ya kimataifa yanaweza kusaidia vipi kukabiliana na umaskini?
8. Jadili sehemu kuu za hotuba hii.
9. Msemaji katika hotuba hii amehitimisha hotuba yake vipi?
10. Taja ajira zinazoweza kupatikana kupitia kwa shughuli za kilimo.

## 13.2 Msamiati kutokana na hotuba husika

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tafuteni msamiati mpya kutoka katika hotuba mliyosoma hapo awali kuhusu kupigana na umaskini kisha mweleze maana zake. Zingatieni muktadha wa hotuba hiyo. Mnaweza kutumia kamusi inapohitajika.*

**Kwa mfano:**

***janga*** – tukio baya ambalo linaweza kusababisha taabu, mateso au maafa

### Zoezi la 1

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, elezeni maana ya msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi zifuatazo kisha mtunge sentensi sahihi kwa kutumia msamiati huo kama ulivyotumika katika hotuba mliyosoma kuhusu kupigana na umaskini.*

**Kwa mfano:** Kalisa aliamka baada ya jua <u>kuchomoza</u>.

**Maana:** ***kuchomoza*** – kutokeza kwa jua na kuonekana

***Matumizi katika sentensi:*** Sisi huenda shuleni kabla ya jua ***<u>kuchomoza</u>***.

1. Wageni ***<u>waheshimiwa</u>*** walikaribishwa katika sebule iliyopambwa.
2. Siku hizi pesa zimekuwa ***<u>adimu</u>*** sana.
3. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa ***<u>kutukirimia</u>*** afya njema.
4. Msemaji aliwashukuru wanakijiji kwa ***<u>kutenga</u>*** muda wao ili kuhudhuria mkutano.
5. Serikali iko katika ***<u>harakati</u>*** za kuanzisha miradi mingine.
6. ***<u>Utapiamlo</u>*** ni ugonjwa ambao huwapata watoto.
7. Kila mtu akijitahidi kufanya kazi atapata ***<u>riziki</u>***.
8. Viongozi walafi hupenda ***<u>kujilimbikizia</u>*** pesa na kuwasahau wananchi waliowachagua.
9. Tujitahidi kufanya kazi ili tujiondoe katika ***<u>lindi</u>*** la umaskini.
10. Wananchi wanashauriwa wasiwachague viongozi ***<u>fisadi</u>***.

## 13.3 Matumizi ya lugha: Tofauti kati ya hotuba na insha

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, jadilini kuhusu:*

a) Tofauti zilizopo kati ya insha na hotuba.
b) Uhusiano uliopo kati ya insha na hotuba.

*Kila kikundi kiwasilishe matokeo yake ya majadiliano mbele ya wanafunzi wenzao.*

**Kwa mfano:**

***Tofauti:*** Hotuba huwa ni taarifa inayosemwa mbele ya hadhira ilhali insha huandikwa ili isomwe na mtahini au wasomaji wengine.

***Uhusiano:*** Insha na hotuba huwa na sehemu kuu ambazo ni: utangulizi, mwili na hitimisho.

## Zoezi la 2

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, tungeni:*

a) Insha ya maelezo kuhusu umuhimu wa maji.

b) Hotuba kuhusu umuhimu wa maji.

*Kila kikundi kiwasomee wanafunzi wenzao insha pamoja na hotuba walizobuni kuhusu umuhimu wa maji.*

## 13.4 Kusikiliza na kuzungumza: Kutunga hotuba

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, tungeni hotuba kuhusu umuhimu wa Umuganda kwa Wanyarwanda kwa kuzingatia sehemu za hotuba mlizojadili hapo awali. Kila kundi liwasilishe hotuba yao mbele ya wanafunzi wenzao.*

## Zoezi la 3

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tungeni hotuba kuhusu madhara ya uchafuzi wa mazingira kwa kuzingatia sehemu kuu za hotuba pamoja na sifa za hotuba mlizofundishwa hapo awali.*

## 13.5 Sarufi: Viambishi tamati

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, chunguzeni mabadiliko ya silabi za mwisho katika kitenzi 'pika' kinaponyambuliwa katika kauli mbalimbali kisha mjaze nafasi zilizoachwa wazi kwa usahihi na mwelezane ugunduzi wenu.*

| Kauli | Kitenzi 'pika' | Mzizi wa kitenzi | Kiambishi tamati cha mnyambuliko | Kimalizio |
|---|---|---|---|---|
| **Kauli ya kutendea** | pikia | pik' | -i- | -a |
| **Kauli ya kutendewa** | pikiwa | pik' | -iw- | ________ |
| **Kauli ya kutendeka** | pikika | ________ | -ik- | -a |
| **Kauli ya kutendesha** | pikisha | pik' | ________ | -a |
| **Kauli ya kutendwa** | ________ | pik' | -w- | -a |

## Zoezi la 4

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, onyesheni mizizi ya vitenzi vilivyopigiwa mistari katika sentensi zifuatazo kisha mweleze maana inayobebwa na viambishi tamati mbalimbali vinavyojitokeza katika vitenzi hivyo.*

**Kwa mfano:** Mbwa wa jirani *alipigwa* mawe hadi akafa.

**Jibu:** Mzizi wa kitenzi ni ***pig'***

- Kiambishi *'-w-'* ni kiambishi cha mnyambuliko, kauli ya kutendwa
- Kiambishi *'-a'* ni kimalizio

1. Tafadhali usicheze kwenye uwanja huo.
2. Mama alishangazwa na wezi walioiba katika duka la jirani.
3. Kikombe kipya hakijanunuliwa.
4. Viti vingine vinahitajika katika kanisa lao.
5. Nguo aliyonunua bado haijavaliwa.

## Zoezi la 5

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tungeni sentensi kumi sahihi zilizo na vitenzi vyenye viambishi awali pamoja na viambishi tamati.*

**Kwa mfano:** Mama alitugawia njugu. *(a+li+tu+gaw+i+a)*

## Zoezi la 6

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, rejeleeni hotuba mliyosoma hapo awali kuhusu kupigana na umaskini kisha mworodheshe vitenzi kumi vilivyotumika katika hotuba hiyo na mfafanue maana ya viambishi tamati vyao.*

**Kwa mfano:**

***Kutuwezesha:*** Mzizi wa kitenzi ni '*wez*'

- Kiambishi *'-esh-'* ni kiambishi cha mnyambuliko, kauli ya kutendesha
- Kiambishi *'-a'* ni kimalizio

# Somo la 14: Ufupisho


## 14.1 Hotuba kuhusu umuhimu wa maadili

*Katika makundi ya wanafunzi watano watano, tazameni michoro hii kisha msome hotuba kuhusu maadili na mjibu maswali ya ufahamu.*










Wakurugenzi wa shule hii, mwalimu mkuu, naibu wa mwalimu mkuu, wazazi, walimu wenzangu na wanafunzi, hamjambo! Kwanza kabisa ningependa kumshukuru Maulana kwa kutupa uhai na afya nzuri ndiposa tuko hapa siku ya leo. Pili, ningependa kumshukuru mkurugenzi wa shule yetu kwa kunipa nafasi hii ili kutoa hotuba kwa niaba yake kuhusu maadili. Ninawashukuru pia walimu wenzangu ambao wamejitolea mhanga kuwafundisha na kuwaelekeza wanafunzi wetu katika masomo yao. Walimu hawa wamewafaa wanafunzi kwa hali na mali katika elimu yao bila kuwasahau wazazi wetu ambao wamejikaza kisabuni kuhakikisha kuwa wamewalipia watoto wao karo ili kuwawezesha kuendelea na masomo. Naomba nizungumze kuhusu maadili kwa dakika chache zijazo. Mimi ni mwalimu wa somo la Kiswahili katika shule hii.

Mkurugenzi aliiteua mada hii baada ya kukumbana na visa vingi vya utovu wa maadili vinavyowahusu baadhi ya wanafunzi wetu hapa shuleni. Kuna baadhi ya wazazi ambao wamekuwa wakiitwa hapa shuleni mara kwa mara ili kuja kusuluhisha kesi zinazohusu tabia za watoto wao. Leo tungependa kuzungumza kuhusu umuhimu wa kuwa na maadili katika mkutano huu wa walimu, wazazi pamoja na wanafunzi.

Hebu tujiulize, maadili ni nini? Maadili ni mwenendo au tabia njema inayokubalika katika jamii. Baadhi ya maadili yanayokubalika katika jamii ni pamoja na: kuwa na heshima, kuwa mnyenyekevu, kuwa mkweli, kuwa mwaminifu, kuwa na nidhamu, kuwa na bidii, kuwajibika katika shughuli unazopewa, kumcha Mungu, kutumia lugha yenye heshima miongoni mwa mengine.

Wahenga walinena kuwa heshima si utumwa. Kuwa na heshima ni tabia ambayo ni muhimu sana katika maisha ya mtu yeyote, awe mwanafunzi, mzazi au hata mwalimu. Kwa kuwaegemea wanafunzi wetu, nawahimiza mjifundishe na mjizoeshe kuwa na heshima kila wakati, kila mahali na kwa kila mtu. Waheshimuni wazazi wenu, walimu wenu, wakubwa wenu, marika wenu pamoja na wadogo wenu. Heshimu kila mtu unayekumbana naye licha ya jinsia yake au hali yake. Maandiko matakatifu yanatushauri kuwa heshima kwa wazazi wetu huleta baraka tele maishani mwetu. Hapa shuleni, mwanafunzi asiye na heshima kwa walimu, viranja na wanafunzi wenzake huadhibiwa vikali sana. Heshima pia inahusisha lugha unayotumia unapozungumza na wenzako. Wapo wanafunzi wachache ambao hutumia lugha chafu iliyosheheni matusi wanapozungumza na wanafunzi wengine na wakati mwingine wanapozungumza na walimu wao. Ni vyema kila mara unapozungumza na mtu yeyote, mkubwa au mdogo wako, utumie lugha yenye heshima.

Kusema ukweli humfanya mtu kuwa huru kiakili na kimwili. Najua wengi wenu mnajiuliza, 'kuwa huru' kivipi? Mtu aliyesema ukweli hatakuwa na woga wa kugundulika wala kufuatwa, kwa hivyo, yeye atakuwa huru kinyume na mtu aliyesema uongo ambaye ataishi kwa wasiwasi na shauku moyoni kuwa huenda akagundulika au hata akatafutwa na watu aliodanganya. Mwongo hana amani hata kidogo kwa hofu ya kugunduliwa. Nawaomba wanafunzi wetu mjifundishe kusema ukweli kila mara, mkiwa hapa shuleni, nyumbani, sokoni na popote pale. Kuna baadhi ya wanafunzi hapa ambao wametudanganya katika siku zilizopita lakini ukweli ukaja kudhihirika baadaye na wakaishia kupewa adhabu kali sana. Hata kuna wanafunzi wengine ambao walifukuzwa kutoka shuleni kabisa kwa kutosema ukweli ambao uliibua matatizo mengine mengi. Baadhi ya wanafunzi hufuta alama walizotuzwa na mwalimu kwenye karatasi za mitihani yao na kujituza alama za juu kwa udanganyifu. Hii ni tabia mbaya sana tunayotaka ikome kabisa. Mwanafunzi atakayepatikana akijiingiza katika udanganyifu wa aina hii atachukuliwa hatua kali sana.

Ningependa kuangazia suala la kutia bidii katika masomo. Kuna baadhi ya wanafunzi ambao kwa hakika wanafahamu sababu iliyowaleta hapa shuleni ilhali kuna wanafunzi wengine ambao ni wavivu kupindukia. Nataka mfahamu kuwa wazazi hawa wamejitolea kuwalipia karo ili msome na mwasaidie katika siku zao za usoni. Kwa hivyo, malipo wanayotaka kutoka kwenu sasa hivi ni kutia bidii katika masomo yenu. Jizoesheni kuamka mapema, kufanya kazi zote za ziada mnazopewa na mwalimu na kutenga muda wa kibinafsi wa kudurusu mliyofundishwa darasani. Nawaomba nyote muwajibike katika masomo yenu ili mastakimu yenu yawe mazuri.

Kando na kuzungumza kuhusu maadili yanayokubalika katika jamii, ningependa kugusia kidogo kuhusu baadhi ya tabia zisizokubalika katika jamii. Hizi ni kama vile: kuwa mvivu, kuwa na wivu, wizi, ubakaji, kutozingatia usafi, kutumia dawa za kulevya, kutumia lugha chafu iliyojaa matusi, kuwa na kiburi, kuzua vita, unyanyasaji miongoni mwa mengine.

Kujiingiza katika tabia zisizokubalika katika jamii ni jambo ambalo humpotezea mwanafunzi muda wake wa kusoma na kushiriki katika shughuli muhimu za kuyajenga maisha yake. Kama tujuavyo, uvivu ni adui wa maendeleo. Kwa hivyo nawaomba wanafunzi wetu mjiepushe na uvivu. Mtie bidii katika shughuli zenu zote nanyi mtavuna matunda mema katika siku za usoni.

Tabia za wizi, ubakaji na matumizi ya dawa za kulevya zinaweza sio tu kukufanya ukafukuzwa shuleni bali pia unaweza ukafungwa jela. Tumekuwa na visa vichache sana vya tabia hizi na ninafurahi kuripoti leo hapa kuwa wanafunzi waliokuwa wameanza kujiingiza katika tabia hizi wamejirekebisha na kufuata mkondo wa kusoma kwa bidii na kuwa wema. Mwanafunzi yeyote atakayepatikana akiiba, akitumia dawa za kulevya au hata kuwauzia wenzake bila kusita atachukuliwa hatua kali mno na hata kushtakiwa kwa polisi. Pia, tabia za kuzua vita na kuwanyanyasa wanafunzi wengine zimetengewa adhabu kali sana. Nawaomba tujiepushe na tabia kama hizi. Tukiwa hapa shuleni sote tu wanafunzi, hakuna mwanafunzi aliye bora zaidi kuliko wengine kiasi cha kuwataka wanafunzi wengine hasa wa madarasa ya chini kumfulia nguo, kumpigia viatu rangi, kumfanyia kazi zake za ziada pamoja na kumpa pesa zote mnazopewa kwa ajili ya matumizi yenu. Tabia hii ikome kabisa miongoni mwa baadhi ya wanafunzi wachache tuliowaonya wiki jana.

Mwisho, ningependa kuwahimiza wanafunzi kuwa hapa shuleni ndiko unaweza kuujenga msingi mwema wa maisha yako ya kesho na pia unaweza kuyaharibu maisha yako ya kesho. Tieni bidii katika masomo yenu. Wazazi pamoja na walimu wenu tunawaahidi kuwa tutawasaidia na kuwashika mikono hadi mtakapofanikiwa na kufaulu katika elimu yenu. Asanteni kwa kunisikiliza. Maulana awabariki.

## Maswali ya ufahamu

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, someni tena hotuba kuhusu maadili mliyosoma hapo awali kisha mjibu maswali yafuatayo.*

1. Ni watu gani waliohudhuria mkutano huu?
2. Msemaji wa hotuba mliyosoma alikuwa nani?
3. Kwa nini mada hii kuhusu maadili ilichaguliwa na mkurugenzi wa shule?
4. Taja na ueleze maana ya methali moja iliyotumika katika hotuba mliyosoma.

5. Eleza adhabu ambayo mwanafunzi atakayejiingiza katika wizi anaweza kupewa.
6. Eleza maana ya '*Walimu hawa wamewafaa wanafunzi kwa hali na mali*'.
7. Jadili tabia ambazo zinaweza kumpeleka mwanafunzi gerezani.
8. Taja maadili yanayokubalika katika jamii kulingana na hotuba mliyosoma.
9. Kwa nini ni muhimu kwa mwanafunzi kutia bidii katika masomo yake?
10. Jadili tabia zisizokubalika katika jamii kulingana na hotuba mliyosoma.

## 14.2 Msamiati kutokana na hotuba ya umuhimu wa maadili

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, tafuteni msamiati mpya kutoka katika hotuba mliyosoma kuhusu maadili kisha mweleze maana zake. Zingatieni muktadha wa hotuba mliyosoma. Mnaweza kutumia kamusi inapohitajika.*

**Kwa mfano:**

***Maulana*** – jina la kumwitia Mungu

### Zoezi la 1

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, elezeni maana ya msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi zifuatazo kisha mtunge sentensi sahihi kwa kutumia msamiati huo kwa usahihi.*

**Kwa mfano:** *Uvivu* ni adui wa maendeleo ya kila binadamu.

***Maana:*** ***uvivu*** – hali ya kutopenda au kutotaka kufanya kazi

***Sentensi:*** Akimana hakufaulu katika masomo yake kwa sababu ya kuwa na ***uvivu***.

1. Walimu ***wamejitolea mhanga*** kuwafundisha na kuwaelekeza wanafunzi.
2. Wazazi ***wamejikaza kisabuni*** ili kuwalipia watoto wao karo ya shule.
3. ***Utovu*** wa nidhamu ni tabia isiyokubalika katika shule hii.
4. Mwanafunzi huyu amekuwa na ***kesi*** nyingi mwaka huu.
5. Nina ***hofu*** kuwa mwanafunzi huyu hajabadilisha tabia yake.
6. Ninawapenda walimu wangu ***kupindukia*** kwa kazi yao nzuri.
7. ***Elimu*** ndiyo ufunguo wa maisha mazuri ya siku za usoni.
8. Tabia ya ***ubakaji*** ni hatia kali sana.
9. ***Uaminifu*** ni mojawapo ya maadili yanayokubalika katika jamii.
10. Kujiingiza katika ***wizi*** ni tabia inayoweza kumfunga mtu jela.

## 14.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano kuhusu sifa za ufupisho

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, jadilini kuhusu:*

a) Maana ya ufupisho au muhtasari.

b) Sifa za ufupisho au muhtasari.

*Kila kikundi kiwasilishe hoja zake mbele ya wanafunzi wenzao.*

### Maelezo muhimu

Muhtasari wa mambo muhimu katika taarifa fulani huitwa ***ufupisho***.

**Sifa za ufupisho:**

- Huwa mfupi ukilinganishwa na taarifa asilia.
- Huhifadhi ujumbe wa taarifa asilia.
- Huandikwa kwa kuzingatia idadi ya maneno yanayotakikana.
- Viunganishi hutumika ili kupunguza idadi ya maneno.

### Zoezi la 2

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, fupisheni hotuba mliyosoma hapo awali kuhusu maadili kwa kutumia maneno mia moja pekee (100) na kwa kuzingatia sifa za ufupisho mlizofundishwa hapo awali. Kila kikundi kiwasilishe kwa kuwasomea wanafunzi wenzao ufupisho watakaoandika.*

## 14.4 Kusikiliza na kuzungumza: Kufupisha hotuba

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne:*

a) Tungeni hotuba kuhusu '*Umuhimu wa mbuga za wanyamapori nchini Rwanda*'.

b) Fupisheni hotuba mliyotunga kuhusu '*Umuhimu wa mbuga za wanyamapori nchini Rwanda*' kwa kutumia maneno mia moja pekee (100).

*Kila kundi liwasilishe ufupisho wa hotuba yake mbele ya wanafunzi wenzao.*

### Maelezo muhimu

Taratibu za kuandika ufupisho:

1. Soma taarifa uliyopewa kwa mfululizo kuanzia mwanzo hadi mwisho.
2. Soma taarifa hiyo kwa mara ya pili huku ukidondoa hoja muhimu na kuziandika.

3. Chunguza iwapo kuna hoja ambazo zimesahaulika katika taarifa asilia.
4. Unganisha hoja zako kwa kutumia viunganishi mwafaka panapostahili.
5. Soma hoja ulizounganisha kuhakikisha zina mtiririko mzuri.
6. Hariri makala yako ili kuondoa makosa ya kisarufi.
7. Zingatia idadi ya maneno yanayostahili.

## 14.5 Sarufi: Uundaji wa nomino kutokana na vitenzi

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, chunguzeni na mtambue aina za maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi zifuatazo.*

**Kwa mfano:** Mwimbaji aliimba kwa sauti nyororo.

**Jibu:**

- '*Mwimbaji*' ni nomino kwa sababu inaonyesha mtenda
- '*imba*' ni kitenzi kwa sababu kinaonyesha kitendo

1. Mchezaji alicheza mpira wa miguu kwa uhodari.
2. Mlevi huyo alipata ugonjwa wa ini kwa kuzoea kulewa sana.
3. Mvuvi amewakamata samaki wengi kwa sababu alianza kuvua mapema.
4. Mkulima alivuna mazao mengi baada ya kulima na kupanda mashamba mengi.
5. Mrina asali alirina asali nyingi jana usiku.

*Je, mmegundua nini?*

**FAHAMU:** Nomino zinaweza kuundwa kutokana na vitenzi kwa kuongezewa viambishi awali na viambishi tamati.

### Maelezo muhimu

*Kuunda maneno kunahusu uzalishaji wa maneno mapya kutokana na kuambisha mzizi wa neno linaloshughulikiwa kwa kutumia viambishi awali na viambishi tamati. Maneno yanayotumiwa kuunda maneno mengine yanaweza kuwa vitenzi, nomino au vivumishi. Shughuli hii ya kuunda maneno mapya kutokana na maneno mengine huitwa **uambishaji**.*

**Kwa mfano:**

| Kitenzi | Nomino |
|---|---|
| chonga | mchongaji *(m+chonga+ji)* |

| | |
|---|---|
| imba | mwimbaji *(mw+imba+ji)* |
| soma | msomaji *(m+soma+ji)*, msomi *(m+som+i)* |
| shtaki | shtaka *(shtak+a)*, mshtaki *(m+shtak+i)*, mshtakiwa *(m+shtak+iw+a)* |

## Zoezi la 3

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, undeni nomino kutokana na vitenzi vifuatavyo.*

**Kwa mfano:** andika

**Jibu:** mwandishi, maandiko, andiko, kuandika

1. jadili
2. adhibu
3. samehe
4. lima
5. vua
6. andika
7. kunywa
8. kimbia
9. pika
10. chora

## Zoezi la 4

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, undeni nomino moja kutokana na kila kitenzi kifuatacho kisha mtunge sentensi sahihi kwa kila nomino mtakayounda.*

**Kwa mfano:** dhulumu

**Nomino:** dhuluma

**Sentensi:** <u>*Dhuluma*</u> aliyopata kutoka kwa mwajiri wake ilimfanya aache kazi hiyo.

1. okoa
2. hariri
3. okota
4. osha
5. penda

# Somo la 15: Mwongozo wa kuandika ufupisho


## 15.1 Hotuba kuhusu manufaa ya elimu

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tazameni michoro hii kisha msome hotuba ifuatayo kuhusu manufaa ya elimu na baadaye mjibu maswali ya ufahamu.*


A



B



CH



D



Waziri wa elimu, afisa wa elimu wa Mkoa wa Kusini, wasimamizi wa shule mbalimbali, walimu wakuu wa shule mbalimbali, wananchi wazalendo, wanafunzi, mabibi na mabwana, hamjambo! Habari za asubuhi? Ni matumaini yangu kuwa nyote mko salama. Natoa shukrani jazila kwa Rabana kwa kutuwezesha kufika mahali hapa na kwa kutupa uhai na afya njema. Nawashukuru nyote kwa kutenga muda wenu ili kuhudhuria mkutano huu. Mimi ni mmoja wa maafisa wa elimu katika mkoa wa Kusini. Ningependa kuzungumza kwa ufupi kuhusu umuhimu wa elimu kwetu sote pamoja na madhara ya kutoelimika.

Kama tujuavyo, elimu ina manufaa mengi kwa binadamu lakini kabla ya kufafanua umuhimu wa elimu, ningependa tujiulize, elimu ni nini? Elimu ni mafunzo ambayo hutolewa na jamii kwa watu wake, darasani au mahali pasipokuwa darasani. Hii ni kumaanisha kuwa binadamu huweza kupata elimu kutoka kwa watu mbalimbali mahali popote, sio darasani pekee. Kabla ya mfumo wa elimu kuanzishwa katika enzi za mababu zetu, maarifa yalipitishwa kwa watoto kupitia kwa masimulizi yaliyofanywa na nyanya na mababu zetu. Maadili yalipitishwa kupitia kwa masimulizi ya hadithi, vitendawili, misemo na methali mbalimbali. Siku hizi mambo yamebadilika na kuboreka kwani watoto hupata elimu kwa kwenda shuleni na kufundishwa na walimu wao kwa kuzingatia mtaala maalum unaotoka kwa serikali.

Elimu humsaidia mtu kupata uwezo wa kuandika na kusoma. Haya ndiyo maarifa ya kimsingi sana katika kuelimishwa shuleni. Katika ulimwengu wa leo, kila kitu hufanyika kwa kuandika na kusoma kama vile: kusoma taarifa za magazeti, kusoma

vitabu, kusoma maelezo ya bidhaa zinazouzwa madukani, kuweza kuwasiliana na watu, kutumia teknolojia ya kisasa, kuelewa matumizi ya vifaa na vyombo vya nyumbani, kusoma maelezo ya matumizi ya dawa mbalimbali n.k. Ninawahimiza kuwa watoto wote waliofikisha umri wa kusoma waanze kuhudhuria masomo shuleni. Pia, iwapo kuna mtu mzima ambaye anahisi amepitisha umri wa kuwa darasani lakini angependa kujifundisha kusoma na kuandika, asife moyo kwani nina habari njema leo, tumeanzisha mradi unaoitwa '*elimu ya gumbaru'* ambapo tunawafundisha watu wazima elimu ya kimsingi ya kuwawezesha kuandika, kusoma na kuwasiliana na watu wengine pamoja na kuishi kwa ustaarabu.

Umuhimu mwingine wa elimu ni kumwezesha aliyeelimika kupata ajira. Ajira humwezesha mtu kupata mshahara ambao humsaidia kuweza kuyatimiza mahitaji yake ya kimsingi kama vile: kupata chakula, mavazi, elimu na mahali pa kuishi. Elimu huwezesha nchi kupata wataalamu ambao hutekeleza miradi mingi ya kuwafaidi wananchi na nchi kwa jumla. Walioelimika huweza kuwa madaktari, wahandisi, walimu, marubani, makarani, manahodha, viongozi katika serikali, madereva, waashi n.k. Nchi hufaidika kutokana na maarifa ya wafanyakazi walioelimika kwa sababu mapato ya nchi huongezeka. Wananchi huweza kujikimu kimaisha, hupata matibabu, huwa na barabara nzuri za kutumia, hupata elimu n.k.

Elimu husaidia kuboresha shughuli za kibiashara na wafanyabiashara huweza kuendeleza biashara zao kwa urahisi. Hili huifaidi jamii na nchi kwa ujumla. Watu walioelimika huweza kudhibiti miradi mingi na mikubwa pamoja na kuhusisha teknolojia katika shughuli zao. Mtu aliyeelimika anaweza kuiendesha biashara yake vizuri kwa sababu ana maarifa ya namna ya kuepuka kupata hasara na hata kufanya hesabu zake vizuri. Pia, elimu huwawezesha wafanyabiashara kuendesha mitambo au mashine mbalimbali ambazo husadia katika kurahisisha shughuli za biashara.

Umuhimu wa elimu ni mada ambayo inaweza kuzungumziwa bila kumalizika kwa sababu manufaa yake ni mengi sana. Kwa kutaja tu kwa sababu ya wakati, manufaa mengine ya elimu ni kama vile: kuwapa waandishi na watunzi maarifa ya kuweza kuandika tungo za kifasihi kama vile: riwaya, tamthilia, mashairi, hadithi fupi n.k., wakulima huweza kupata maarifa ya kuendesha shughuli zao za ukulima pamoja na ufugaji, uhusiano wetu na watu wa mataifa mengine huboreshwa kwa vile walioelimika huweza hata kuzungumza lugha za mataifa mengine hivyo kupanua mawanda yao ya biashara pamoja na shughuli nyingine kama za matibabu na mashauriano, watangazaji wa habari na maripota huweza kutekeleza kazi yao vizuri miongoni mwa manufaa mengine.

Licha ya manufaa mengi ya elimu, ningependa kuwaeleza tu kwa ufupi kuhusu madhara ya kutoelimika. Kwanza, mtu asiyeelimika hana uwezo wa kusoma na

kuandika. Kwa hivyo, mawasiliano yake na watu wengine hutatizika. Mtu huyu huwa na tatizo kubwa kufahamu yanayoendelea katika jamii yake, nchi yake na mataifa mengine. Mtu asiyeelimika hupata ugumu wa kushiriki katika biashara na kufaulu kwa sababu ya matatizo ya kuwasiliana na wateja na wauzaji bidhaa mbalimbali pamoja na kutodhibiti hesabu zake. Kwa hivyo, mtu wa aina hii husalia nyuma katika maendeleo yake binafsi na ya jamii yake.

Mtu ambaye hajaelimika huwa na ugumu wa kupata ajira hasa ajira zinazohitaji maarifa maalum yanayopatikana tu shuleni. Familia ya mtu huyu hupitia shida nyingi kwa sababu huwa vigumu kuyatimiza mahitaji ya kimsingi. Watu wengi wa aina hii huishia kuwa maskini wa kuombaomba. Kutoweza kuajiriwa huwafanya watu wengine kujiingiza katika uhalifu ili kujipatia riziki ya haraka kama vile kuingilia wizi, uuaji na ujambazi. Wahalifu hawa huwakosesha wananchi amani na kuwa kero kubwa kwa jamii. Wengine hujiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya ili kujisahaulisha shida zao za kukosa pesa. Mtu asiyeelimika pia hana maarifa ya kutumia teknolojia. Yeye hubaki nyuma kimawasiliano na kimaendeleo.

Mwisho, ningependa kuwahimiza nyote mliofika hapa leo kufahamu kuwa elimu ina manufaa tele. Tuhakikishe kuwa watoto wetu pamoja na watoto wote katika jamii na nchi yetu wanapata fursa ya kwenda shuleni. Watu wazima ambao hawakuwahi kukanyaga mlango wa darasa pia wana fursa sasa ya kujiunga na madarasa ya '*elimu ya gumbaru*' ili kuelimika. Kumbukeni kuwa elimu ndio ufunguo wa maendeleo ya mtu binafsi, nchi nzima na pia ulimwengu mzima. Asanteni kwa kunisikiliza. Mungu awabariki.

## Maswali ya ufahamu

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, someni tena hotuba kuhusu manufaa ya elimu mliyosoma hapo juu kisha mjibu maswali yafuatayo.*

1. Taja watu waliohudhuria mkutano huu.
2. Utangulizi wa hotuba mliyosoma unahusu nini?
3. Eleza maana ya '*elimu ya gumbaru*'.
4. Jadili manufaa ya kujua kusoma na kuandika.
5. Eleza manufaa ya elimu katika shughuli za kibiashara.
6. Uhalifu kama vile ujambazi huathiri vipi jamii?
7. Jadili umuhimu wa elimu katika teknolojia.
8. Ajira huwasaidia watu na nchi kwa njia zipi?
9. Jadili madhara ya kutoelimika kwa mtu binafsi na kwa nchi kwa ujumla.
10. Msemaji wa hotuba mliyosoma anahitimisha hotuba yake vipi?

## 15.2 Msamiati wa hotuba kuhusu manufaa ya elimu

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tafuteni msamiati mpya kutoka katika hotuba mliyosoma hapo awali kuhusu manufaa ya elimu kisha mweleze maana zake. Zingatieni matumizi ya msamiati huo katika muktadha wa hotuba mliyosoma. Mnaweza kutumia kamusi inapohitajika.*

**Kwa mfano:**

***afisa:*** mtu mwenye madaraka katika ofisi fulani

### Zoezi la 1

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, elezeni maana ya msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi zifuatazo kisha mtunge sentensi sahihi kwa kutumia msamiati huo kwa usahihi. Mnaweza kutumia kamusi inapohitajika.*

**Kwa mfano:** Waziri wa elimu alimkaribisha rais awahutubie wananchi.

***Maana: waziri*** – afisa aliyepewa jukumu la kusimamia na kuongoza wizara katika serikali

***Sentensi:*** Mjomba wangu amekuwa *waziri* wa elimu tangu mwaka wa 2015.

1. Ningependa kutoa shukrani jazila kwenu nyote.
2. Ninawaombea mema maishani na Rabana awabariki na kuwalinda.
3. Wajukuu wale wanapenda masimulizi ya babu yao.
4. Mwalimu mkuu alituhimiza tusife moyo bali tutie bidii masomoni.
5. Mama anahisi kutapika kutokana na dawa alizokunywa.
6. Mshahara wa mwezi uliopita umeshatumwa kwenye benki.
7. Kaka yangu mkubwa amepata ajira ya kuwa karani mjini Kigali.
8. Wahandisi waliozitengeneza barabara hizi walifanya kazi nzuri.
9. Majumba marefu yaliyo mjini yalijengwa na waashi hawa.
10. Marubani wamegoma kwa sababu ya malipo duni wanayopata.

## 15.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano kuhusu mwongozo wa kuandika ufupisho

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadilini kuhusu mwongozo wa kuandika ufupisho. Kila kikundi kiwasilishe majadiliano yake kwa kuwasomea wanafunzi wenzao.*

**Kwa mfano:** Katika kuandika ufupisho, sentensi fupi fupi huunganishwa kwa kutumia viunganishi mwafaka panapostahili.

### Maelezo muhimu

Taratibu za kuandika ufupisho:

1. Soma taarifa uliyopewa kwa mfululizo kuanzia mwanzo hadi mwisho.
2. Soma taarifa hiyo kwa mara ya pili huku ukidondoa hoja muhimu na kuziandika.
3. Chunguza iwapo kuna hoja ambazo zimesahaulika katika taarifa asilia.
4. Unganisha hoja zako kwa kutumia viunganishi mwafaka panapostahili.
5. Soma hoja ulizounganisha kuhakikisha zina mtiririko mzuri.
6. Hariri makala yako kuondoa makosa ya kisarufi.
7. Zingatia idadi ya maneno yanayostahili.

### Zoezi la 2

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, someni tena hotuba kuhusu manufaa ya elimu kisha muifupishe kwa kutumia maneno mia moja pekee (100). Hakikisheni kuwa mnafuata mwongozo wa kuandika ufupisho mliojadiliana hapo juu. Kila kikundi kiwasilishe kwa kuwasomea wanafunzi wenzao ufupisho wake.*

## 15.3 Kusikiliza na kuzungumza: Kufupisha hotuba

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu:*

a) *Tungeni hotuba kuhusu mada yoyote mtakayochagua katika kundi lenu.*

b) *Fupisheni hotuba mliyobuni kwa kutumia maneno themanini pekee (80).*

*Kila kikundi kiwasilishe mbele ya wanafunzi wenzao hotuba waliyotunga pamoja na ufupisho wake.*

## 15.4 Sarufi: Uundaji wa vitenzi jina

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, chunguzeni maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi zifuatazo kisha mwelezane maneno hayo ni ya aina gani na yameundwa kwa viambishi vipi.*

**Mfano 1:** *Kinywaji* alicholetewa kilikuwa cha bei ghali sana.

**Jibu:** Neno '*kinywaji*' ni nomino ya kawaida iliyoundwa kwa kiambishi awali '*ki-*', kitenzi cha silabi moja '*nywa*' pamoja na kiambishi tamati '*-ji*' = ***ki+nywa+ji***

**Mfano 2:** <u>*Kuimba*</u> kwa moto yule kuliwafurahisha wananchi.

**Jibu:**

Neno '*kuimba*' ni nomino ya kitenzi-jina iliyoundwa kwa kiambishi awali '*ku-*' pamoja na kitenzi '*imba*' = ***ku+imb+a***

1. <u>Kuchora</u> kwa mtoto yule kulimfanya akatuzwa.
2. <u>Kuandika</u> kwa mwanafunzi huyu kulimfurahisha mwalimu.
3. <u>Kulia</u> kwa waombolezaji kuliwasikitisha waliohudhuria mazishi hayo.
4. <u>Kucheza</u> kwa wasichana wale kuliwapendeza watazamaji.

## Maelezo muhimu

Vitenzi vinapoambishwa kiambishi awali '*ku*' huunda nomino zinazoitwa ***vitenzi – jina***.

**Kwa mfano:**

i) ku +la = kula

*<u>Kula</u> kwa mwendawazimu yule kuliwashangaza watu wote.*

ii) ku + hariri +kuhariri

*<u>Kuhariri</u> kwa mhariri yule kulimfanya apandishwe cheo kazini.*

iii) ku + pika

*<u>Kupika</u> kwa mpishi yule kuliwafurahisha wageni waliohudhuria harusi.*

## Zoezi la 3

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tungeni sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia nomino za vitenzi-jina zifuatazo.*

**Kwa mfano:** kusamehe

**Jibu:** <u>*Kusamehe*</u> kwa makosa aliyofanyiwa kulimpa amani moyoni.

1. Kuchonga
2. Kusafisha
3. Kulima
4. Kufuga
5. Kukimbia
6. Kusali
7. Kushona
8. Kutembea
9. Kulala
10. Kula

## Tathmini ya mada ya 3

**Zoezi la 1 la kuandika**

Andika hotuba kuhusu umuhimu wa kudumisha usafi wa mwili na mazingira.

**Zoezi la 1**

*Ambisha vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizo kwenye mabano.*

a) Ungua (kutendesha)
b) Tembea (kutendewa)
ch) Lia (kutendea)

**Zoezi la 2**

*Onyesha mizizi ya vitenzi vifuatavyo.*

a) Alilima
b) Nitakuja
ch) Wameenda
d) Hajatulia
e) Nakuona

**Zoezi la 3**

1. *Unda nomino kutokana na vitenzi vifuatavyo:*
   a) Vua
   b) Panda
   ch) Pika
   d) Tibu
   e) Chunga
2. Tunga sentensi sahihi zenye nomino ulizounda katika swali la 1 hapo juu.

**Zoezi la 2 la kuandika**

Andika hotuba utakayowasomea wanafunzi wenzako katika sherehe ya siku ya wazazi shuleni mwenu.

## Zoezi la 4

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jazeni jedwali lifuatalo kwa usahihi.*

| Kitenzi (kauli ya kutenda) | Kauli ya kutendea | Kauli ya kutendeka | Kauli ya kutendesha | Kuali ya kutendewa |
|---|---|---|---|---|
| shona | shonea | shoneka | shonesha | shonewa |
| andika | ___________ | ___________ | ___________ | ___________ |
| ___________ | onea | ___________ | ___________ | ___________ |
| ___________ | ___________ | pikika | ___________ | ___________ |
| ___________ | ___________ | ___________ | onjesha | ___________ |
| ___________ | ___________ | ___________ | ___________ | tembelewa |

## Zoezi la 5

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, ainisheni vitenzi vilivyopigiwa mistari katika sentensi zifuatazo kwa kueleza maana ya kila kiambsihi husika.*

*Kwa mfano: Mama anapikiwa uji wa mahindi na muhogo.*

*Jibu: a+na+pik+iw+a =*

- *'-a-' ni kiambishi ngeli*
- *'-na-' ni kiambishi cha wakati uliopo*
- *'pik-' ni mzizi wa kitenzi*
- *'-iw-' ni kiambishi cha mnyambuliko*
- *'-a-' ni kiishio*

a) Mtoto amenyweshwa uji baridi.

b) Mbona umemkasirisha mwalimu wa Kiswahili?

ch) Sisi tutapalilia miche tuliyopanda shambani kwetu.

d) Wanafunzi walizuru mbuga ya wanyama ya Akagera.

e) Wanyarwanda wanasherehekea mwaka mpya

## Zoezi la 6

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tungeni sentensi tano sahihi kisarufi katika kauli ya kufanyisha/kutendesha.*

**Kwa mfano**: Mfugaji anawalisha ng'ombe wake.

## Faharasa

| | |
|---|---|
| **adimu:** | ngumu kupatikana |
| **ajira:** | kazi ya kulipwa mshahara |
| **baraza:** | kundi la watu wenye majukumu maalumu |
| **dhahiri shahiri:** | wazi kabisa |
| **elimu ya gumbaru:** | mafundisho ya kimsingi yanayotolewa kwa watu waliopitisha umri wa kuwa shuleni |
| **jinsia:** | hali ya kuwa mke au mume |
| **kiambishi:** | herufi au silabi zinazoongezwa mwanzoni au mwishoni mwa neno (hasa vitenzi) ili kuwakilisha dhana fulani |
| **kujikaza kisabuni:** | kujitahidi |
| **kujitolea mhanga:** | kujitolea kwa hali na mali |
| **manahodha:** | watu wanaoongoza vyombo vya majini kama vile: meli |
| **marubani:** | watu wenye ujuzi wa kuongoza ndege angani |
| **mitaro:** | mifereji mirefu ya kupitisha mabomba ya maji |
| **mkoa:** | eneo la nchi kiutawala ambalo hujumuisha wilaya kadhaa |
| **mshahara:** | malipo anayopata mtu mwishoni mwa mwezi baada ya kufanya kazi fulani |
| **mwito:** | taarifa ya kumtaka mtu aende mahali fulani; mwaliko |
| **riziki:** | kipato |
| **tusife moyo:** | tusikate tamaa |
| **usafi:** | hali ya kuwa nadhifu |
| **utapiamlo:** | maradhi yanayosababishwa na ukosefu wa lishe bora kwa watoto |
| **utovu:** | ukosefu wa |
| **uvivu:** | hali ya kutotaka kufanya kazi |
| **waashi:** | mafundi wa kujenga nyumba kwa mawe au matofali |
| **wahandisi:** | watu wenye elimu na ujuzi wa kuhudumia mitambo, majengo na madaraja |
| **wizi:** | hali ya kuchukua vitu au mali ya mtu bila idhini yake |

# SURA YA NNE

**MADA KUU 4:** **UKUZAJI WA MATUMIZI YA LUGHA KIMAZUNGUMZO**

**MADA NDOGO:** **Midahalo na mijadala**

## Somo la 16: Sifa za mdahalo

### 16.1 Mdahalo kuhusu athari za mavazi ya kisasa

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tazameni picha na mchoro huu kisha msome mdahalo unaofuata kuhusu athari za mavazi ya kisasa katika kuunga mkono tabia za uzinifu nchini na baadaye mjibu maswali ya ufahamu.*







**Mwenyekiti:** Mabibi, mabwana, ndugu wasemaji na wasikilizaji ambao mmefika hapa leo, hamjambo! Nachukua fursa hii kuwakaribisha nyote. Mdahalo wetu wa leo unahusu '***athari za mavazi ya kisasa katika kuunga mkono tabia za uzinifu nchini mwetu'***. Kabla ya kuanza mdahalo wetu, ningependa kuwakumbusha kuwa kila mzungumzaji atapewa muda wa kutoa hoja zake. Vilevile, muda uliopangwa wa kutoa hoja utazingatiwa. Sasa, ningependa kumkaribisha Bagirishya ambaye ndiye msemaji mkuu wa kwanza wa upande wa watetezi ili atoe hoja zake.

**Bagirishya:** Asante sana mwenyekiti. Ni kweli kabisa kuwa mitindo ya mavazi ya kisasa imekuwa kikwazo katika maadili ya wanawake wengi. Hii ni kwa sababu mitindo hii imeathiri namna ambavyo wanawake wanachukulia suala zima la uhuru wa mtu binafsi. Matokeo yake ni kuvunjika kwa miiko na maadili na jamii kudhoofika kiutamaduni.

Yote haya yanatokana na kukubali tamaduni za kigeni na sera zilizo ngeni kutoka kwa mataifa mbalimbali.

Naunga mkono hoja kwamba mavazi ya kisasa yamechangia kwa kiwango kikubwa tabia za uzinifu nchini. Je, nani asiyeona mavazi mafupi yanayovaliwa na wanawake siku hizi ambayo yanaonyesha kila sehemu ya miili yao? Si mapaja yote kuwa wazi, matiti yao kuwa nje na viuno vyao kuwa wazi. Hata kina mama waliokomaa wametekwa na kasumba hii na hawaogopi tena! Kweli, shetani wa mtu ni mtu. Sasa mama wa sampuli hii ataweza vipi kumpa mawaidha binti yake ilhali yeye mwenyewe anashiriki katika mienendo isiyofaa? Tabia hii imechangia kutoweka kwa heshima na maadili kutupiliwa mbali. Wavulana wadogo wanazini na kina mama waliokomaa huku wasichana wadogo wakizini na kina baba waliokomaa. Je, tutaepuka maradhi sugu kama Ukimwi? Asante mwenyekiti.

**Mwenyekiti:** Asante Bwana Bagirishya. Ningependa kumkaribisha msemaji mkuu wa upande wa upinzani Binti Mukamwiza ili naye atoe hoja zake.

**Mukamwiza:** Asante sana mwenyekiti, wasikilizaji na washiriki wa mdahalo huu. Kwa kweli mimi sikubaliani kabisa na maoni ya msemaji ambaye amenitangulia kuwa wanawake wote siku hizi huvalia mavazi mafupi yanayoonyesha miili yao yote. Hata ukiwatazama wanawake walio katika ukumbi huu, ni wangapi waliovalia mavazi yasiyo na heshima? Ni wangapi? Ukitazama vizuri, wanawake walio katika ukumbi huu wamevalia nadhifu. Kwa hivyo, si sahihi kusema kuwa wanawake wote siku hizi wanavalia mavazi yasiyokubalika. Huenda kuna asilimia ndogo sana ya vibiritingoma wachache tu ambao huvalia hivi ili kuendeleza biashara zao za kuuza miili yao kwa pesa, suala ambalo serikali imeahidi kukabiliana nalo. Nawaomba wanaotetea mada hii waache porojo nyingi na wafanye utafiti wao vizuri. Asante mwenyekiti.

**Mwenyekiti:** Kwa sasa, ningependa kumkaribisha mtetezi wa pili ili naye atoe hoja zake. Karibu Mukagatera.

**Mukagatera:** Asante sana mwenyekiti kwa fursa hii. Wakati umefika ambapo serikali inahitaji kupiga marufuku mavazi ya kisasa yanayomwacha mwanamke akitembea uchi. Njia mojawapo ni kusisitiza ununuzi wa mavazi yanayoshonwa nchini na watu kurejelea utamaduni

wao. Hii ndiyo njia pekee ya kurejesha fahari ya jamii zetu. Isitoshe, itapunguza visa vya watu kudhani kwamba urembo na ustaarabu ni kuvaa kama wanawake wa jamii za Ulaya wanavyovaa. Mavazi marefu bado yanaweza kumfanya mwanamke apendeze na kuwa na heshima. Urembo mkubwa ni ule wa kuwa na tabia njema na maadili. Aidha, kumjua Mungu ni njia mwafaka zaidi ya kujua kuvaa.

Mavazi ya kisasa yamechangia katika kuwafanya wasichana wadogo kujiingiza katika maisha ya kushiriki ngono wakiwa wachanga. Wengi wa wasichana hao hudanganyika wanapoelezwa na wanaume kwamba, wao ni warembo kwa kutajiwa sehemu za miili yao zilizoachwa uchi ama kudhihirishwa kwa mavazi waliyovaa. Mengi ya sifa wanazopewa huwa za uongo na hulenga kuibua hisia za uongo ndani ya nafsi zao. Matokeo yake huwa ni ushawishi wa kufanya ngono na hili limechangia uasherati na uzinzi nchini mwetu. Hatutaweza kuepuka ugonjwa wa Ukimwi hali kama hii ikiendelea nchini. Visa vya ubakaji hasa mitaani na mijini vimetokana na uvaaji wa mavazi yasiyo ya heshima. Asante mwenyekiti.

**Mwenyekiti:** Asante sana. Ningependa kumkaribisha msemaji wa pili kutoka upande wa upinzani ili naye atoe hoja zake. Karibu sana Nyiraneza.

**Nyiraneza:** Asante mwenyekiti. Nimezisikiliza kwa makini hoja zilizotolewa na watetezi wa mada hii ila maoni yangu kuhusiana na chanzo cha uasherati na uzinzi ni tofauti. Mtu anayejiheshimu na aliye na maadili mema huweza kuuwajibikia mwili wake mwenyewe pamoja na akili zake. Mwanamume anayependa uasherati anaweza hata kumtongoza mwanamke aliyevalia nguo ndefu kabisa. Kisa na maana, hiyo ni tabia aliyoizoea kwa kukosa maadili. Kwa hivyo, kabla ya kuanza kuwalaumu wanawake na mavazi yao, wanaume wanafaa pia kuzichunguza tabia zao. Kuna wanaume wengi ambao hutumia muda mwingi sana kwenye mtandao wakitazama filamu chafu na picha za wanawake wakiwa uchi. Mwanamume wa aina hii tayari huwa ameshavuruga akili yake na atakachotafuta ni mwanamke yeyote ili amkidhie haja yake. Wavulana pamoja na wanaume waliokomaa, tafadhali muadilike ili kuzuia fikira chafu na potovu zinazowapelekea kujiingiza katika uasherati na uzinzi. Wahenga walisema, mbaazi ukikosa kuzaa husingizia jua. Msitusingizie sisi wanawake. Asante

mwenyekiti.

**Mwenyekiti:** Asante. Wasemaji, wasikilizaji na washiriki wote, naona kuwa watu wengi wangependa kutoa maoni mengine lakini muda hauturuhusu kwa sasa. Naomba tukamilishe mdahalo wetu ila kwa ujumla, ningemalizia kwa kusema kuwa kuiga kila mtindo wa nguo za kisasa kutoka katika nchi za kimagharibi na kupuuza utamaduni wetu ni hatari kwa umma. Sharti tutahadhari sana.

Tutauendeleza mdahalo huu kesho inshallah. Asanteni nyote kwa kushiriki.

## Maswali ya ufahamu

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, someni tena mdahalo kuhusu athari za mavazi ya kisasa katika kuunga mkono tabia za uzinifu nchini kisha mjibu maswali yafuatayo.*

1. Taja na ueleze maana ya methali moja iliyotumika katika mdahalo huu.
2. Unga mkono ama upinge kauli kwamba '*kila mtu ana uhuru wa kuvaa atakavyo*'.
3. Jadili madhara mawili ya mavazi ya kisasa kwa jamii.
4. Eleza maana ya:
   (a) Uzinzi
   (b) Uasherati
5. Kwa maoni yako, serikali ina wajibu gani kuhusiana na mavazi ya kisasa?
6. Eleza madhara ya mavazi ya kisasa kwa wasichana wadogo.
7. Kulingana na mdahalo, suluhisho kwa mavazi ya kisasa ni nini?
8. Kwa maoni yako, uzinifu una suluhisho?
9. Jadili kuhusu mambo mengine yanayoweza kusababisha uasherati na uzinzi kando na mavazi.
10. Eleza maana ya mdahalo.

## 16.2 Msamiati kutokana na mdahalo husika

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tafuteni msamiati mpya kutoka katika mdahalo mliousoma hapo awali kuhusu athari za mavazi ya kisasa katika kuunga mkono tabia za uzinifu nchini kisha mweleze maana zake. Zingatieni muktadha wa mdahalo mliosoma. Mnaweza kutumia kamusi inapohitajika.*

**Kwa mfano:**

***uzinifu*** – tabia ya uasherati au kufanya uzinzi

## Zoezi la 1

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, elezeni maana ya msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi zifuatazo kisha mtunge sentensi sahihi kwa kutumia msamiati huo.*

*Mnaweza kutumia kamusi inapohitajika.*

**Kwa mfano:** Shule yetu iliwakilishwa na *watetezi* watano katika mdahalo huo.

**Maana:** ***watetezi*** - watu wanaounga mkono au wanaokubaliana na suala fulani

**Sentensi:** *Watetezi katika mdahalo huo walikuwa na hoja nyingi.*

1. Shule yetu haijawahi kushiriki katika ***mdahalo***.
2. Tabia ya ***uzinifu*** inafaa kukomeshwa katika kijiji chenu.
3. ***Wapinzani*** walitoa ***hoja*** nyingi kuliko watetezi wa mada hiyo.
4. Kuiga mavazi ya kisasa kumekuwa ***kikwazo*** cha kuhifadhi utamaduni wetu.
5. Sote tunastahili kuwa na ***maadili*** yanayokubalika katika jamii.
6. Hii ni ***sampuli*** ya wanawake ambao hawajali maisha yao.
7. Ugonjwa wa Ukimwi ni miongoni mwa magonjwa ***sugu*** duniani.
8. Kule mjini kuna ***vibiritingoma*** wengi ambao huwasaka wanaume.
9. Tabia ya ***uasherati*** inafaa kukomesha shuleni mwenu.
10. Pamekuwepo na ***ushawishi*** mkubwa kuhusiana na mitindo ya mavazi.

## 16.3 Matumizi ya lugha: Sifa bainifu za mdahalo

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadilini sifa bainifu za mdahalo. Kila kikundi kiwasilishe matokeo yake ya majadiliano mbele ya wanafunzi wenzao.*

**Kwa mfano:** Mdahalo huhusisha majadiliano yenye mitazamo tofauti kati ya watu wengi.

### Maelezo muhimu

- Mazungumzo au majadiliano kati ya watu wengi ambao huzungumzia jambo moja maalumu na huwa na mitazamo tofauti huitwa ***mdahalo***.
    - Mtazamo wa kwanza hutoa hoja zinazotetea au kuunga mkono wazo kuu.
    - Mtazamo wa pili hutoa hoja za kupinga au kukataa wazo kuu.

- Washiriki wa mdahalo huwa: mwenyekiti, katibu, wapinzani, watetezi pamoja na wasikilizaji washiriki.
- Baadhi ya sifa za mdahalo ni: *huwa ni mazungumzo, huhusisha mitazamo miwili, huhusu mada maalum, mada yenyewe huhusu jamii* n.k.

**Zoezi la 2**

*Sikilizeni mdahalo uliorekodiwa katika redio kisha katika makundi ya wanafunzi watatu watatu:*

a) Mjadili sifa za mdahalo huo mliousikiliza darasani.
b) Mweleze mada ya mdahalo huo.
ch) Mjadili hoja zilizotolewa na wapinzani katika mdahalo huo.
d) Mjadili hoja zilizotolewa na watetezi katika mdahalo huo.

## 16.4 Kusikiliza na kuzungumza: Maigizo

*Katika makundi ya wanafunzi watano watano, igizeni mdahalo mliousoma hapo awali kuhusu athari za mavazi ya kisasa katika kuunga mkono tabia za uzinifu nchini. Kila kikundi kiwasilishe maigizo yake mbele ya wanafunzi wenzao.*

## 16.5 Sarufi

### Maana ya nomino

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, chunguzeni maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi zifuatazo kisha mwelezane ugunduzi wenu.*

**Mfano 1:** ***Maji*** *yaliyochotwa jana yameisha.*

**Jibu:** Neno *'maji'* ni nomino ya wingi.

**Mfano 2:** ***Viatu*** *vilivyonunuliwa mwaka uliopita vimeraruka.*

**Jibu:** Neno *'viatu'* ni nomino ya kawaida.

1. Ng'ombe anakula nyasi zizini.
2. Akimana anasoma kitabu cha hadithi ya Kiswahili.
3. Tutaenda kanisani Jumapili ijayo.
4. Kwa nini kitanda chako hakijatandikwa?
5. Kusoma kwa mwanafunzi huyu kunatia moyo.
6. Nguo aliyonunuliwa inapendeza sana.

7. Kikombe cha mtoto kimesafishwa.
8. Maziwa yaliyochemshwa yamenywewa na wageni.
9. Unga uliosagwa jana umemwagika.
10. Duka letu limejaa bidhaa nyingi.

## Maelezo muhimu

Neno linalotaja mtu, kitu, jambo, hali au mahali huitwa ***nomino***.

**Aina za nomino:**

1. Nomino za kawaida. Mifano: *mpira, kalamu, chakula* n.k.
2. Nomino za pekee. Mifano: *Mutoni, Jumapili, Kigali, Kiswahili* n.k.
3. Nomino za dhahania. Mifano: *uvivu, njaa, upendo, amani* n.k.
4. Nomino za jamii. Mifano: *thurea, baraza, tita, umati, bunda* n.k.
5. Nomino za wingi. Mifano: *maji, mafuta, marashi, maziwa* n.k.
6. Nomino za vitenzi-jina. Mifano: *kuimba, kula, kucheza, kuandika* n.k.

## Zoezi la 3

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tajeni aina za nomino mnazozifahamu kisha mtoe mifano miwili miwili ya nomino kwa kila aina.*

**Kwa mfano:** Nomino za pekee

**Mifano:** Jumapili (*jina la siku*), Kalisa (*jina la mtu*)

## Zoezi la 4

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tungeni sentensi mbili mbili sahihi kwa kutumia:*

a) Nomino dhahania
b) Nomino za wingi

**Kwa mfano:**

a) ***Wema*** wake umewafanya watu kumpenda sana. (*'wema' ni nomino dhahania*)
b) ***Mafuta*** waliyonunua yalikuwa yameharibika. (*'mafuta' ni nomino ya wingi*)

## 16.5.1 Uundaji wa nomino

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jaribuni kuunda nomino kwa kutumia maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi zinazofuata kisha mtunge sentensi sahihi kwa kutumia nomino mtakazounda.*

**Mfano 1:** Mwalimu mkuu alim<u>*samehe*</u> mwanafunzi aliyekuwa amechelewa.

***Jibu:*** Kutokana na kitenzi '*samehe*' tunaweza kuunda nomino '*msamaha*' na '*kusamehe*'.

***Mfano wa sentensi*:** i) Binadamu wote walipata <u>*msamaha*</u> wa Mungu.

ii) <u>*Kusamehe*</u> kwa makosa yake kumempa amani moyoni.

**Mfano 2:** Msichana <u>*mrembo*</u> amefika ofisini mwake.

***Jibu:*** Kutokana na kivumishi '*mrembo*' tunaweza kuunda nomino '*urembo*'.

***Mfano wa sentensi*:** <u>*Urembo*</u> wa malkia yule unapendeza.

**Mfano 3:** <u>*Mchoraji*</u> wa nyumba ile alituzwa jana.

***Jibu:*** Kutokana na nomino '*mchoraji*' tunaweza kuunda nomino '*mchoro*'.

***Mfano wa sentensi*:** <u>*Mchoro*</u> wa nyumba ile ulipendeza sana.

1. Muumini ali<u>*tubu*</u> dhambi zake kwa padri wao.
2. Wanafunzi wana<u>*jadili*</u> sababu za kuwafanya wasipite mitihani yao.
3. Mwizi alini<u>*tisha*</u> baada ya kumfumania akiiba.
4. Kaka yangu ndiye <u>*mrithi*</u> wa mali ya baba yangu.
5. Ukuta <u>*mrefu*</u> umebomoka.

## Maelezo muhimu

Uzalishaji wa maneno mapya kutokana na mizizi ya maneno mengine huitwa ***uundaji wa maneno***.

Nomino zinaweza kuundwa kutokana na mizizi ya vitenzi, vivumishi na nomino nyingine.

**Kwa mfano:**

| | | |
|---|---|---|
| i) | **Kitenzi** | **Nomino** |
| | Imba | wimbo, mwimbaji, kuimba |
| ii) | **Kivumishi** | **Nomino** |
| | Mrefu | urefu |
| iii) | **Nomino** | **Nomino** |
| | mtu | utu, jitu, kitu |

**FAHAMU:** Nomino huundwa kutokana na maneno mengine kwa kuongeza viambishi awali au viambishi tamati kwenye mzizi wa neno linalounda.

## Zoezi la 5

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, undeni nomino kutokana na maneno yafuatayo kisha mtunge sentensi sahihi kwa kutumia nomino mtakazounda.*

**Kwa mfano:** -safi

**Jibu:** *Usafi* wa hospitali ile uliwapatia tuzo kubwa.


1. -erevu
2. fagia
3. chora
4. -baya
5. upendo


# Somo la 17: Mwongozo wa kuandika mdahalo

## 17.1 Mdahalo kuhusu athari za rushwa

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tazameni michoro hii kisha msome mdahalo unaofuata kuhusu athari za rushwa kwa Wanyarwanda kisha mjibu maswali ya ufahamu.*




**Mwenyekiti:** Mabibi na mabwana mliofika hapa leo hamjambo! Karibuni katika mdahalo wa leo. Mada ya mdahalo wa leo ni kuhusu athari za rushwa kwa Wanyarwanda. Bila kupoteza muda ningependa kumkaribisha Kawera kutoka upande wa watetezi ili atoe hoja zake kuhusiana na mada ya leo.

**Kawera:** Asante mwenyekiti. Rushwa pia huitwa *hongo, chai* au *kitu kidogo*. Rushwa ni chanzo cha uovu katika mataifa mengi duniani. Mara nyingi wananchi huwachagua viongozi wasio waadilifu kwa sababu ya kupewa hongo. Hongo hutolewa kwa njia nyingi. Wakati mwingine hutolewa kwa njia ya ahadi za kupewa masomo ya bure, kazi ama nafasi za mamlaka katika ubalozi na kampuni za nchi za kigeni ama kampuni za kibinafsi na asasi za kibinafsi. Ahadi hizi hutoa vishawishi vikubwa kwa wananchi hasa maskini ambao huishia kuwachagua viongozi wasiofaa na ambao lengo lao ni kupora hazina ya umma na kuhodhi mali. Matokeo ya vitendo vyao ni kurudisha maendeleo ya taifa nyuma. Pesa ambazo zingetumiwa kujenga shule, hospitali na barabara huishia kwenye mifuko ya watu wenye ubinafsi. Asante mwenyekiti.

**Mwenyekiti:** Asante Kawera kwa hoja zako. Ningependa kumkaribisha

Bagirimana kutoka upande wa upinzani ili naye atoe hoja zake. Karibu sana.

**Bagirimana:** Asante mwenyekiti. Kwa kusema kweli, suala hili la rushwa halijakita mizizi katika nchi yetu kama inavyosawiriwa na watetezi wa mada ya mdahalo wa leo. Kulingana na takwimu nilizo nazo, nchi yetu imeorodheshwa miongoni mwa baadhi ya nchi zilizo na visa vichache mno vya ufisadi. Serikali yetu imejitahidi juu chini kupigana na donda hili sugu la ufisadi. Watangazaji habari pamoja na vyombo vya dola vyenye majukumu ya kudhibiti rushwa nchini vimeripoti kwamba kuna watu wachache ambao bado wanaomba rushwa katika kutoa huduma kwa wananchi. Kamera nyingi zimewekwa katika ofisi za umma ili kuweza kunasa matukio yoyote ya ufisadi. Wafanyakazi na viongozi katika vitengo mbalimbali wameweza kuelimishwa kuhusu athari za ufisadi pamoja na adhabu anayoweza kupata mtu yeyote atakayejiingiza katika shughuli za kiufisadi. Kwa kweli ufisadi umepungua nchini kwa kiwango kikubwa sana. Asante mwenyekiti.

**Mwenyekiti:** Asante sana Bagirimana kwa hoja zako. Sasa tumkaribishe Mukandayisenga kutoka upande wa watetezi ili naye atueleze maoni yake. Karibu.

**Mukandayisenga:** Asante mwenyekiti. Kwa maoni yangu, suala la rushwa bado lipo katika nchi yetu hasa katika afisi kadhaa ambazo hutoa huduma mbalimbali kwa wananchi. Rushwa huathiri namna huduma mbalimbali zinavyotolewa katika afisi za umma. Kucheleweshwa kupewa huduma ama kukosa hata kuipata kunatokana na watu fisadi ambao huweka matumbo yao mbele. Wanyarwanda wanastahili kuungana na kupigana na uovu huu. Kama tujuavyo, elimu hutolewa bure. Mahakama ya jadi hasa katika ngazi za kata na tarafa huamua kesi bila matatizo yoyote. Rushwa ni adui wa taifa letu na sharti tupigane naye. Tusipofanya hivyo, watu wanaostahili kupata kazi na kujenga taifa letu watakosa ajira. Wengi ambao ni vijana wataingilia uhalifu ambao utaiathiri jamii vikali sana. Asante mwenyekiti.

**Mwenyekiti:** Nakushukuru sana Mukandayisenga kwa mchango wako. Sasa namkaribisha Birasa ambaye atakuwa msemaji wa mwisho kutoka upande wa wapinzani ili naye atoe hoja zake. Karibu ndugu.

**Birasa:** Asante mwenyekiti. Hivi majuzi tumekuwa na kampeni kwenye redio na runinga kuhusu suala hili la ufisadi ambapo tuliwaomba wananchi wawe huru kuripoti visa vyovyote vya ufisadi. Katika tangazo hilo, tulitoa nambari kadhaa za simu pamoja na anwani kadhaa za baruapepe ambazo wananchi wanaweza kutumia kuripoti visa vya aina hii wakati wowote vinapotokea. Kwa kusema ukweli, suala la ufisadi ni jukumu la kila mwananchi kwa sababu wananchi ndio wanaokubali kutoa rushwa ili kupata huduma ambazo serikali inawalipa wafanyakazi wake ili kuwahudumia wananchi wote. Asante mwenyekiti.

**Mwenyekiti:** Asanteni sana wasemaji, wasikilizaji na washiriki wote. Naona kuwa watu wengi wangependa kutoa maoni zaidi kuhusiana na mada ya leo lakini kwa sasa muda hauturuhusu. Naomba tukamilishe mdahalo wetu kwa leo. Tutauendeleza kesho inshallah. Asanteni nyote kwa kushiriki.

## Maswali ya ufahamu

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, someni tena mdahalo kuhusu athari za rushwa kwa Wanyarwanda kisha mjibu maswali yafuatayo.*

1. Taja washiriki katika mdahalo mliosoma.
2. Jadili madhara ya ufisadi kwa wananchi na nchi.
3. Kwa nini wananchi huwachagua viongozi wasio waadilifu?
4. Eleza sababu ambazo huwafanya wananchi kutoa hongo.
5. Serikali imeweka mikakati ipi ili kukabiliana na visa vya ufisadi?
6. Jadili hoja walizotoa wapinzani katika mdahalo mliosoma.
7. Eleza maana ya '*ufisadi umekita mizizi*'.
8. Taja visawe vya neno '*rushwa*'.
9. Wananchi wanaweza kuchangia vipi katika kukomesha ufisadi nchini?
10. Je, umewahi kujipata katika hali iliyokuhitaji utoe hongo? Eleza.

## 17.2 Msamiati kutokana na mdahalo husika

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tafuteni msamiati mpya kutoka katika mdahalo mliosoma hapo awali kuhusu athari za rushwa kwa Wanyarwanda kisha mweleze maana zake. Zingatieni muktadha wa mdahalo huo. Mnaweza kutumia kamusi inapohitajika.*

**Kwa mfano:**

***rushwa*** – fedha au kitu chochote anachopewa mtu mwenye uwezo au madaraka ili amfanyie mtoaji hisani au upendeleo fulani

### Zoezi la 1

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, elezeni maana ya msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi zifuatazo kisha mtunge sentensi sahihi kwa kutumia msamiati huo kama ulivyotumika katika mdahalo mliosoma kuhusu athari za rushwa kwa Wanyarwanda.*

**Kwa mfano:** Tutajadiliana kuhusu *mada* nyingine katika mdahalo ujao.

**Maana:** ***mada*** – kiini cha jambo ambalo linazungumziwa au kujadiliwa

***Matumizi katika sentensi:*** Mwalimu aliteua ***mada*** ya mdahalo wa kesho.

1. Polisi walipewa ***hongo*** ili kuliachilia gari lililokuwa limehusika katika ajali.
2. Wananchi wanafaa kuwachagua viongozi ***waadilifu***.
3. Viongozi fisadi humaliza pesa kutoka katika ***hazina*** ya umma.
4. Watu wenye madaraka ***huwapora*** maskini ili kuwahudumia.
5. ***Ubinafsi*** husababisha visa vya ufisadi kuongezeka.
6. ***Takwimu*** zinaonyesha kuwa visa vya ufisadi nchini vimepungua sana.
7. ***Ufisadi*** umekuwa donda sugu nchini Kenya.
8. Serikali imeweka ***mikakati*** ya kukomesha ufisadi.
9. ***Asasi*** nyingi za kibinafsi zimejengwa nchini.
10. Viongozi fisadi ***huhodhi*** mali inayofaa kuwasaidia wananchi.

## 17.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadilini kuhusu mwongozo wa kutunga mdahalo kwa kuzingatia mambo muhimu yanayofaa kuwepo kwa kurejelea mifano ya midahalo mliyosoma hapo awali. Kila kikundi kiwasilishe matokeo yake ya majadiliano mbele ya wanafunzi wenzao.*

**Kwa mfano:** Sharti mdahalo uhusishe pande mbili zenye mitazamo miwili.

## 17.4 Kusikiliza na kuzungumza: Kutunga mdahalo

*Katika makundi ya wanafunzi watano watano, tungeni mdahalo kuhusu unyanyasaji wa kijinsia. Kila kundi liwasilishe mdahalo wake mbele ya wanafunzi wenzao.*

### Zoezi la 2

*Katika makundi ya wanafunzi sita sita, igizeni mdahalo mliosoma hapo awali kuhusu athari za rushwa kwa Wanyarwanda kwa kuzingatia sehemu kuu za mdahalo. Kila kundi liwasilishe maigizo yake mbele ya wanafunzi wenzao.*

## 17.5 Sarufi

### Maana ya kivumishi

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, jaribuni kueleza sifa za mwanafunzi mwenzako kama vile anavyoonekana au sifa za vitu vya mwenzako. Kwa mfano: kuwa mrefu, kuwa mwembamba, kuwa mnene, kuwa na macho mazuri, kuwa na ngozi nyororo, kuwa na vitabu vingi, kuwa na mkoba mpya, kuwa na viatu vyeusi n.k. Kila kikundi kitunge sentensi sahihi ili kueleza maelezo yao.*

**Kwa mfano:**

1. Mwanafunzi <u>mrefu</u> ameketi chini. (*'mrefu' ni kivumishi cha sifa ya nomino 'mwanafunzi'*)
2. Mkoba <u>mpya</u> ni wa Akimana. (*'mpya' ni kivumishi cha sifa ya nomino 'mkoba'*)
3. Viatu <u>vyeusi</u> vimevaliwa na Kalisa. (*'vyeusi' ni kivumishi cha sifa ya nomino 'viatu'*)
4. Yeye ni <u>mzuri</u>. (*'mzuri' ni kivumishi cha sifa ya kiwakilishi cha nomino 'yeye'*)
5. Nyabineza ana ngozi <u>nyororo</u> inayopendeza. (*'nyororo' ni kivumishi cha sifa ya nomino 'ngozi'*)

*Je, mmegundua nini?*

## Maelezo muhimu

Neno linaloeleza zaidi kuhusu nomino au kiwakilishi chake huitwa ***kivumishi***.

**Aina za vivumishi:**

1. Vivumishi vya sifa. Mifano: *-zuri, -ekundu, -baya, -refu* n.k.
2. Vivumishi vionyeshi/viashiria. Mifano: *huyu, huyo, hiki, lile, hapo* n.k.
3. Vivumishi vimilikishi. Mifano: *wangu, chako, lake, petu, zako* n.k.
4. Vivumishi vya idadi. Mifano: *wawili, vichache, kumi, wengi* n.k.
5. Vivumishi viulizi. Mifano: *gani, ngapi, yupi, upi* n.k.
6. Vivumishi vya pekee. Mifano: *-enyewe, -enye, -ingine, -ote* n.k.

## Zoezi la 3

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tajeni aina za vivumishi mnazofahamu kisha mtoe mifano miwili miwili ya vivumishi kwa kila aina.*

**Kwa mfano:** Vivumishi vya sifa

**Mifano:**

- Paka *mkubwa* amefugwa kwetu. (‘*mkubwa’ ni kivumishi cha sifa*)
- Msichana mrembo ameimba vizuri. (‘*mrembo’ ni kivumishi cha sifa*)

## Zoezi la utafiti

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, fanyeni utafiti kuhusu:*

a) Vivumishi visisitizi

b) Vivumishi vya nomino

ch) Vivumishi virejeshi

*Toeni mifano katika sentensi kwa kila aina ya vivumishi mtakavyoshughulikia hapo juu.*

**Kwa mfano:**

a) Mtoto ***huyu huyu*** atanunuliwa viatu vingine.

Maneno ‘huyu huyu’ yanasisitiza kuhusu nomino ‘*mtoto*’.

b) Mlinda ***lango*** ameajiriwa kazi.

Neno ‘lango’ ni nomino lakini katika sentensi hii ni ‘kivumishi’ kwa sababu linaeleza kuhusu nomino ‘*mlinda*’.

ch) Kiti ***ambacho*** kimenunuliwa ni cha babu.

Neno ‘ambacho’ linatumika kurejelea nomino ‘*kiti*’.

## Zoezi la makundi

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, husisheni kwa usahihi mchoro na picha zifuatazo na sentensi sahihi kutoka kwa zile ulizopewa hapo chini.*

A



1. Kondoo ***mnono*** atauzwa sokoni kesho.

B



2. Baba amenunua gari ***zuri*** sana.

CH



3. Viatu ***vyeusi*** vilivyonunuliwa ni vya dada yangu mdogo.

D



4. Uzi ***mwekundu*** umenunuliwa na fundi.

E



5. Mwanafunzi ***mrefu*** anazungumza na rafiki yake.

## 17.5.1 Uundaji wa vivumishi

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, jaribuni kuunda vivumishi kwa kutumia maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi zinazofuata kisha mtunge sentensi sahihi kwa kutumia vivumishi utakavyounda.*

**Mfano 1:** Mwanasiasa yule anapendwa kwa *ucheshi* wake.

***Jibu:*** Kutokana na nomino '*ucheshi*' tunaweza kuunda kivumishi '*mcheshi*'.

***Mfano wa sentensi***: Mwanasiasa *mcheshi* anapendwa sana.

**Mfano 2:** Kiongozi huyu alini*saliti* kwa wazazi wangu.

***Jibu:*** Kutokana na kitenzi '*saliti*' tunaweza kuunda kivumishi '*msaliti*'.

***Mfano wa sentensi***: Kiongozi *msaliti* alinishtaki kwa wazazi wangu.

1. Mama alii*remba* nyumba kwa ajili ya kuwapokea wageni.
2. *Urefu* wa jumba hili unaogopesha.

3. Kwa nini mtoto wako ana*lia*?
4. *Uchafu* wa chumba kile umekifanya hakikaliki.
5. *Ubaya* wako umekupotezea kazi.

## Maelezo muhimu

Vivumishi vinaweza kuundwa kutokana na mizizi ya vitenzi na nomino.

**Kwa mfano:**

| | | |
|---|---|---|
| i) | **Kitenzi** | **Kivumishi** |
| | tukuka | mtukufu |
| ii) | **Nomino** | **Kivumishi** |
| | Ukubwa | mkubwa, kikubwa, kubwa n.k. |

**FAHAMU:** Kivumishi huundwa kutokana na maneno mengine kwa kuongeza viambishi awali au viambishi tamati kwenye mzizi wa neno husika.

## Zoezi la 4

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, undeni vivumishi kutokana na maneno yafuatayo kisha mtunge sentensi sahihi kwa kutumia vivumishi mtakavyounda.*

**Kwa mfano:** usafi

**Jibu:** Nguo *safi* zimepigwa pasi.

1. werevu
2. cheka
3. wembamba
4. unene
5. udogo


# Somo la 18: Mjadala

## 18.1 Mjadala kuhusu umuhimu wa uzalendo

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, tazameni picha na mchoro huu kisha msome mjadala unaofuata kuhusu umuhimu wa uzalendo kwa Wanyarwanda na baadaye mjibu maswali ya ufahamu.*

A






**Mwenyekiti:** Wananchi watukufu, mabibi na mabwana mliofika hapa leo hamjambo! Nachukua fursa hii kuwakaribisha nyote katika mjadala wa leo. Mada ya mjadala wa leo ni umuhimu wa uzalendo kwa Wanyarwanda. Nyinyi nyote mnafahamu kuwa Rwanda ni nchi yetu na hivyo hatuna budi kuipenda na kuitunza. Bila kupoteza muda ningependa kumkaribisha Uwase ili atoe hoja zake kuhusu mada ya leo. Karibu.

**Uwase:** Asante mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii. Mimi ningependa kutanguliza kwa kueleza kuwa uzalendo ni hali au fikira ya mtu kuipenda nchi yake kwa dhati. Uzalendo ni nguzo ya mshikamano wa kitaifa na umoja wa wananchi. Kuishi pamoja kama Wanyarwanda ni muhimu. Maendeleo katika pembe za taifa letu yanaweza kuafikiwa bila kubaguana wala kuchukiana. Tukiwa na uzalendo, biashara baina ya jamii mbalimbali zitafaulu na watu wataweza kupata faida kubwa ya jasho lao. Isitoshe, watu wataishi bila hofu ya kushambuliana ama uhalifu kutokea. Asante mwenyekiti.

**Mwenyekiti:** Asante sana Uwase kwa mawazo yako. Ningependa kumkaribisha Birasa naye atoe maoni yake kuhusiana na umuhimu wa uzalendo. Karibu.

**Birasa:** Asante sana Mwenyekiti. Kwa kweli, uzalendo ni kujali nchi yako, kuipenda, kuitetea na kuistawisha. Ndiposa suala la kupiga kura ni muhimu kwa kila Mnyarwanda ili kuhakikisha ya kwamba nchi yetu inatawaliwa na viongozi waadilifu. Faida za uongozi bora ni nyingi zikiwemo kuwa na amani, maendeleo, umoja wa nchi, kukua kwa uchumi na ustawi katika elimu na miundo msingi. Wanyarwanda wenzangu, tunafahamu kuwa uhalifu wa kimataifa ni suala ambalo linatishia usalama wa nchi na ulimwengu mzima. Je, haya yanahusiana vipi na uzalendo wetu? Wajibu wa kwanza wa Mnyarwanda ni kulinda mipaka ya nchi yake. Raia ana wajibu wa kuripoti wahalifu na washirika wao na kuepukana na vishawishi vya makundi ya kigaidi kama vile '*Al shabaab', 'Isis'* na mengine. Mahali popote panapolipuliwa kwa bomu ni Mnyarwanda anayepoteza mali na maisha yake. Kwa hivyo, kila mmoja akiwajibika vilivyo, tutaishi kwa amani. Asante mwenyekiti.

**Mwenyekiti:** Asante Birasa kwa maoni yako. Tumkaribishe Mukagatera.

**Mukagatera:** Asante mwenyekiti kwa nafasi hii. Nawaunga mkono wenzangu walionitangulia kuzungumza kuhusu umuhimu wa uzalendo wetu. Ningependa kutoa hoja kwamba uzalendo ni kufanya kazi kwa bidii ili kuistawisha nchi yetu na kuepuka tabia zinazokiuka maadili kama vile: rushwa na ufisadi. Wanaopora mali ya nchi yao sio wazalendo. Wizi wa mali ya umma husababisha uchumi kuzorota, miundo msingi kukosekana na ile iliyopo kudhoofika na kufanya gharama ya bidhaa muhimu kuwa ghali. Nadhani mnajua matokeo yake! Umaskini, maradhi na njaa huwaandama wananchi. Watu wenye njaa, maradhi na umaskini hawawezi kuwa na ari na nguvu ya kujenga taifa lao. Kwa hivyo, uzalendo ni muhimu kwetu sote. Asante mwenyekiti.

**Mwenyekiti:** Asante sana Mukagatera kwa maoni yako. Naomba nimkaribishe Mutoni ambaye atakuwa msemaji wa mwisho katika mjadala wetu wa leo. Karibu dada.

**Mutoni:** Asante mwenyekiti kwa fursa hii. Wakati mwingi mtu akizungumza baada ya wasemaji wengine huwa hana mengi ya kusema kwa sababu waliomtangulia huwa wameshasema yote. Ningependa kuongezea kwa kusema kuwa uzalendo ni njia ya kuhakikisha kwamba maadili tunayowapa watoto wetu nyumbani na shuleni yanaambatana na umoja wetu, utamaduni na utu wetu kama Wanayarwanda. Watoto wetu wafundishwe wimbo wa taifa letu,

mila na tamaduni zetu, ushirikiano, kula pamoja na kuheshimu wazee. Wimbo wa taifa letu utawafanya watoto wetu kuipenda nchi yetu, kuthamini uhuru wa nchi yao, historia yao na kutetea umoja wa nchi yao. Kama tunavyofahamu, watoto ndio raia na viongozi wa kesho. Asante mwenyekiti.

**Mwenyekiti:** Asanteni sana kwa mchango wenu kuhusiana na mada ya mjadala wa leo. Ni dhahiri shahiri kuwa uzalendo ni muhimu sana kwa Wanyarwanda kwa sababu ndio unaoweza kuwaleta pamoja na kuleta maendeleo katika nchi hii. Tukipata muda mwingine tutauendeleza mjadala huu. Asanteni.

## Maswali ya ufahamu

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, someni tena mjadala kuhusu umuhimu wa uzalendo kwa Wanyarwanda kisha mjibu maswali yafuatayo.*

1. Eleza maana ya uzalendo kulingana na mjadala mliosoma.
2. Kwa nini suala la kupiga kura huonyesha uzalendo?
3. Jadili mambo yoyote matatu yanayoonyesha kwamba mtu ni mzalendo.
4. Kutokana na mjadala mliosoma, uzalendo unachangia vipi kwa usalama wa nchi?
5. Eleza umuhimu wa uzalendo kwa Mnyarwanda.
6. Eleza namna mtoto Mnyarwanda anaweza kufundishwa uzalendo.
7. Bila shaka ukosefu wa uzalendo una madhara kwa taifa. Je, Wanyarwanda wanaweza kuathirika vipi iwapo uzalendo utakosekana?
8. Viongozi wana wajibu gani katika kuwahamasisha watoto kuhusu uzalendo wa nchi yao?
9. Eleza umuhimu wa wimbo wa taifa kwa uzalendo wa vizazi vichanga.
10. Je, unaufahamu wimbo wa taifa wa nchi ya Rwanda? Imbeni kwa pamoja.

## 18.2 Msamiati kutokana na mjadala husika

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, tafuteni msamiati mpya kutoka katika mjadala mliousoma hapo awali kuhusu umuhimu wa uzalendo kwa Wanyarwanda kisha mweleze maana zake. Zingatieni muktadha wa mjadala huo. Mnaweza kutumia kamusi inapohitajika.*

**Kwa mfano:**

**Uzalendo** – hali ya mtu kuipenda nchi yake kwa dhati

## Zoezi la 1

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, elezeni maana ya msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi zifuatazo kisha mtunge sentensi sahihi kwa kutumia msamiati huo kama ulivyotumika katika mjadala mliosoma kuhusu umuhimu wa uzalendo kwa Wanyarwanda.*

**Kwa mfano:** Wananchi walishiriki katika *mjadala* huo.

**Maana:** ***mjadala*** – mazungumzo yanayohusu mada mahususi ambayo hufanywa kwa kujenga hoja

***Matumizi katika sentensi:*** Mwenyekiti aliongoza ***mjadala*** wetu vizuri.

1. Uchumi wa nchi yetu ***umeimarika***.
2. Wanyarwanda wana ***ari*** ya kufanya bidii katika shughuli zao ili wajiimarishe.
3. Kila binadamu anastahili kuwa na ***utu*** kwa wenzake.
4. ***Bomu*** lililotupwa kwenye hoteli ile halikulipuka.
5. ***Mshikamano*** wa Wanyarwanda ni ishara ya uzalendo wao.
6. ***Uhalifu*** una madhara mengi kwa mtu binafsi na nchi.
7. Polisi wanaombwa kudumisha ***usalama*** katika mipaka yetu.
8. Ni ***dhahiri shahiri*** kuwa uzalendo ni muhimu kwetu.
9. Viongozi wanaoshiriki katika ***ufisadi*** huzorotesha uchumi wa nchi yetu.
10. Serikali itahakikisha kuwa ***miundo msingi*** imestawishwa.

## 18.3 Matumizi ya lugha: Sifa bainifu za mjadala

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, jadilini sifa bainifu za mjadala. Kila kikundi kiwasilishe matokeo ya majadiliano yao mbele ya wanafunzi wenzao.*

**Kwa mfano:** Mjadala huhusisha mazungumzo yenye kujenga hoja kwa mtazamo mmoja.

### Maelezo muhimu

- Mazungumzo kati ya watu wengi ambao huzungumzia jambo moja maalumu na huwa na mtazamo mmoja huitwa ***mjadala***.
- Washiriki wa mjadala huwa: *mwenyekiti, katibu, wapinzani, watetezi pamoja* na *wasikilizaji washiriki.*
- Baadhi ya sifa za mjadala ni: *kuwepo kwa mazungumzo; huhusisha mtazamo mmoja; huhusu mada maalum, mada yenyewe huhusu jamii* n.k.

## Zoezi la 2

*Sikilizeni mjadala uliorekodiwa katika redio kisha katika makundi ya wanafunzi wanne wanne:*

a) Mjadili sifa za mjadala huo mliousikiliza darasani.

b) Mweleze mada ya mjadala huo.

ch) Mjadili hoja zilizotolewa katika mjadala huo.

## 18.4 Kusikiliza na kuzungumza: Maigizo

*Katika makundi ya wanafunzi sita sita, igizeni mjadala mliousoma hapo awali kuhusu umuhimu wa uzalendo kwa Wanyarwanda. Kila kikundi kiwasilishe maigizo yake mbele ya wanafunzi wenzao.*

## 18.5 Sarufi

### Maana ya kitenzi

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, chunguzeni na mweleze maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi zifuatazo ni ya aina gani.*

**Mfano 1:** *Mwalimu ana**fundisha** wanafunzi wa kidato cha sita.*

**Jibu:** Neno '*fundisha*' ni kitenzi kwa sababu kinaeleza kuhusu utoaji wa mafundisho.

**Mfano 2:** *Mama **alikuwa anapika** chai wageni walipoingia.*

**Jibu:** Neno '*alikuwa*' ni kitenzi kisaidizi cha kitenzi kikuu '*anapika*'.

1. Mchezaji anacheza mpira wa miguu uwanjani.
2. Wanafunzi wamekwisha kula chakula chao cha mchana.
3. Mama angali analala chumbani mwake.
4. Neza amewahi kupata zawadi katika somo hili.
5. Polisi waliweza kujua ukweli wa kesi hiyo.
6. Mimi ni mgonjwa.
7. Hiki ndicho kiti cha babu yetu.
8. Mimi sikumruhusu akirarue kitabu cha mwalimu.
9. Tulitahiniwa, tukarudishiwa karatasi zetu na tukapongezwa.
10. Mwanafunzi aliamka, akaoga, akanywa kiamshakinywa na kwenda shuleni.

## Maelezo muhimu

Neno ambalo hueleza kuhusu kinachofanywa, kilichofanywa au kitakachofanywa huitwa ***kitenzi***.

**Aina za vitenzi**

1. ***Vitenzi halisi:*** Huchukua viambishi awali na viambishi tamati na hujisimamia vyenyewe. Mifano: anawahudumia, amefukuzwa n.k.
2. ***Vitenzi visaidizi:*** Hutumika pamoja na vitenzi vikuu ili kuwa na maana kamili. Mifano: ***alikuwa*** akila, ***angali*** anasoma n.k.
3. ***Vitenzi vikuu:*** Hubeba maana kuu ya katika sentensi, hutumika pamoja na vitenzi visaidizi. Mifano: alikuwa ***akiimba***, anaweza ***kusoma*** n.k.
4. ***Vitenzi sambamba:*** Hutumika pamoja katika sentensi moja vikifuatana. Mifano: sikumwambia apike chakula, nilimwona akiiba n.k.

## Zoezi la 3

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tungeni sentensi tano tano kwa usahihi kwa kila aina za vitenzi zifuatazo.*

**Kwa mfano:** Kitenzi kikuu

**Sentensi:** Mtahini <u>*amesahihisha*</u> mitihani yote ya wanafunzi wake.

1. Kitenzi kikuu
2. Kitenzi kisaidizi

## 18.5.1 Uundaji wa vitenzi

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, jaribuni kuunda vitenzi kwa kutumia maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi zinazofuata kisha mtunge sentensi sahihi kwa kutumia vitenzi mtakavyounda.*

**Mfano 1:** <u>*Upendo*</u> alio nao kwa mtoto wake unashangaza.

***Jibu:*** Kutokana na nomino '*upendo*' tunaweza kuunda kitenzi '*penda*'.

***Mfano wa sentensi***: Mama wa kambo anam<u>*penda*</u> mtoto wake wa kambo.

**Mfano 2:** Mti <u>*mrefu*</u> ulikatwa na wanakijiji.

***Jibu:*** Kutokana na kivumishi '*mrefu*' tunaweza kuunda kitenzi '*refusha*'.

***Mfano wa sentensi***: Mchoraji aliu*refusha* mstari aliokuwa amechora.

1. Nitaenda sokoni kununua *ufagio* mwingine.
2. Huyu ndiye *mlezi* wa watoto wangu.
3. Nyumba *safi* itapakwa rangi kesho.
4. *Mchoro* huo utauzwa kwa pesa nyingi.
5. Rinda *fupi* alilonunua halimtoshi tena.

## Maelezo muhimu

Vitenzi vinaweza kuundwa kutokana na mizizi ya vivumishi na nomino.

**Kwa mfano:**

| | | |
|---|---|---|
| i) | **Kivumishi** | **Kitenzi** |
| | nadhifu | nadhifisha, nadhifika n.k. |
| ii) | **Nomino** | **Kitenzi** |
| | eneo | enea, eneza n.k. |

**FAHAMU:** Kitenzi huundwa kutokana na maneno mengine kwa kuongeza viambishi awali au viambishi tamati kwenye mzizi wa neno linaloundwa.

## Zoezi la 4

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, undeni vitenzi kutokana na maneno yafuatayo kisha mtunge sentensi sahihi kwa kutumia vitenzi mtakavyounda.*

**Kwa mfano:** -safi

**Jibu:** Dada yangu mdogo aliya*safisha* madirisha ya nyumba yetu.

1. -erevu
2. uchovu
3. mchezo
4. -nene
5. mfugaji

# Somo la 19: Mwongozo wa kuandika mjadala


## 19.1 Mjadala kuhusu ugonjwa wa Ukimwi

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tazameni picha na michoro hii kisha msome mjadala unaofuata kuhusu ugonjwa wa Ukimwi na mjibu maswali ya ufahamu.*










**Mwenyekiti:** Wananchi wenzangu, mabibi na mabwana mliotenga muda wenu kuwa hapa leo, hamjambo! Karibuni katika mjadala wetu wa leo. Mada ya mjadala wa leo inahusu ugonjwa wa Ukimwi. Bila kupoteza muda ningependa kumkaribisha msemaji wa kwanza ambaye ni Neza. Karibu Neza.

**Neza:** Asante mwenyekiti. Ningependa kwanza kufafanua maana ya neno UKIMWI. Hili ni neno ambalo limeundwa kwa silabi zinazosimamia '***U***pungufu wa ***KI***nga ***MWI***lini. Ugonjwa huu ni hatari sana na unaweza kumpata binadamu yeyote bila kujali jinsia wala hadhi ya kimaisha. Ugonjwa huu husababishwa na virusi hatari na sugu vya Ukimwi (VVU). Huu si ugonjwa wa kawaida kama yalivyo magonjwa mengine kama vile: homa, ukambi, utapiamlo, kipindupindu au kifuakikuu. Hii ni kwa sababu magonjwa mengine yanaweza kutibiwa lakini ugonjwa wa Ukimwi hauna tiba. Ndio maana watu duniani kote wanaombwa kujiepusha na ugonjwa huu kwa sababu ya usugu wake wa kutotibika. Nitakomea hapo kwa leo ili niwape wenzangu nafasi watueleze kuhusu namna ugonjwa huo unavyoweza kuambukizwa kwa watu wengine. Asante mwenyekiti.

**Mwenyekiti:** Asante Neza kwa utangulizi huo mzuri kuhusiana na maana ya UKIMWI. Ningependa kumkaribisha Ngabo naye atoe hoja zake. Karibu.

**Ngabo:** Asante mwenyekiti. Mimi ningependa kueleza kuhusu namna ambavyo mtu anaweza kuambukizwa ugonjwa wa Ukimwi. Kwanza, ni kupitia kwa kushiriki ngono na mtu aliyeambukizwa ugonjwa huo. Mtu yeyote, mkubwa au mdogo anapojiingiza katika vitendo vya ngono kiholela na mtu aliye na virusi vya Ukimwi hana budi kuambukizwa virusi hivyo. Njia nyingine ya kuambukiwa virusi hivi ni kupitia kwa matumizi ya pamoja ya vifaa vyenye makali kama vile: nyembe, sindano, visu n.k. Pindi unapotumia kifaa chochote kilichogusa damu ya mtu aliye na virusi vya Ukimwi, basi pia wewe unaweza kuambukizwa virusi hivyo iwapo damu yako itagusana na damu yake iliyo kwenye vifaa hivyo. Katika jamii zinazotekeleza tohara kwa wavulana wao, matumizi ya wembe mmoja au kisu kimoja kuwatahiri wavulana zaidi ya mmoja huwaweka katika hatari ya kuambukizwa virusi vya ugonjwa huo iwapo patakuwepo na mmoja miongoni mwa wavulana hao aliye na virusi hivyo. Njia nyingine ya kuambukizwa virusi vya ugonjwa huu hatari ni kutoka kwa mama mzazi aliye na virusi hivi hadi kwa mtoto wake kupitia kwa maziwa anayonyonya. Mwisho, kuchanganyika kwa damu ya mtu aliye na virusi vya Ukimwi pamoja na damu ya watu wasio na virusi hivyo ni njia nyingine ya kuambukizana ugonjwa huu. Hili linaweza kutokea katika ajali kama vile ya barabarani ambapo abiria wanaweza kuumia na kutokwa na damu na damu hiyo ikachanganyika. Naomba kukomea hapo kwa leo ili nimpe nafasi mwenzangu atufahamishe athari za ugonjwa huu hatari. Asanteni.

**Mwenyekiti:** Nakushukuru Ngabo kwa ufafanuzi wako kuhusiana na njia za kuambukizwa virusi vya Ukimwi. Sasa, ninamkaribisha Kayitare ili atufafanulie kuhusu athari za ugonjwa wa Ukimwi. Karibu Kayitare.

**Kayitare:** Asante sana mwenyekiti. Nashukuru kwa nafasi hii ya kuwaeleza kuhusu athari za ugonjwa wa Ukimwi. Virusi vya ugonjwa huu vinapoingia katika mwili wa binadamu huwa vinadhoofisha kinga ya mwili mzima dhidi ya magonjwa mengine. Kwa hivyo, mtu aliyeathirika na virusi vya Ukimwi huweza kupatwa na magonjwa mengine kwa haraka sana. Hii ni kwa sababu kinga ya mwili wake huwa imedhoofishwa kabisa. Mwathiriwa wa ugonjwa huu huwa mnyonge sana kwa kuwa mgonjwa kila mara. Athari nyingine ni

afya kudhoofika na mwathiriwa kukonda sana. Wengine hukonda kiasi cha kubaki mifupa mitupu. Virusi hivi huathiri mwili sana na kuumaliza nguvu kabisa. Pia, vipele huweza kutokea kwenye ngozi za baadhi ya waathiriwa jambo ambalo huwafanya kujikuna sana. Katika kujikuna huku, vipele hivi husambaa kwenye mwili wote na kuwa vikubwa. Vipele hivi huwasha sana. Kuna baadhi ya waathiriwa ambao huwa na kikohozi cha kudumu. Wao hukohoa sana na kwa sauti.

Fahamu kuwa huwezi kuambukizwa virusi vya Ukimwi kwa kuwasalimu walioathiriwa na ugonjwa huo wala kwa kula chakula kwa kutumia sahani zao au hata kwa kulala kwenye vitanda vyao. Je, Ukimwi una athari gani kwa jamii yetu? Kama nchi, Ukimwi hutupora wafanyakazi wenye elimu na ujuzi na kuirejesha jamii nyuma kimaendeleo. Pia, idadi ya mayatima na wajane huongezeka hivyo kuwa mzigo mkubwa kwa jamii. Asante mwenyekiiti.

**Mwenyekiti:** Asante Kayitare kwa maelezo yako. Namkaribisha Munyana atoe hoja zake kuhusiana na namna ya kujikinga dhidi ya virusi vya Ukimwi. Karibu Munyana.

**Munyana:** Asante sana mwenyekiti. Nitachukua tu dakika chache nizungumzie njia za kujikinga dhidi ya ugonjwa wa Ukimwi. Kwa sababu ugonjwa huu hauna tiba, ni bora kila mtu afahamu namna ya kujikinga dhidi ya kuupata. Vitendo vya kushiriki ngono kiholela husababisha maambukizo ya virusi hivi, kwa hivyo kila mtu mzima anayeshiriki ngono anashauriwa kuwa na mpenzi mmoja pekee. Mke awe na mume mmoja pekee na mume awe na mke mmoja na wote wawili wawe waaminifu kwao. Tabia za vijana kujiingiza katika kushiriki ngono kiholela ni kujiletea balaa katika siku za usoni. Njia nyingine ya kujikinga dhidi ya ugonjwa huu ni kuhakikisha kuwa vifaa vyenye makali kama vile: nyembe, sindano na makasi unavyotumia havijatumiwa na mtu mwingine. Mwisho, mwanamke aliye mjamzito, ahakikishe kuwa amepimwa ili kubaini iwapo ana virusi vya Ukimwi ndiposa aweze kujua iwapo atamnyonyesha mtoto wake au atatafuta njia mbadala za kumlisha mtoto huyo. Asante mwenyekiti.

**Mwenyekiti:** Asante Munyana kwa mawazo yako. Namkaribisha Bagabo ambaye ndiye msemaji wa mwisho wa mjadala huu ili naye atoe hoja zake. Karibu.

**Bagabo:** Asante mwenyekiti. Mimi ningependa kuwaeleza kuwa iwapo mtu amepimwa na akapatikana ana virusi vya Ukimwi, asife moyo. Hii ni kwa sababu kuna tembe ambazo zinapatikana katika hospitali zetu ambazo husaidia kupunguza makali ya virusi vyenyewe. Kwa kumeza tembe hizi, mwathiriwa wa Ukimwi anaweza kuishi kwa miaka mingi sana. Pia, iwapo una ugonjwa huu, ili uweze kuishi kwa muda mrefu unashauriwa kula chakula kilicho na madini yote muhimu kwa mwili, kula matunda kwa wingi pamoja na kufanya mazoezi ya mwili. Haya huusaidia mwili kupata uwezo wa kupigana na maradhi mengine hivyo mwathiriwa huweza kuishi kwa muda mrefu. Jambo la mwisho ambalo ningependa kuwashauri waathiriwa wa Ukimwi ni kuwa na moyo mtulivu, amani na utulivu wa kiakili huweza kumsaidia mtu kupata nafuu ya kumsogeza mbele kimaisha. Asante mwenyekiti.

**Mwenyekiti:** Asanteni nyote kwa kushiriki katika mjadala wa leo. Natumai kuwa sote tumeweza kupata uelewa mpana kuhusiana na ugonjwa wa Ukimwi. Tumieni maarifa mliyopata hapa leo kuwaelimisha watu wote uwajuao. Asanteni na ninawatakia kila la heri.

## Maswali ya ufahamu

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, someni tena mjadala kuhusu athari za ugonjwa wa Ukimwi kisha mjibu maswali yafuatayo.*

1. Eleza maana ya neno UKIMWI.
2. Fafanua maana ya VVU.
3. Jadili namna ambavyo mtu anaweza kuambukizwa virusi vya ugonjwa wa Ukimwi.
4. Kwa nini ugonjwa wa Ukimwi ni tofauti na magonjwa mengine?
5. Eleza namna mtu anavyoweza kujikinga dhidi ya kuupata ugonjwa wa Ukimwi.
6. Jadili athari za ugonjwa wa Ukimwi kwa mtu binafsi.
7. Kwa nini mwili wa mwathiriwa wa ugonjwa wa Ukimwi hudhoofika sana?
8. Jadili athari za ugonjwa wa Ukimwi kwa jamii na taifa.
9. Utamshauri vipi mwathiriwa wa ugonjwa wa Ukimwi?
10. Unadhani kwa nini ni muhimu kwa kila mtu kupimwa kuhusiana na ugonjwa wa Ukimwi?

## 19.2 Msamiati kutokana na mjadala husika

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tafuteni msamiati mpya kutoka katika mjadala mliosoma hapo awali kuhusu athari za ugonjwa wa Ukimwi kisha mweleze maana zake. Zingatieni muktadha wa mjadala huo. Mnaweza kutumia kamusi inapohitajika.*

**Kwa mfano:**

***virusi*** – viini vinavyosababisha ugonjwa

### Zoezi la 1

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, elezeni maana ya msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi zifuatazo kisha mtunge sentensi sahihi kwa kutumia msamiati huo kama ulivyotumika katika mjadala mliosoma kuhusu athari za ugonjwa wa Ukimwi.*

**Kwa mfano:** Kinga dhidi ya ugonjwa wa Ukimwi imependekezwa kwa kila mtu.

**Maana:** ***kinga*** – jambo la kusaidia kujiepusha na madhara au ugonjwa

***Matumizi katika sentensi:*** Nimeamua kufuata ushauri wa daktari kuhusu ***kinga*** dhidi ya ugonjwa wa Malaria.

1. Ugonjwa wa Ukimwi unaweza kumpata mtu wa ***hadhi*** yoyote.
2. Neno UKIMWI lina ***silabi*** tatu.
3. Ugonjwa wa ***kipindupindu*** ni hatari kwa watoto wadogo.
4. Mwanangu anaugua ugonjwa wa ***ukambi***.
5. Kushiriki ngono ***kiholela*** kunaweza kumwingiza mtu katika matatizo mengi.
6. Jirani yetu ni ***mwathiriwa*** wa ugonjwa wa Ukimwi.
7. ***Mayatima*** wamekuwa wengi katika mkoa wetu.
8. ***Wajane*** wote watasaidiwa na rais kukidhi mahitaji yao kifedha.
9. Ugonjwa wa Ukimwi huambukizwa kwa ***virusi***.
10. Baadhi ya waathiriwa wa ugonjwa wa Ukimwi hupata ***vipele*** mwilini.

## 19.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, jadilini kuhusu mwongozo wa kutunga mjadala kwa kuzingatia mambo muhimu yanayofaa kuwepo kwa kurejelea mifano ya mijadala mliyosoma hapo awali. Kila kikundi kiwasilishe matokeo yake ya majadiliano mbele ya wanafunzi wenzao.*

**Kwa mfano:** Mjadala huhusisha mtazamo mmoja wa kujenga hoja.

## 19.4 Kusikiliza na kuzungumza: Kutunga mjadala

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, tungeni mjadala kuhusu manufaa ya malezi bora. Kila kundi liwasilishe mdahalo wake mbele ya wanafunzi wenzao.*

### Zoezi la 3

*Katika makundi ya wanafunzi sita sita, igizeni mjadala mliosoma hapo awali kuhusu athari za ugonjwa wa Ukimwi kwa kuzingatia mambo muhimu kuhusiana na mjadala. Kila kundi liwasilishe maigizo yake mbele ya wanafunzi wenzao.*

## 19.5 Sarufi

### Maana ya kiwakilishi

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, chunguzeni maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi zifuatazo katika umoja na wingi kisha mueleze maneno hayo ni ya aina gani.*

**Mfano 1:**

***Sentensi yenye nomino:*** *Mwanafunzi* anasoma kwa bidii sana.

***Sentensi isiyo na nomino:*** *Yeye* anasoma kwa bidii sana.

**Jibu:** Neno '*yeye*' katika sentensi isiyo na nomino limetumika badala ya nomino. Yaani, linawakilisha nomino '*mwanafunzi*'.

**Mfano 2:**

***Sentensi yenye nomino:*** *Kitabu* hiki kitasomwa shuleni kesho.

***Sentensi isiyo na nomino:*** *Hiki* kitasomwa shuleni kesho.

**Jibu:** Neno '*hiki*' katika sentensi isiyo na nomino limetumika badala ya nomino. Yaani, linawakilisha nomino '*kitabu*'.

**Mfano 3:**

***Sentensi yenye nomino:*** *Mama* anapika jikoni.

***Sentensi isiyo na nomino:*** Anapika jikoni.

**Jibu:** Kiambishi '*a*' katika sentensi isiyo na nomino kimetumika badala ya nomino. Yaani, kinawakilisha nomino '*mama*'.

**Mfano 4:**

***Sentensi yenye nomino:*** <u>*Msichana*</u> mrembo ameimba vizuri sana.

***Sentensi isiyo na nomino:*** <u>*Mrembo*</u> ameimba vizuri sana.

**Jibu:** Neno '*mrembo*' katika sentensi isiyo na nomino limetumika badala ya nomino yenyewe. Yaani, linawakilisha nomino '*msichana*'.

## Maelezo muhimu

Neno au kiambishi ambacho hutumika badala ya nomino katika sentensi huitwa ***kiwakilishi***.

**Aina za viwakilishi:**

1. Viwakilishi vya nafsi. Mfano: ***<u>Mimi</u>*** *ninasoma kwa bidii.*
2. Viwakilishi vya ngeli. Mfano: ***<u>Ki</u>****nasomwa na wanafunzi shuleni.*
3. Viwakilishi vya sifa. Mfano: ***<u>Mrembo</u>*** *anaimba vizuri sana.*
4. Viwakilishi vimilikishi. Mfano: ***<u>Langu</u>*** *limeuzwa kwa bei rahisi.*
5. Viwakilishi viulizi. Mfano: ***<u>Wangapi</u>*** *wamefika kwenye mkutano?*

## Zoezi la utafiti

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, tafitini kuhusu aina zifuatazo za viwakilishi kisha mvitolee mifano miwili miwili katika sentensi mbili mbili sahihi.*

a) Viwakilishi virejeshi

b) Viwakilishi vya pekee

**Kwa mfano:**

***Kiwakilishi kirejeshi:*** <u>*Ambaye*</u> aliwasili ni wetu. (*Neno* ***'ambaye'*** *ni kiwakilishi kirejeshi kwa sababu kinaturejesha kwenye nomino husika.)*

***Kiwakilishi cha pekee:*** '<u>*Chote*</u>' kililiwa na watoto wake. (*Neno* ***'chote'*** *ni kiwakilishi cha pekee kwa sababu kinazungumzia nomino husika pekee.)*

## Zoezi la 4

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, tumieni viwakilishi sahihi badala ya nomino zilizotumika katika sentensi zifuatazo.*

**Kwa mfano:** <u>*Mwalimu*</u> anafundisha vizuri.

**Jibu:**

i) <u>***A***</u>nafundisha vizuri. (*kiwakilishi cha nafsi*)

***au***

ii) <u>***Yeye***</u> anafundisha vizuri. (*kiwakilishi cha nafsi*)

1. <u>*Kiatu*</u> kilichoraruka kimeshonwa tena.
2. <u>*Mtoto*</u> ambaye alikuwa akilia amenyamaza.
3. <u>*Nguo*</u> zote zimefuliwa zikawa safi na kuanikwa.
4. <u>*Magari*</u> mangapi yameagizwa kutoka ng'ambo?
5. <u>*Mafuta*</u> yake yamemwagika sakafuni.

## 19.5.1 Uundaji wa viwakilishi

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jaribuni kuunda viwakilishi kwa kutumia maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi zinazofuata kisha mtunge sentensi sahihi kwa kutumia viwakilishi mtakavyounda.*

**Mfano 1:** Mwalimu <u>*mkali*</u> amefika darasani na kiboko.

***Jibu:*** Kivumishi '*mkali*' kinaweza kutumika kilivyo kama kiwakilishi.

***Mfano wa sentensi***: <u>*Mkali*</u> amefika darasani na kiboko.

**Mfano 2:** Mvulana <u>*ambaye*</u> amepita mtihani ni wa shule yetu.

***Jibu:*** Kivumishi '*ambaye*' kinaweza kutumika kilivyo kama kiwakilishi.

***Mfano wa sentensi***: <u>*Ambaye*</u> amepita mtihani ni wa shule yetu.

1. Jicho <u>*langu*</u> linauma sana.
2. Watoto <u>*wazuri*</u> bado hawajazaliwa.
3. Meno <u>*yetu*</u> yatang'olewa kwa kuwa yanauma.
4. <u>*Zipi*</u> zilijengwa na waashi hawa?
5. Vyuma <u>*ambavyo*</u> vimenunuliwa vitatumika kesho.

### Maelezo muhimu

Vivumishi vinaweza kutumika kama viwakilishi moja kwa moja katika umbo lao bila kuongeza viambishi awali au viambishi tamati.

**Kwa mfano:**

***Sentensi yenye kivumishi:*** Mtoto <u>*mkorofi*</u> amefukuzwa shule.

***Sentensi yenye kiwakilishi:*** <u>*Mkorofi*</u> amefukuzwa shule.

## Zoezi la 5

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tungeni sentensi kwa kutumia vivumishi vifuatavyo kama viwakilishi.*

**Kwa mfano:** *mchafu*

**Jibu:** *Mchafu* amekubali kuoga mwili.

1. mwekundu
2. ndefu
3. safi
4. vyeusi
5. vikali

## Tathmini ya mada ya 4

## Zoezi la 1

1. Andika mifano miwili ya nomino za pekee.
2. Nomino zifuatazo ni za aina gani?
   a) Chuki
   b) Manukato
   ch) Uji
   d) Kitabu
   e) Ijumaa

## Zoezi la 2

1. Tunga mdahalo kuhusu hali ya usalama nchini.
2. *Onyesha vivumishi katika sentensi zifuatazo.*
   a) Mikate mitamu imenunuliwa.
   b) Viazi vipi vinachongwa?
   ch) Karamu kubwa imeandaliwa kwetu.
   d) Kikao hiki kitatufaa.
   e) Mwalimu mzee amefariki.

## Zoezi la 3

1. Ainisha vitenzi vya Kiswahili kwa kutolea mifano.
2. *Sentensi zifuatazo zimeundwa kwa maneno ya aina gani?*
   a) Mimi nitaondoka asubuhi.
   b) Maria amenipa kalamu mpya.
   ch) Daktari hodari atamtibu mgonjwa mahututi.

## Zoezi la 4

1. *Katika makundi ya wanafunzi wanane wanane, andaeni mdahalo kuhusu 'Uvivu ni adui wa maendeleo'.*
2. *Katika makundi ya wanafunzi wanane wanane, andaeni mjadala kuhusu umuhimu wa ushirikiano na uzalendo kwa Wanyarwanda.*

## Zoezi la 5

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tungeni sentensi tano sahihi kwa kutumia vivumishi visisitizi.*

**Kwa mfano:**
Mtoto *huyu huyu* ndiye aliyezaliwa jana usiku.

## Zoezi la 6

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, undeni vitenzi kutokana na vivumishi vifuatavyo kisha mvitungie sentensi sahihi kisarufi.*

**Kwa mfano:** -nene

**Jibu:** Dada *amenenepa* siku hizi.

1. safi
2. nadhifu
3. mwerevu
4. chafu
5. fupi

## Faharasa

**ari:** hamu ya kutaka kufanya jambo bila ya kushindwa
**asasi:** shirika la kutoa huduma kama vile: elimu au matibabu
**bomu:** silaha ambayo imetengenezwa ili kutoa mlipuko na husababisha uharibifu
**huhodhi:** hukusanya
**kikwazo:** pingamizi, kizingiti au kizuizi cha mafanikio au utekelezaji wa jambo fulani
**kuambukizwa:** kupatwa na ugonjwa
**mdahalo:** mazungumzo au majadiliano kati ya watu wengi wenye mitazamo tofauti kuhusu jambo fulani wanalozungumzia
**mikakati:** mipango mikubwa sana
**mshikamano:** hali ya kuwa na msimamo na ushirikiano katika kutimiza jambo fulani
**rushwa:** pesa au kitu chochote cha thamani anachopatiwa mtu mwenye uwezo au madaraka katika jambo fulani ili amfanyie mtoaji hisani au upendeleo
**sugu:** -enye tabia isiyoweza kubadilika kwa urahisi
**takwimu:** maelezo ya kihesabu yanayotumiwa kufafanua na kulinganisha ukweli wa matukio au jambo fulani
**tiba:** kitu cha kuponya magonjwa
**uasherati:** tabia ya kupenda sana kufanya ngono
**ubinafsi:** tabia ya mtu kujali maslahi yake pekee na kuyapuuza ya wengine
**usalama:** hali ya kutokuwepo hatari au fujo
**utu:** hali ya kuwa na tabia nzuri ya kibinadamu
**uzinifu:** tabia ya kupenda sana kufanya ngono
**vibiritingoma:** wanawake malaya
**waadilifu:** wenye maadili mema au tabia zinazokubalika katika jamii
**wapinzani:** watu wanaopinga jambo fulani au maoni fulani
**watetezi:** wanaotetea au wanaounga mkono jambo fulani

## Vitabu vya Rejea


BAKITA (2015); *Kamusi Kuu ya Kiswahili*; Longhorn Kenya Ltd; Nairobi, Kenya.

Mbaabu I. (1992); *Sarufi ya Kiswahili*; Longman; Nairobi, Kenya.

Mdee J.S. , Njogu K., na Shafi A. (2011) *Kamusi ya Kiswahili ya Karne ya 21*; Longhorn Kenya Ltd; Nairobi, Kenya.

Ntawiyanga S. na Kinya J. (2015); *Kiswahili kwa Shule za Rwanda, Kidato cha 2*; Longhorn Kenya Ltd; Nairobi, Kenya.

Said A. Mohammed (1980); Riwaya ya *Utengano*; Longhorn; Kenya.

Timothy M. Arege (2009); Tamthilia ya *Kijiba cha Moyo*; Longhorn; Kenya.

TUKI (2009); *Stadi za Lugha ya Kiswahili*; Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.

Waihiga G. na Wamitila K. W. (2013); *Chemchemi za Kiswahili, kidato cha 3*; Longhorn Kenya Ltd; Nairobi, Kenya.

Waihiga G. na Kagwa F. M. (2003); *Darubini ya Kiswahili*; Phoenix Publishers; Nairobi, Kenya.

Walibora K. (2002); Riwaya ya *Siku Njema*. Longhorn; Kenya.